# Nipashe

Ijumaa Agosti 30, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 05780010

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper 0745 400 710 the guardian digital




## Ripoti kuhusu ‘unga’, simu gerezani yatua wizarani

UKURASA 2



UCHUMI

Wahitimu digirii wawabunia walima mboga Dodoma 'soko la kiganjani' Ukurasa 19

BUFE

Ijumaa Agosti 30, 2019 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

MVUTANO WA CHINA, MAREKANI

Huawei inabuni mfumo mpya wa ‘simu janja’ kuziacha Google, Apple

Ukurasa 14

SADC DAR & TANZANIA YA VIWANDA

Wahandisi, wawekezaji wanaibukia mayowe serikali iwafanye sehemu ya miradi mikubwa

Ukurasa 16


UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UKURASA 13

# Kigogo CCM akataa uteuzi

UKURASA 4



Rais John Magufuli, akiteta jambo na Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, baada ya kuhutubia Mkutano wa Sita wa Jukwaa la Uongozi Afrika, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Rais mstaafu wa Nigeria, Jenerali Olusegun Obasanjo. **PICHA: IKULU.**

# JPM ataja sababu 3 za umaskini Afrika

**ASEMA** masalia ya fikra za kikoloni ni tatizo sugu, Mkapa abainisha suluhisho lake...*Endelea uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### CUF YALIA UPENDELEO WA MIKUTANO KISIASA

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimeelezea kushangazwa na upendeleo wa mikutano kwa baadhi ya vyama vya siasa huku vingine vikizuiwa kufanya hivyo...

UKURASA WA 5

### MADUKA YANAYOUZA DAWA HOLELA YABANWA

SERIKALI imeyanyooshea kidole maduka binafsi ya dawa kwa uuzaji holela wa dawa za kiuavijasumu (antibiotics) na za kusaidia wajawazito wakati wa...

UKURASA WA 5

### HASUNGA: KUNA ZIADA YA CHAKULA



SERIKALI imesema hali ya chakula nchini ni nzuri baada ya uzalishaji wa mazao ya chakula kufikia tani 16,408,309 zaidi ya mahitaji, ambayo ni...

## Amnyonga mke wake kisha naye kujiua

UKURASA 2

MICHEZO **MAYANGA ATOA SIRI ‘KUIPAPASA’ YANGA** UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6




Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Mhandisi Hamad Masauni, akizungumza wakati wa kufunga semina ya usalama wa matairi na mfumo wa breki, iliyotolewa kwa askari wa usalama barabarani na wadau wengine kutoka taasisi zinahusika na usalama barabarani, lengo likiwa kudhibiti ajali za barabarani zinazosababishwa na uchakavu wa vipuri kwenye vyombo vya moto, jijini Dar es Salaam. **PICHA: WMNN**

# JPM ataja sababu 3 umaskini wa Afrika

**Romana Mallya na Agnes Shayo**

RAIS John Magufuli amesema mifumo mibovu ya usimamizi na masalia ya fikra za kikoloni ndizo sababu zinazolifanya Bara la Afrika kuendelea kuwa maskini licha ya utajiri wa rasilimali uliopo.

Aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa Jukwaa la Uongozi Afrika ambao ulihudhuriwa na viongozi wakuu wastaafu kutoka nchi mbalimbali barani.

Mkutano huo uliongozwa na Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa huku Rais mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, akiwa miongoni mwa waliohudhuria.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Rais Magufuli alisema tatizo la umaskini Afrika linatokana na usimamizi mbovu na matumizi bora ya rasilimali zilizopo.

"Nitataja sababu chache, nyingine nitawaachia wataalamu. Kwa maoni yangu sababu kubwa ya kwanza ni masalia ya fikra za kikoloni ambazo Afrika tumeendelea kubaki nazo, kimsingi hatukutafsiri vizuri dhana ya uhuru.

"Dhana ya uhuru haiwezi kutenganishwa na kujitegemea, kama hujitegemei, uhuru wako utakuwa mikononi mwa unayemtegemea," alisema.

Rais Magufuli alisema maana hasa ya kupigania uhuru ilikuwa kurejesha rasilimali hasa maliasili na kuwa na uamuzi kamili wa namna ya kuzisimamia na kuzitumia kwa manufaa ya kuleta ukombozi wa kiuchumi.

"Hii ndiyo namna pekee ya kulinda uhuru wa kisiasa, kutokana na kutoelewa dhana kamili ya uhuru, tukadhani kwamba watawala wetu wa zamani ndiyo wenye uwezo wa kutusaidia kusimamia na kuendeleza rasilimali zetu, huu ndiyo mwanzo wa ugonjwa wa utegemezi unaolitesa Bara la Afrika," alisema.

"Tusidanganyike, watawala wetu wa zamani hawawezi kugeuka usiku mzima na kuwa wajomba zetu na wakombozi wetu kiuchumi. Utegemezi huu ndiyo ulioimarisha mizizi na misingi ya ukoloni mamboleo ni lazima tuamke.

"Na kusimamia kuleta mageuzi ya kiuchumi ni tafsiri potofu ya msingi wa maendeleo. Mara nyingi, tumedanganyika na kudhani kuwa fedha ndiyo msingi wa

INAENDELEA UK. 8

# Aua mke kisha kujiua kwa sumu

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MKAZI wa kijiji cha Iponya katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, Paschal Clement (32), amemuua mkewe Ashura Paschal (30) kwa kumnyonga shingo kisha kujiua kwa kunywa sumu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Richard Abwao, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa moja jioni katika kijiji cha Iponya.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni wivu wa kimapenzi na kwamba kabla ya tukio hilo, wanandoa hao walikuwa na ugomvi huku mume akimtuhumu mkewe kuwa si mwaminifu kwenye ndoa.

Abwao alisema Paschal baada ya kutekeleza mauaji hayo, alijiiua kwa kunywa sumu ambayo mpaka sasa bado haijafahamika ni ya aina gani na kukutwa chumbani kwake akiwa amealala sakafuni.

"Ilikuwa saa moja jioni huko kijijini Iponya kata ya Kagongwa, Paschal Clement alimuua mkewe kwa kumnyonga shingoni kisha kumlaza kitanda na baadaye naye akajiua kwa kunywa sumu ambayo haijafahamika ni ya aina gani," alisema.

Kamanda Abwao alisema miili ya marehemu hao imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa uchunguzi zaidi wa daktari na uchunguzi utakapokamilika watakabidhiwa ndugu kwa taratibu za mazishi.

BENKI KUU YA TANZANIA

**KUSITISHWA KWA MNADA WA HADHARA WA MAGARI NA VIFAA VYA OFISI CHAKAVU BENKI KUU TAWI LA ARUSHA ULIOPANGWA KUFANYIKA TAREHE 31-08-2019**

Benki Kuu ya Tanzania, Tawi la Arusha, inapenda kutoa taarifa kwa umma kuwa imesitisha mnada wa hadhara uliopangwa kufanyika siku ya **Jumamosi tarehe 31/08/2019 kuanzia saa 03:00** asubuhi katika majengo ya Benki Kuu yaliyopo KIBLA Kitalu namba 565 katika Jiji la Arusha.

**Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote ulioyojitokeza.**

**Mkurugenzi wa Tawi**
**Benki Kuu ya Tanzania – Tawi la Arusha**
**S.L.P. 3034**
**Arusha**

XXXXXX

# Serikali yapokea ripoti ya 'unga', simu gerezani

**Na Romana Mallya**

TUME iliyoundwa kuchunguza uingizaji wa simu na dawa za kulevya gerezani imekamilisha kazi na kukabidhi ripoti yake serikalini kwa hatua zaidi.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, aliliambia Nipashe juzi kuwa tume hiyo ambayo iliundwa miezi mitatu iliyopita, imeshakabidhi ripoti yake.

Machi 22 mwaka huu, Masauni aliagiza kuundwa kwa tume hiyo baada ya kutembelea gereza la Ruanda mkoani Mbeya na kubaini baadhi ya askari kwa kushirikiana na wafungwa wamekuwa wakiingiza simu na dawa za kulevya gerezani.

Kwa mujibu wa Masauni, ripoti hiyo ilikuwa na lengo la kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo magerezani na wameshakabidhiwa

INAENDELEA UK. 8

SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




# Mkakati waja kudhibiti wahamiaji haramu Dar

**Mary Geofrey na Jovin Lamwel**

MKOA wa Dar es Salaam, unakabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa wimbi la wahamiaji haramu ambao wamebainika kufanya shughuli zao katika nyumba za ibada, viwanda, shule na makazi ya watu.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam, Novaita Mrosso, wakati wa uzinduzi wa mkakati wa udhibiti wa uhamiaji haramu utakaotekelezwa katika kila kaya, mitaa na kata zote.

Alisema idadi ya wahamiaji haramu wanaokamatwa kila mwaka inaongezeka kutoka 1,010 waliokamatwa mwaka 2016 hadi 1,232 waliokamatwa mwaka jana.

Alisema wahamiaji hao wanatoka Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Malawi, Burundi na Somalia na wapo waliooa na kuolewa na Watanzania.

"Mkakati huu utasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya wahamiaji haramu katika mkoa wetu kwa sababu tutakuwa tumewadhibiti kuanzia ngazi ya kaya hadi mtaa ambako walikuwa wakijificha," Mrosso alisema.

Alisema wahamiaji hao wamekuwa wakijichanganya mitaani na kupata nyaraka za serikali ili kupata uhalali wa kuendelea kuishi nchini.

Alisema kwa sababu hawatambuliki pia wamekuwa wakinufaika na huduma muhimu zinazotolewa kwa Watanzania kama elimu bure, mikopo na vitambulisho vya umachinga.

Alisema wamesababisha migogoro ya ardhi, matukio ya uhalifu, msongamano magerezani na kuipa serikali mzigo wa kuwalisha.

Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, akizindua mkakati huo, alisema utekelezaji wake utashirikisha viongozi wa vitongoji, mitaa na kata kuhakikisha wanawabaini wahamiaji haramu wote.

"Leo nazindua mkakati mpekenyo, utakaopekenyua kila kaya na kufukunyua kila mtaa, ili kufahamu kila mtu anaishi wapi na anafanya shughuli gani, na wahamiaji haramu wanaoishi nchini kinyume cha taratibu wakamatwe na kuchukuliwa hatua," alisema.

Alisema ipo haja ya watendaji wa mitaa kurejesha daftari la wakazi ili kusaidia kuwa na taarifa za watu wao na shughuli wanazofanya.

"Kuelekea uchaguzi mkuu ujao mwakani kuna umuhimu wa kuwa na daftari hili la wakazi ili watu watambulike kwa sababu wanaweza kuingia kwenye mitaa kwa lengo la kuvuruga amani," Makonda alisema.

Kadhalika, Makonda aliahidi kuwapatia kompyuta maofisa uhamiaji kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi wa shughuli hizo.

Alizitaka wilaya za mkoa huo, kurudisha kompyuta nane waliozopatiwa kila wilaya kwa ajili ya kusaidia kutoa vibali vya ujenzi ndani ya mwezi mmoja kutokana na kushindwa kutekeleza azma hiyo.

Aidha, alilitaka Jeshi la Polisi kurudisha kompyuta nyingine 20 zilizotolewa kila wilaya ya kipolisi kwa ajili ya kuchukua taarifa za mahabusu, lakini zimekuwa hazitumiki na badala yake wanaendelea kutumia madaftari kuchukua taarifa.



Washtakiwa Evans Aveva (wa pili kushoto), Geofrey Nyange 'Kaburu' (wa pili kulia) na Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Simba, Zacharia Hans Poppe, wakitoka kizimbani baada ya kesi inayowakabili kuahirishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# CUF yalia upendeleo mikutano kisiasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimeelezea kushangazwa na upendeleo wa mikutano kwa baadhi ya vyama vya siasa huku vingine vikizuiwa kufanya hivyo.

Kutokana na hali hiyo, kikimtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, kutekeleza agizo la Rais John Magufuli la kupiga marufuku mikutano ya vyama vya siasa kwa vyama vinavyokiuka vinginevyo na wao wataanza kufanya mikutano nchi nzima.

Akizungumza na waandishi wa habari jiji hapa, Makamu Mwenyekiti wa CUF (Tanzania Bara), Maftaha Nachuma, alisema agizo hilo la Rais Magufuli hivi sasa linatekelezwa kwa upendeleo.

Nachuma alisema wakati vyama vingine vimekuwa vikitii kutekeleza agizo hilo, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimekuwa kikiendelea na mikutano katika maeneo mbalimbali ya nchi.

"IGP inabidi aliangalie hili kwani agizo la Rais Magufuli ni kwa vyama vyote vya siasa nchini na si wao kuendelea kufanya mikutano katika maeneo yao lazima haki izingatiwe. Kila chama kina haki zake za msingi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa," alisema Nachuma.

Alisema kama Jeshi la Polisi litaendelea kuipendelea CCM na kuiachia kuendelea kufanya mikutano ya kisiasa, CUF pia itaanza kufanya mikutano hiyo kuzunguka nchi nzima.

"Leo (jana) hii tulikuwa tufanye mkutano wa chama chetu katika maeneo ya Vingunguti jijini Dar es Saalam, lakini Jeshi la Polisi limetukataza na kusema kuwa hilo ni agizo la Rais Magufuli lakini wenzetu CCM wanajiandaa Agosti 31 (leo) watakuwa na mkutano kule Mtwara na mgeni rasmi atakuwa Mzee (Mizengo) Pinda (Waziri Mkuu mstaafu)," alisema Nachuma.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana ya CUF, Hamidu Bobali, ambaye pia ni Mbunge wa Mchinga, alisema CCM kimekuwa kikifanya mikutano kwa kutumia ujumbe wa Tanzania ya Kijani.

Bobali alisema mikutano hiyo ambayo CCM imekuwa ikiifanya watu wakihoji wanadai kuwa wanakwenda kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya chama chao.

"Kama wao wanakwenda kukagua utekelezaji wa ilani kwa nini na sisi kule ambako kuna diwani wetu, mbunge wetu tusiruhusiwe kwenda kuona kuna ahadi zipi zimetekelezwa katika eneo hilo?" Alihoji Bobali.

Naibu Katibu Mkuu wa CUF Tanzania Bara, Magdalena Sakaya, ambaye ni Mbunge wa Kaliua, alisema Tanzania ni nchi ya mfumo wa vyama vingi, hivyo hakuna sababu ya polisi kuendelea kukibeba chama kimoja.

"Katika mikutano hii ambayo inafanywa na watu wa CCM katika maeneo mbalimbali wamekuwa wakiitumia kuwatisha wananchi kuwa wakichagua chama kingine watakoma. Sasa tunawataka hawa makatibu wa kata wa CCM pamoja na mabolozi wakome kuwatisha wananchi. Wawaache wachague viongozi kwa utashi wao," alisema Sakaya.

TAIFA STARS vs BURUNDI
SEPTEMBA 8, 2019 • UWANJA WA TAIFA

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# Katibu Mkuu CCM: Sitaki tena uteuzi

## Azungumzia ajira hewa CCM



"Hakuna kazi yoyote nitaifanya baada ya kazi hii, sitagombea cheo chochote cha kisiasa na sitakubali uteuzi wowote wa kisiasa katika nchi hii baada ya nafasi hii."

**Na Enock Charles**

KATIKA sehemu ya pili ya mahojiano haya jana, Dk. Bashiru Ally, alieleza namna Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilivyotekeleza ahadi ya kutoa Sh. milioni 50 kila kijiji/mtaa.

Vilevile, Katibu Mkuu huyo wa CCM alizungumzia kuhusu hatima ya vigogo waliofuja mali za chama hicho na changamoto zinazoukabili mfumo wa vyama vingi nchini.

Leo katika sehemu ya tatu ya mahojiano haya, Dk. Bashiru anabainisha kuwa hatawania nafasi yoyote ya kisiasa na hatakuwa tayari kuteuliwa kushika nafasi yoyote ya kisiasa baada ya miaka 10 ya uongozi alionao sasa ndani ya CCM.

Dk. Bashiru aliiambia Nipashe kuwa fedha hizo zimeshatolewa, lakini dhana ya utolewaji wake haijaeleweka kwa umma kutokana na ahadi hiyo kutotafsiriwa vyema. Endelea na mahojiano ya Nipashe na mtaalamu huyo wa sayansi ya siasa:-

**SWALI: Ulinukuliwa wiki iliyopita ukisema unatamani kurejea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kufundisha. Nini kilichokusibu?**

**DK. BASHIRU:** Hiyo ndiyo kazi ambayo mimi ninaipenda kuliko kazi nyingine na hiyo kauli niliitoa mbele ya watu ambao mimi nimeishi nao miaka mingi pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nilianza kazi pale mwaka 1997, mwanangu wa kwanza wakati huo alikuwa ana miaka miwili, sasa hivi anaelekea kuwa na miaka 23, ni binti mkubwa.

Pale ni kama vile sehemu kubwa ya maisha yangu na ujana wangu na nguvu zangu niliwekeza pale, nimesoma pale shahada ya kwanza, shahada ya pili, shahada ya tatu na nimefundisha kwa zaidi ya miaka 10 pale na wanafunzi wangu, walimu wenzangu, wafanyakazi wenzangu, marafiki zangu.

Kwa hiyo, ni kweli na nilikuwa nazungumza kwa hisia kwamba natamani kurudi pale kufundisha kwa sababu hii kazi (Katibu Mkuu wa CCM) ni ya muda, si ya kudumu, kazi ambayo nimeiomba ya kudumu ni ya kuwa mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Na tamaa yangu ipo kule kesho au kesho kutwa au baada ya miaka 10 baada ya kazi hii, nitaifanya, hakuna kazi yoyote nitaifanya baada ya kazi hii, sitagombea cheo chochote cha kisiasa baada ya kazi hii katika nchi hii baada ya kazi hii na sitakubali uteuzi wowote wa kisiasa katika nchi hii baada ya nafasi hii na bado umri wangu unaniruhusu.

**SWALI: Kuna baadhi ya viongozi ambao wamekuwa wakilalamikiwa kutokuendana na kasi ya Rais John Magufuli. Unalizungumziaje hili ukiwa kiongozi mkubwa ndani ya chama?**

**DK. BASHIRU:** Kasi ya Rais Magufuli ni kubwa na wengi wanaanza kuendana na kasi yake, si kama alivyoanza miaka minne iliyopita.

Miaka minne iliyopita, kulikuwa na uzito, kulikuwa na kusitasita ndani ya watendaji wa chama na serikali, kulikuwapo na hali ya mazoea ya kuendesha mambo bila kusimamiwa kwa karibu.

Kulikuwapo na vitendo vya ubadhirifu, kulikuwa na uzembe, sasa miaka minne baadaye, mambo yamebadilika sana na hali inaridhisha sana, wengi wameanza kushika kasi.

Lakini, bado kuna baadhi ni wazito, hao lazima watasimamiwa na wengine wanapewa mafunzo, wengine wanaadhibiwa kwa mujibu wa sheria, wengine wanaondolewa kwenye nafasi zao na zoezi hilo litaendelea.

**SWALI: Kuna watu ndani ya CCM wameonyesha wazi kutofautiana na mwenyekiti wa chama. Je, chama kitachukua hatua gani dhidi yao?**

**DK. BASHIRU:** Hawapo wasiokubaliana na mwenyekiti kwa sababu ili uweze kujua hawa hawakubaliani na mwenyekiti, ni kwenye vikao na mimi ndiyo Katibu Mkuu wa CCM na ndiye katibu wa vikao vyote.

Tunakaa vikao vya usalama na maadili, kamati kuu kila baada ya miezi mitatu, na mwezi kesho tutafanya na hatujaacha kufanya kikao hata kimoja cha kikatiba, tunafanya halmashauri kuu.

Mimi tangu nimeteuliwa, nimeshahudhuria mikutano ya halmashauri kuu karibu mitatu na mwaka huu tumeshafanya mmoja na mwingine wa pili tutafanya, ni vikao viwili viwili kila mwaka.

Wakati wote pamekuwa na mwafaka katika vikao na sijamwona mjumbe yeyote anampinga mwenyekiti ingawa wapo wanaotofautiana naye kimawazo kwa sababu vikao vile siyo vya mahubiri, bali vya mijadala, tena wakati mwingine mijadala mikali.

**SWALI: Ni mambo yapi unajivunia toka ushike nafasi hii?**

**DK. BASHIRU:** Najivunia chama kuwa imara na madhubuti, najivunia uongozi jasiri na shupavu wa mwenyekiti wetu na makamu wake wawili Zanzibar na Bara, najivunia ushauri wao, najivunia busara zao, najivunia maelekezo yao.

Ni viongozi ambao sijutii kufanya nao kazi, lakini pia najivunia wanachama ambao wameniunga mkono pamoja na ugeni wangu, mimi ni mgeni kweli, nafasi kubwa ambayo nimeishika ya uongozi ndani ya chama ni kuwa Katibu Mwenezi wa Kata ya Katerero.

Sasa, kupanda kutoka kuwa katibu mwenezi wa kata hadi kuwa Katibu Mkuu heee! Ni kupaa lakini bado wamenipokea, wapo waliokuwa na wasiwasi, lakini wameanza kuelewa, wameanza kunizoea na tumeanza kuelewana, nimezunguka karibu nchi nzima, mapokeo ninayoyapata nauona uhai wa chama.

Najivunia kuona wanachama wameanza kuelewa kuwa siasa za makundi ndiyo zimedhoofisha chama hiki. Kwa hiyo, vita dhidi ya siasa za makundi imeshika kasi ndani ya chama chetu.

Najivunia wanachama kujitolea nguvu zao na pesa zao na mawazo yao kuendesha chama, najivunia chama kinachosimamia serikali, najivunia chama kuendelea kupata ushindi katika uchaguzi mdogo, tangu nimeingia, sijapoteza hata mmoja, sana sana vishindo vya chama vimewakimbiza wapinzani, kila uchaguzi mdogo wanakwepa mpira kwapani.

Najivunia wanachama wengi wameanza kulipa ada, najivunia umoja wa vijana kwa kazi kubwa wanayoifanya kupitia mkakati wao wa Tanzania ya Kijani, ni mkakati mzuri sana, umesisimua vijana na wameanza kujiunga na chama chetu.

Najivunia umoja wa wanawake kwa kuhamasisha kina mama, najivunia kwa ufupi jumuiya zote tatu za chama; wazazi, vijana na wanawake.

**SWALI: Ni changamoto zipi ulizokutana nazo katika kipindi chako cha uongozi?**

**DK. BASHIRU:** Changamoto ya kwanza ni rasilimali, uendeshaji wa chama hiki ni gharama kubwa. Tunashindwa kutekeleza mipango yetu kwa sababu ya rasilimali hasa rasilimali fedha.

Tunayo mipango mingi ya kuimarisha chama, tunayo mipango mingi mizuri ya kuboresha maslahi ya watumishi wa chama lakini uwezo wetu bado uko chini.

Kwa hiyo, changamoto ni namna ya kuzalisha mali na kukusanya rasilimali fedha kwa njia ya michango, ada na miradi ili mapato yetu yawiane na mahitaji yetu, bado mahitaji yetu ni makubwa zaidi ya mapato yetu.

Na bado juhudi za kuongeza mapato yetu haziendi kwa kasi ukilinganisha na mahitaji, tunahitaji kuwa na programu za kufika kwa wanachama na wananchi kukijenga kiitikadi na kuwapa wanachama wetu mafunzo, kuwapa mafunzo watumishi wetu, kuboresha maslahi yao, lakini uwezo wetu bado ni mdogo.

**SWALI: Kulikuwa na taarifa za kuwapo kwa ajira hewa ndani ya chama. Kuna ukweli kuhusu hili?**

**DK. BASHIRU:** Siyo hilo tu, yalikuwapo matatizo ya aina hiyo, kulikuwa na ubadhirifu, kulikuwa na watu wameshabinafsisha mali za chama na hata mfumo wa kuajiri nao ulikuwa hauendani na mahitaji.

Wakati mwingine mfumo huo ulikuwa hauzingatii sifa, eeh! Tatizo hilo kwa sasa limeisha, tatizo lililobaki ni hilo nililosema kwamba uwezo wetu wa mapato ni mdogo.

**SWALI: Je, ni vipaumbele vipi vitazingatiwa katika maandalizi ya ilani ya uchaguzi wa mwaka 2020?**

**DK. BASHIRU:** Kamati Kuu imeshaunda kamati ya kuandaa nyaraka mbili kubwa; waraka wa kwanza ni mwelekeo wa sera za CCM kwa miaka 10 ijayo kuanzia mwaka 2020 unaoweka vipaumbele vya kisera kwa chama chetu kwa miaka 10.

Waraka uliopo sasa hivi unaisha mwaka 2020 ambao huu uliandaliwa wakati wa awamu ya nne na umetekelezwa kwa mafanikio makubwa sana.

Sasa mwelekeo wa sera za CCM mwaka 2020 hadi mwaka 2030 ndiyo unaandaliwa na kamati hiyo hiyo, ndiyo itakayoandaa ilani na kamati inaongozwa na Mzee Mangula kama Mwenyekiti na Makamu wake ni Makamu wa Rais Mama Samia.

Kwa hiyo, mchakato unaendelea, ninachofanya sasa hivi ni kuhamasisha umma kwa makundi mbalimbali, wafanye tathmini kwa ilani hii tuliyonayo, waweze kutupa maoni, nimeshakutana na vyama mbalimbali vya kitaaluma.

Nimekutana na chama cha madaktari, nimekutana na viongozi wa chama cha manesi, nimeshakutana na viongozi wa vyuo vikuu, nimeshasema hadharani yeyote ambaye ana maoni katika maeneo ambayo ni ya kimkakati kwenye eneo la uchumi kwa mfano kilimo.

Tungehitaji kupata maoni mazuri ya kisera ya namna ya kukifanya kilimo chetu kiwe na tija, kilimo chetu kiweze kuzalisha ziada na kiweze kutoa malighafi muhimu kwa viwanda vyetu.

Sekta ya muhimu ya pili ni viwanda, viwanda vya aina gani tuvijenge? Tuna matatizo, kwa mfano kwenye kilimo mazao yetu mengi tunayauza yakiwa ghafi kwa bei ya chini sana na wakulima wetu hawawezi wakanufaika kwa jasho lao kwa sababu hakuna viwanda vya kusindika yale mazao yao.

Kwa hiyo, tunaomba vyombo vya habari mtusaidie kutoa taarifa kwa umma kwa sababu zoezi hili la kutengeneza ilani lazima liwe shirikishi, yeyote mwenye mawazo anaweza akaja moja kwa moja ofisini kwangu, mimi ndio ninaratibu na ndio katibu wa kamati hiyo.

**SWALI: Kwa tathmini yenu, utekelezaji wa ilani ya CCM 2015-2020 ni kwa kiwango gani?**

**DK. BASHIRU:** Eeeh, bado tuna mwaka mzima na kasi yetu si unaiona. Ninachoweza kusema, bado tuna mwaka mzima na yote tuliyoahidi kwenye ilani hiyo tuna uhakika yatatekelezwa yote na mengi tumeshaanza vizuri kuyatekeleza, hakuna eneo ambalo tuko nyuma, mengine tuko mbele ya matarajio.

Mafanikio tuliyopata yapo ya aina mbili; kuna maendeleo yanayoonekana kwa miundombinu na yanashikika, barabara mijini na vijijini, usambazaji wa maji, sekta ya elimu, afya, miundombinu ya bandari, reli, viwanja vya ndege, mashirika yetu ambayo tumeyafufua ya simu ya ndege, Tanesco, umeme, mawasiliano ya kimtandao, sekta zote tumefanya vizuri, hayo unaweza ukayahesabu.

Yako yasiyohesabika na yasiyopimika kwa uzito, kwa mfano amani. Nchi yetu imeendelea kuwa na sifa hiyo ya kisiwa cha amani, huwezi ukapima.

Kupambana na rushwa na ufisadi ni vigumu sana kupima, sana sana utaona kutokana na kuongezeka kwa kodi na pesa nyingi kukusanywa na kupelekwa kwenye maendeleo, lakini rushwa ilikuwa imekuwa kikwazo cha haki kwa watu wengi.

Nidhamu katika utumishi wa umma huwezi ukaipima tani ngapi, lakini kila mmoja anafurahia watumishi wa umma kuwajibika na kuwa na nidhamu, mshikamano wa kitaifa na umoja wa kitaifa.

Bado kuna majaribio ya watu kuwabagua wenzao lakini watu wanajua kabisa hapa haikubaliki, ubaguzi ni dhambi katika Tanzania na ni kosa la kifalsafa na kisiasa, siyo la jinai tu. Hata kisiasa, kumbagua mtu kwa namna yoyote ni kosa.

Kulinda rasilimali zetu; kulikuwa na mchezo hapa watu wanachezea ardhi yetu, wanachezea madini, wanachezea samaki wetu, wanyama wetu, misitu yetu, sasa uharibifu huo haupo tena, leo tembo wanalindwa vizuri na wameongezeka. Ilani ya CCM inatekelezwa kwa sababu wako salama.

HABARI KITAIFA

# Maduka yanayouza dawa holela yanyooshewa kidole

**Na Devota Mwachang'a**

SERIKALI imeyanyooshea kidole maduka binafsi ya dawa kwa uuzaji holela wa dawa za kiuavijasumu (antibiotics) na za kusaidia wajawazito wakati wa kujifungua bila cheti cha daktari.

Serikali imesema dawa hizo hutumiwa kwa matumizi yasiyo sahihi ikiwamo kutolea mimba.

Naibu Wziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndungulile, amewaonya wamiliki wa maduka hayo watakaobainika katika ukaguzi utakaofanywa kupitia utaratibu na ukaguzi uliowekwa, watachukuliwa hatua za kisheria.

Aliyasema hayo alipokutana na Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawalilishi Zanzibar waliotembelea ofisi za Mamalaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) jijini Dar es Salaam jana.

"Zipo dawa nyingi zenye matumizi zaidi ya moja, kwa dawa za kiuavijasumu na nyingine ambazo hutolewa bila cheti cha daktari zimebainika kuleta madhara kwa watumiaji, mfano ni dawa aina ya Mistoprostol... hii inatumiwa vibaya kwa kutoa mimba badala ya matumizi yake sahihi ya kumuongezea uchungu mama anayetaka kujifungua, na kumsaidia asitokwe na damu nyingi baada ya kujifungua," amesema.

Kwa mujibu wa Dk. Ndugulile, madhara yatokanayo na matumizi ya dawa hii ni pamoja kifo, hivyo kumekuwapo na vifo vingi vya wanawake/wajawazito wanaotumia dawa vibaya kwa lengo la kujaribu kutoa ujauzito.

Aidha amesema: "Wajibu wa serikali ni kulinda usalama wa maisha ya wananchi, hivyo tunadhibiti kwa kuchukua hatua, si kwa kuondoa kutotumika bali kuweka utaratibu mzuri zaidi wa kuisimamia dawa kuhakikisha zinatolewa hospitali tu siyo madukani kama ilivyo dawa zingine za maumivu ikiwemo Pethdine ambazo watu huzitumia kama dawa za kulevya."

Aidha, ameeleza kuwa dawa ya Misoprostol itadhibitiwa kuanzia uagizaji, usambazaji na utumiaji wake hospitali kwa kuzingatia ni mgonjwa gani anastahili kupewa na kwa kiwango gani.

Hatua nyingine ni kuziondoa katika mfuko wa dharura wa mama mjamzito ambapo zilijumuishwa na vifaa vingine kama pamba, gloves.

Aliwatoa hofu wananchi kuhusu uwapo wa dawa zisizo bora kwa sababu TMDA ina maabara zenye ubora na ni ya kwanza barani Afrika. Dawa kabla ya kusambazwa huthibitishwa na mamlaka, na zisizo na ubora ufuatiliwa na kuondolewa sokoni.

Mkurugenzi wa Maabara TMDA, Dk. Danstan Hipolite, alibainisha kuwa pamoja na mafanikio kwenye udhibiti wa dawa, baada ya mabadiliko ya majukumu mamlaka inakabiliwa na changamoto ya kuandaa sheria mpya ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya sasa ya udhibiti ili pamoja na mambo mengine kuboresha masuala ya uendeshaji wa TMDA.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Bunge la Baraza la wawakilishi Z'bar, Mohamed Said Dimwa, aliishukuru serikali kwa kuwapa fursa kujifunza kupitia ziara hiyo.

**Wajibu wa serikali ni kulinda usalama wa maisha ya wananchi, hivyo tunadhibiti kwa kuchukua hatua, si kwa kuondoa kutotumika bali kuweka utaratibu mzuri zaidi wa kuisimamia dawa kuhakikisha zinatolewa hospitali tu siyo madukani kama ilivyo dawa zingine za maumivu ikiwemo Pethdine ambazo watu huzitumia kama dawa za kulevya**

# Hasunga: Nchi ina chakula cha kutosha

**Na Enock Charles**

SERIKALI imesema hali ya chakula nchini ni nzuri baada ya uzalishaji wa mazao ya chakula kufikia tani 16,408,309 zaidi ya mahitaji, ambayo ni tani milioni 13.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika mkutano na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na nafaka, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema kutokana na uzalishaji huo nchi ina ziada ya chakula, hivyo hakuna uwezekano wa Taifa kukumbwa na njaa.

"Tathmini iliyofanyika hivi karibuni inaonyesha uzalishaji wa mazao ya chakula ulifikia tani 16,408,309 ukilinganisha na mahitaji ya tani milioni 13 yaliyopo," Hasunga alisema.

Alisema tani 9,070,909 ni za mazao ya nafaka na tani 7,400,400 ni mazao yasiyokuwa ya nafaka na kusema kiwango hicho kimewezesha nchi kujitosheleza kwa mahitaji yake ya chakula kwa asilimia 119.

Akitaja mikoa iliyofanya vizuri katika uzalishaji wa chakula ni Ruvuma ambayo imezalisha chakula kwa asilimia 227 na Rukwa asilimia 220 na mkoa wa Songwe.

Alisema mikoa minane ambayo haijafikia uzalishaji mzuri ni Dar es Salaam uliozalisha asilimia tatu na halmashauri 44 ambazo zina upungufu wa chakula wa kati ya asilimia 90 na 99.

Kuhusu huduma za bima katika kilimo, waziri huyo alisema kwa sasa ni muhimu kilimo kikawa na bima ya mazao ili kuwalinda wanaowekeza katika mazao wasipate hasara pale wanapokutana na changamoto za ukame na magonjwa, hivyo kuwahamasisha wakulima kukata bima ya mazao.

Kuhusu changamoto ya urasimu katika biashara ya mazao, Hasunga alisema serikali imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa leseni na vibali ili kuwarahisishia wafanyabiashara wa mazao ya kilimo kupata vibali hivyo bila usumbufu.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Anjelina Mabula, amewataka wananchi kutovamia ardhi ya kilimo na kuitumia kwa makazi ili kuepuka uwezekano wa kukosekana kwa ardhi ya kilimo hapo baadaye.

**Tathmini iliyofanyika hivi karibuni inaonyesha uzalishaji wa mazao ya chakula ulifikia tani 16,408,309 ukilinganisha na mahitaji ya tani milioni 13 yaliyopo**


FARM RADIO INTERNATIONAL — REDIO KWA WAKULIMA

## VACANCY ANNOUNCEMENT

| | |
|---|---|
| Position title: | Country Representative |
| Position Location: | Arusha |
| Reports to: | Director of Operations-Africa |
| Application Deadline: | 16th September 2019 |

**Introduction to the Organization**

Farm Radio International (FRI) is a Canadian non-profit organization at the forefront of ICT-enabled extension and communication for scale. FRI's interactive rural radio approach addresses the information, communication and extension needs of millions of small-scale farmers, rural entrepreneurs and citizens.

In Tanzania, FRI currently works in thematic areas of agriculture value chains, livestock, climate information services and conservation agriculture, in collaboration with over 15 radio stations nationally, reaching out to millions of small scale farmers.

**Summary of the Position**

The Country Representative is a key position in Farm Radio International, with overall responsibility for leading and developing the growth of the organization within a specific country. The key expectations of a successful Country Representative are that they: create a strong reputation and profile for FRI; engage with government partners effectively; position FRI to participate in major rural development initiatives; secure new funding opportunities; lead the development of a strong, capable, high-functioning, well-coordinated and motivated staff team and; oversee the sound administration and financial management of FRI operations in the country. The Country Representative will also support team members in working effectively with and fulfilling accountabilities to FRI staff in other teams and offices, including the regional, international, and specialty teams and departments.

**Summary of Responsibilities:**

1. Provide overall leadership and coordination to the Country Team including the development of country strategic planning.
2. Raise the profile and develop/maintain an excellent reputation for impact, reliability and performance of Farm Radio International within the country and region.
3. Develop, build and nurture strong relationships with key stakeholders including the public, private, civil society, media, farmer organizations and funding agencies.
4. Grow the organization both in budget size and portfolio within the country by Identifying and developing prospects for new projects in country working closely with FRI's Program Development Team and systems.
5. Manage the country office and any field-offices or sub-offices including all the assets of the organization and oversee the security, safety and welfare of staff.
6. Manage the Human Resources administration to ensure effective and efficient systems for recruitment and retention of staff.
7. Oversee the financial management of the country office including developing and monitoring country annual budgets, spending plans and related periodical financial reports.

**QUALIFICATIONS**

**Experience and requirements**

- +10 years of experience in program implementation and management, including in the communication for development sector or agricultural development at a senior management level
- University degree in agriculture, communication, international development, environmental studies or a related field, a master's degree (an asset and added advantage)
- Experience in leading teams and multiple, multi layered relationships in an international institution
- Proven skills at managing projects with various donor agencies
- Proficiency in English, with very good written and oral communication skills including development of donor reports
- A mature self-starter, good communicator and team builder with the ability to manage and motivate teams

Knowledge requirements

- Knowledge and experience in project development and implementation, including project cycle management and results-based management
- Knowledge of broadcasting and ICT for development (an asset)
- Knowledge of agriculture and rural development priorities and policies in Tanzania and sub-Saharan Africa
- Knowledge of national or international donors and strategic or implementing partners in East Africa
- Significant knowledge of the principles of gender equality and women's rights and experience in integrating these principles into the project cycle

**Skills and attributes**

- Good team building skills
- Excellent intercultural communication skills
- Good organizational and time management skills; ability to work under pressure to meet deadlines
- Be comfortable working with minimal supervision and limited resources

**Application procedure**

Interested and qualified Tanzanians are invited to send their applications enclosing a covering letter and detailed curriculum vitae with names of three referees, and their contacts to tanzania@farmradio.org and Cc rchapota@farmradio.org

Please note that Farm Radio International has no recruitment agent, therefore all applications should only be sent to the above mentioned addresses. Only shortlisted candidates will be contacted.

215394901

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila raia kuwa na bima kuanze sasa

**KATIKA** siku za hivi karibuni kumekuwapo na mijadala mbalimbali inayohusisha umuhimu wa kuwapo kwa utaratibu wa kutumika kwa bima ya afya kwenye matibabu ya Watanzania wote.

Hoja hizo zinakuzwa na taarifa za kuwapo kwa kilio cha wagonjwa wanaoshindwa kumudu gharama za matibabu kutokana na uwezo mdogo na kutokuwapo kwa mfumo wa bima ya afya unaowanufaisha wengi.

Tukisema walio wengi tunamaanisha mifumo ya sasa inawalenga na kuwahudumia zaidi walio kwenye ajira rasmi ama ndani ya sekta ya umma au binafsi.

Taarifa za kutoka vyanzo mbalimbali zikiwamo za Wizara ya Afya, zinaonyesha kuwa ni wastani wa asilimia saba pekee ya Watanzania walio katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Aidha, zinasema ni wastani wa asilimia 13 hadi 15 pekee ya Watanzania ndiyo waliopo kwenye mfumo wa bima ya afya, hii ikihusisha mifumo mingine kama ile inayohudumia wateja kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii kama NSSF.

Takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi hugharamia matibabu kwa kulipa fedha za tiba kila wanapougua.

Ukubwa wa tatizo hili huonekana kuwa kubwa zaidi pale panapotokea magonjwa yanayohitaji vipimo na uchunguzi wa gharama zaidi, wengi hushindwa kugharamia tiba kwa kukosa fedha mifukoni.

Changamoto za kukosekana utaratibu wa bima ya afya unaowahudumia Watanzania wengi umeonekana mara nyingi wagonjwa wanapoomba msaada wa kuchangiwa malipo au fedha kwa ajili ya matibabu iwe ndani au nje ya nchi.

Tatizo hilo linatokana na ukweli kwamba hakuna mifumo imara ya ukusanyaji wa fedha kwa ajili ya kuchangia matibabu ambazo kila mmoja anawekeza kwenye mifuko rasmi ya tiba kupitia bima.

Wakati watumishi wa umma na wachache kutoka sekta binafsi ndiyo waliojiunga kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), wakulima, wamachinga na wanaoishi vijijini baadhi yao wanatibiwa kupitia Mifuko ya Bima ya Jamii (CHF) ambayo sasa huitwa CHF iliyoboreshwa.

Hata hivyo, kiwango cha wanufaika wa huduma za bima nchini ni kidogo na serikali mara kwa mara inasema inaandaa utaratibu wa kuanzisha kwa bima ya afya kwa wote.

Kufanikiwa kutekelezwa kwa mpango huo kutapunguza changamoto za matibabu kwa wananchi wengi na kutokana na kuongezeka kwa magonjwa mengi hasa yaliyosugu na yasiyoambukiza ambayo humwandama mgonjwa katika kipindi chote cha uhai wake.

Tunaamini hili ni suala la msingi na la muhimu kutokana na ukweli kwamba sekta ya tiba imeboreshwa kwa kiwango kikubwa na kuongeza huduma nyingi za kibingwa zenye kuhitaji vipimo vikubwa ambavyo miaka ya nyuma hazikuwa zikipatikana hapa nchini.

Huduma hizo zimesababisha gharama za vipimo kuwa kubwa zaidi zikilinganishwa na kipato cha Mtanzania.

Huduma hizo kama kuchunguzwa moyo, kupandikiza figo, kufanyiwa vipimo na tiba za mifupa, mishipa ya fahamu na ubongo zinapatikana Muhimbili, lakini malipo yake ni makubwa.

Tunaona kuwa bila bima ya afya ni wachache wanaoweza kujigharamia.


Ndiyo maana wakati serikali ikijipanga kuhakikisha wananchi wanajiunga kwenye mifumo rasmi ya bima za matibabu inapaswa kuongeza na kuimarisha elimu ya bima ya afya kwa wananchi ili kuwahamasisha umuhimu wa kujiunga.

Ndiyo maana tunaona kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, anapozungumzia kwa msisitizo kuwa ni vyema kila Mtanzania kuwa na bima ya afya ni suala linalopokelewa na mikono yote.

Tunaungana naye tukisema hatua hizo zitanusuru taifa kutokana na mzigo mzito wa kugharamia tiba unaoiathiri jamii yetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace, MKURANGA

# Tamasha la jinsia laja kuikomboa upya jamii

**TUNAPOZUNGUMZIA** tamasha, huo ni mkusanyiko wa watu kutoka makundi mbalimbali.

Matamasha mara nyingi yanasaidia watu wa sehemu moja kuungana na watu wale sehemu nyingine na baadaye wanakuwa kitu kimoja.

Pia, yanawasaidia watu kujifunza mengi kupitia ushiriki wao. Hapo ndipo panasemwa "mnakutana na kubadilishana mawazo."

Katika tamasha ndiko mtu anapata fursa ya kushiriki na kwa sababu atanufaika na kuyajua mambo mengi.

Hivyo, wanajamii inatakiwa kuwa mbele wanaposikia tamasha wanatakiwa kujitokeza ili kuweza kunufaika na chochote ambacho kitazungumzwa katika tamasha hilo.

Mwezi huu, asasi ya TGNP Mtandao inatarajia kufanya tamasha kubwa litakalokusanya zaidi ya watu 1,500 kutoka ndani ya nchi na nje ya nchi. Ni sehemu ya hatua ya asasi hiyo kuadhimisha miaka 25 tangu kuanzishwa kwake.

Hivyo, kuna mada mbalimbali zitakazojadiliwa, zote zikiwa na ujumbe wa kuisaidia jamii kokote iliko, katika sura pana ya kufahamu tulikotoka na tunakoelekea.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa TGNP Mtandao, Monica John, tamasha hilo litazungumzia masuala ya utekelezaji wa maudhui ya ajenda ya Mkutano wa Beijing na kufanya mikakati ya pamoja kuona wapi tunaenda na wapi tuliko.

**Amina Juma, mmoja wa washiriki wa semina za jinsia na maendeleo (GDSS), anasema tamasha hilo limekuja kwa wakati na litawasaidia washiriki kujua mengi kuhusu ukatili wa kijinsia katika sura pana.**

Monica anasema, tamasha la jinsia linaimarisha ujenzi wa nguvu za pamoja katika umoja wao kupaza sauti.Kutokana na umuhimu wake, umma kutoka mikoa mbalimbali na nchi mbalimbali utakusanyika kushiriki kwenye tamasha hilo.

Anaongeza kuwa tamasha hilo la 14 kwa mwaka huu litafanyika mwezi ujao kuanzia tarehe 23 hadi 27, ambayo hasa ni kipindi cha umri miaka 25 ya TGNP Mtandao inatimizwa, vivyo hivyo kwa azimio la Mkutano wa Beijing.

Monica anasema, malengo ni kutafakari na kupeana taarifa, kisha kujifunza ili kuweza kuzitambua nyanja mbalimbali husika, mada kuu ni harakati za wanawake zinavyoweza kuleta mabadiliko.

Amina Juma, mmoja wa washiriki wa semina za jinsia na maendeleo (GDSS), anasema tamasha hilo limekuja kwa wakati na litawasaidia washiriki kujua mengi kuhusu ukatili wa kijinsia katika sura pana.

Mama huyo anahimiza kwamba, kupitia tamasha hilo washiriki watabadilishana mawazo na makundi mbalimbali na hivyo anashauri jamii, ijitokeze kushiriki tamasha hilo ili inufaike kupitia mada zitakazojadiliwa.

## BARUA/MJADALA

# Kulikoni maduka haya?

**Mhariri,**

*KATIKA siku za karibuni hali ninayoweza kuieleza ikiwa ni ya ghafla, nashangaa kuona hapa kwetu jijini Dar es Salaam, maduka mengi ya kisasa maarufu 'super market' yanafungwa.*

*Nasema hivyo, kwa sababu mimi ni mmoja wa wateja, kila ninapopata kiasi fulani cha pesa, ninafuata mahitaji yangu mahali hapo.*

*Kinachonishtua nijiulize katika siku za miezi kadhaa ni kwamba, kila ninapotembelea maduka hayo ninapata tabu zaidi kwamba mengi yanasuasua.*

*Jambo kuu hapo kwa mtazamo wangu, nahisi lipo tatizo kubwa la kibiashara ambalo wadau husika wa kibiashara wanapaswa kuliingilia kati, kudodosa kujua nini hasa tatizo.*

*Mkazi, Makongo Juu,*
*Dar es Salaam.*

# Afya sokoni hairidhishi

**Mhariri,**

*NASIKITIKA sana kila mara ninapoona hali mbaya ya mazao katika masoko yetu, katika miji mbalimbali.*

*Kweli tuna utajiri wa bidhaa, lakini zinapofikishwa mahali hapo zinawekwa katika hali mbaya kiafya kwamba, hakuna mwongozo na kanuni za kiafya kwa watu hao.*

*Je, ina maana katika sehemu hizo hakuna wasimamizi wa kiafya katika maeneo yetu?*

**Mussa Mbeko,**
**Safarini Mvomero.**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Mbolea kushuka bei tunatarajia itaongeza kipato cha wakulima

**Na Beatrice Moses**



Mbolea iliyoko ghalani mkoani Rukwa. **PICHA: MAKTABA.**

WAKULIMA kadhaa nchini kwa miaka mingi wamejikuta wakiishi katika hali ya umasikini, kwa kutonufaika na kilimo ipasavyo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kutumia mbinu duni zisizozingatia ushauri wa mabwana na mabibi shamba.

Kuna wakulima ambao wamekuwa katika hali hiyo, kutokana na kukosa elimu ya kilimo bora, hivyo wamekuwa wakipanda mbegu, pasipo kujali kuwa ni bora kwamba hazishambuliwi na magonjwa, upandaji wa kuzingatia vipimo kulingana na zao husika.

Pia, suala la kutambua umuhimu wa matumizi ya mbolea kwenye mazao wanayolima, nayo ni changamoto ya aina yake, inayowasababishia baadhi yao kuvuna mazao duni, tofauti na nguvu kubwa waliyoitumia katika kuzalisha.

Serikali kwa upande wake, imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kuhakikisha inawasaidia wakulima wanufaike na kazi yao, hivi karibuni. Sasa imetangaza bei elekezi za mbolea ya kupandia (DAP) katika soko la ndani ya nchi, ambayo inashuka kwa Sh. 8,000 hadi Sh. 10,000 sawa na wastani wa kati ya asilimia 13 na 17.

Waziri wa Kilimo, Japhet Asunga, lipotoa taarifa hiyo kwa vyombo vya habari juzi, alibainisha kuwa hatua hiyo imefikiwa baada ya na ushindani wa zabuni za BPS iliyofunguliwa tangu Juni 21 iliyopita.

Pia, anabainisha kuwa tayari mbolea tani 29,000 imeshawasili nchini na imeanza kupelekwa kwenye maeneo husika. Alifafanua kuwa, katika mbolea ya DAP kwa mwaka huu, chanzo ilipungua kwa asilimia 12 ikilinganishwa na bei za zabuni ya Julai, 2018.

Wizara ilifanya mrejeo wa kikokotoo ambao umefanya bei ya mbolea kwa mkulima kupungua kwa wastani kimkoa wa Sh. 8,000 hadi Sh.10,000 ambayo ni sawa na asilimia 13 hadi 17 kwa mfuko wa kilo 50 wa mbolea hiyo aina ya DAP.

Punguzo la Sh. 5,000 au 6,000 sawa na asilimia 14 na 19 kwa wastani wa kimkoa kwa mfuko wa kilo 0025,wakati kwa mfuko wa kilo tano, bei imepungua kwa Sh.1,300 hadi Sh. 1,500 sawa na asilimia 15 hadi 20.

Bei elekezi iliyotangazwa kwa mbolea ya DAP kwa mikoa ya Kanda ya Mashariki, ya Kati, Kusini na Kaskazini zitakuwa kati ya Sh. 51,900 na Sh. 60,300.

Hii ni habari njema kwa wakulima hasa ambao wapo makini na wameelimika hivyo huzingatia kilimo cha kisasa, tunatarajia kuona mavuno yao yakiongezeka, hivyo wengi nafasi ya kijiongezea kipato kulingana na mazao waliyolima na soko litakavyokuwa.

Wataalam wa masuala ya kilimo wanabainisha kuwa mifumo ya kilimo yenye uzalishaji endelevu inahitaji usimamizi mzuri wa rutuba ya udongo ili kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa uzalishaji wa chakula.

Usimamizi sahihi wa rutuba ya udongo unatajwa kuwa ni wa umuhimu katika uzalishaji wa mazao na kilimo katika kilimo-hai ambacho hushughulikia rutuba ya udongo kwa kuhifadhi na kuulinda dhidi ya jua, mvua na upepo na kulisha mabaki ya viumbe hai kwa njia inayofaa.

Udongo unapokua na rutuba ambayo inafaa kwa matumizi ya kilimo cha mazao ya aina mbalimbali umsaidia mkulima kuzalisha mavuno mazuri ya mazao aliyopanda.

Mkulima baada ya mavuno akiwa ana elimu nzuri ya kutosha kuhusu utunzaji wa udongo ili kulinda rutuba kwa njia ya kiasili anasaidia kupunguza matumizi ya mbolea .

Hatua hiyo, itamuwezesha pia kupunguza gharama ya kununua mbolea na vishamirisho vingine, hivyo atalima kwa gharama nafuu, hali itakayomuwezesha kulingana na msimu wa kilimo cha mazao aliyopanda kuvuna kwa wingi na kupata faida kwa kuhifadhi au kuuza.

Ili kufanikisha hatua ya serikali, ni wazi kwamba wakuu wa mikoa na kamati husika, zikiwamo za ulinzi na usalama, zinapaswa kuhakikisha kuwa hatua hiyoi inazaa matunda mema, kwa kudhibiti wafanyabiashara wenye tamaa ambao wanaweza kukiuka bei hiyo elekezi na kujipangia yao ili kupata faida kubwa zaidi.

Ni wazi bado usimamizi wa serikali unahotajika ili kuwezesha wakulima hawa kufaidi neema ya kushuka kwa bei ya mbolea, pia watahakikisha kwamba maofisa ugani wanawafuatilia kwa karibu.

Maafisa ugani hao wanapaswa kuwakumbusha wakulima umuhimu wa matumizi ya mbolea hiyo, pia Serikali itasimamia kwenye soko la mazao kuhakisha wakulima hao watauza mazao yao, pia kwa bei elekezi ili wanufaike.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



## Serikali yapokea ripoti ya 'unga', simu gerezani

INATOKA UK. 2

mapendekezo ya tume iliyoundwa na wanayapitia kabla ya utekelezaji.

"Ripoti imeshakamilika, tume imetoa mapendekezo yake ya nini kifanyike ili kuondokana na matatizo hayo gerezani, tunayapitia mapendekezo yaliyotolewa, utekelezaji wake unaweza ukawa wa bila kutangazwa au la. Tangu waikabidhi sasa unakaribia mwezi," alisema.

Akizungumza na waandishi wa habari akiwa mkoani Mbeya, Masauni alitaja majina ya alioagiza wasimamishwe kazi kuwa ni Inspekta Longino Mwemezi, Ramadhan Mhagama, Alexander Mwinjano na Benjamini Malango ambao wote ni masajini taji wa Magereza.

Maagizo ya kuwasimamisha kazi askari hao aliyatoa siku hiyo kwa Kamishna Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike, baada ya kufanya ziara ya siku moja ndani ya gereza hilo na kubaini changamoto hiyo.

Masauni alisema alibaini wafungwa wanamiliki simu tisa na dawa za kulevya aina ya bangi ndani ya gereza na kwamba vyote vilikuwa vimeingizwa kwa ushirikiano kati ya askari wasiokuwa waaminifu na wafungwa.

Alisema baada ya kuzinasa simu hizo alizikabidhi kwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya uchunguzi na kwamba taarifa za awali zilionyesha, zilikuwa zinatumika kwenye vitendo vya uhalifu ikiwamo rushwa.

Alisema vitendo vya aina hiyo vilishakemewa na Rais John Magufuli na aliagiza vidhibitiwe ndani ya magereza yote nchini ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

Alisisitiza kuwa vitendo hivyo ni hatari kwa usalama wa magereza endapo askari wataendelea kutokuwa waaminifu kwa kuruhusu viendelee kufanyika ndani ya magereza.

Naibu Waziri Masauni aliwataka wakuu wa magereza yote nchini kuwa makini kwa kuzuia vitendo hivyo vya ukiukwaji wa sheria na maadili ili kulinda usalama wa maeneo hayo ambayo ni hatarishi.

# JPM ataja sababu 3 umaskini wa Afrika

INATOKA UK. 2

maendeleo hivyo tumekuwa tukizunguka kwenye mataifa tajiri kuomba misaada na mikopo.

"Inawezekana kabisa misaada na mikopo hiyo inatokana na maliasili zetu wenyewe kama Waafrika, tunatakiwa kujielekeza kwenye vitu tulivyonavyo na mara moja kuvigeuza kuwa fedha."

Rais Magufuli alisema kuwa na fedha ni matokeo ya mwisho ya matumizi ya maliasili zilizopo na siyo msingi wa maendeleo.

"Hata Mwalimu Julius Nyerere, Baba wa Taifa hili alisema 'ili tuendelee tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora', hakutaja fedha. Fedha alijua itakuja tu kama hayo tutayatimiza.

Rais Magufuli alisema ukosefu wa ubunifu wa teknolojia ya viwanda ni chanzo kingine cha umaskini barani.

"Afrika haitaweza kusimamia rasilimali zake kwa kuendelea ilivyo bila ya kuwa na viwanda. Tukiendelea kuuza mazao ghafi ya kilimo, madini, misitu, mifugo na uvuvi, itakuwa vigumu sana kufikia mageuzi ya kiuchumi na kijamii. Ni lazima tukuze ubunifu na vijana wetu," alisema.

Rais Magufuli alipongeza jukwaa hilo kupitia kauli mbiu yake ya kuimarisha usimamizi bora wa maliasili kwa asili ya mageuzi ya kijamii na kiuchumi Afrika.

Alisema kauli mbiu hiyo inaonyesha umuhimu wa Afrika kujenga mifumo mipya ya kusimamia na rasilimali zake kwa manufaa ya watu wake.

"Vinginevyo rasilimali zetu zitasimamiwa na kutumiwa na watu wengine kwa manufaa yao, ndicho ambacho kimekuwa kikifanyika katika maeneo mengi ya Bara la Afrika, lakini swali la kujiuliza ni kwanini bara tajiri limeshindwa kusimamia na kutumia rasilimali zake ili kuleta mageuzi ya kijamii na kiuchumi?" Rais Magufuli alihoji.

Alisema anatambua mkutano huo ni wa sita tangu kuanzishwa kwa jukwaa hilo mwaka 2014 na wamekuwa wakiifanya nchi mbalimbali na mwaka huu umefanyika Tanzania kwa mara nyingine.

Alisema changamoto za Afrika zitatatuliwa na Waafrika wenyewe na hakuna wajomba watakaokuja kuwasaidia.

"Sisi ni Waafrika, tunafahamu changamoto zetu vizuri zaidi ya watu wengine, nawashukuru marais wastaafu kuendelea kutoa michango yenu, uzoefu wenu unatusaidia kuliongoza bara hili," alisema.

Alisema msingi mkubwa wa maendeleo ni rasilimali na watu na uwapo wao hautoshi kuleta maendeleo endapo kutakosekana mifumo ya kuisimamia.

Rais Magufuli aliwashukuru viongozi wastaafu wa Tanzania kwa ushauri wanaoutoa kumsaidia kuiongoza nchi.

"Rais mstaafu awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, alinisimamia mchakato wa kwanza kupelekea mimi kwa mara ya kwanza kuwa mbunge akiwa Mwenyekiti wa CCM, angeweza kulikataa jina langu," alisema.

"Kikwete ndiye aliyesimamia mchakato wa mimi kuwa Rais. Mchango wenu hautasahaulika, ninawashukuru sana," alisema.

Awali, Mkapa alisema ili kufikia uchumi imara, kuna haja ya kuweka mifumo madhubuti ya kulinda rasilimali kama inavyopendekezwa na Umoja wa Mataifa (UN).

"Utunzaji mazingira endelevu unahitaji kuweka mikakati madhubuti kwa kuunganisha misingi ya maendeleo ya jamii na hii inatakiwa ihusishe wadau wengi wakiwamo watumiaji wa ardhi," alisema.

Mkapa alisema ongezeko la watu Afrika linakua kwa kasi kubwa hivyo kuchochea mahitaji ya ardhi na mikakati ya haraka inahitaji kuhakikisha migogoro ya ardhi inaepukwa.

Mkapa alisema moja ya njia ya kukabiliana na ukataji miti kiholela ni kuipanda mingi na kutoa mapema taarifa za hali ya hewa na mabadiliko ya tabia nchi ili kusaidia kutengeneza mipango mikakati ya kukabiliana na athari zake.



Mafundi wakifyatua matofali kwa ajili ya ujenzi wa jengo la maabara la Shule ya Sekondari Murangi, katika Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara jana, ikiwa ni mwendelezo wa uboreshaji wa maabara za masomo ya sayansi kwenye sekondari za kata, jimboni humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



HABARI MIKOANI

# Utafiti kuhusu nguvu za kiume kuwekwa wazi

**Na Joseph Mwendapole**

UTAFITI wa saba wa magonjwa ya moyo uliofanywa na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) unatarajiwa kuwasilishwa katika mkutano wa wanasayansi, madaktari bingwa na wahudumu wa afya wanaotoka katika nchi za Ukanda wa Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika.

Utafiti huo ambao ulifanyika mwaka jana na mwaka huu ni kuhusu mwenendo wa mapigo ya moyo kwa mgonjwa, wagonjwa wenye moyo ambao uwezo wake wa kufanya kazi umepungua, jinsi wanavyozingatia matibabu kama walivyoshauriwa na madaktari, shinikizo la damu na tatizo la kisukari.

Tafiti nyingine zitakazowasilishwa kwenye mkutano huo wiki ijayo Zambia ni upungufu wa nguvu za kiume katika jamii, uelewa wa sababu hatarishi za magonjwa ya moyo katika jamii, magonjwa matatu kwa pamoja yaani moyo na figo kushindwa kufanya kazi na upungufu wa damu mwilini.

Mkuu wa Kitengo cha Utafiti wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Pedro Pallangyo, alisema tafiti hizo zimefanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka miwili na kwa wagonjwa wanaotibiwa katika taasisi hiyo.

Kuhusu mkutano huo wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, Dk. Pedro alisema kwa upande wa magonjwa ya moyo utawasaidia kubadilishana matokeo ya huduma za matibabu wanazozitoa hasa tafiti zinazofanywa katika nchi mbalimbali ili kuboresha huduma zinazotolewa kwa wagonjwa.

Ofisa Uuguzi wa JKCI, Jalack Milinga, ambaye alishiriki katika kufanya utafiti huo, alisema kwake ni mara ya kwanza kuhudhuria mkutano huo ambao utamsaidia kuongeza ujuzi katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa moyo, lakini kubadilishana uzoefu na wauguzi wenzake watakaoshiriki katika mkutano huo.

"Utafiti wangu uliangalia jinsi ya uzingatiaji wa unywaji wa dawa za moyo kwa wagonjwa ambao mioyo yao haifanyi kazi vizuri. Hivyo naamini ushiriki wangu katika mkutano huu utaniwezesha kupata mbinu mpya za kusimamia jukumu la kuwasaidia wagonjwa wetu kuzingatia matibabu ili kupata matokeo bora ya tiba," alisema Jalack.



Wakazi wa jiji wakiponda kokoto kwa ajili ya kuziuza ili wajipatie riziki katika eneo la Kunduchi Mbuyuni, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**.

# Shule Dar yamwomba DC msaada madarasa

**Na Enock Charles**

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Mbezi Ndumbwi Kinondoni jijini Dar es Salaam amemwombaMkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, kusaidia kupatikana kwa madarasa ya wanafunzi katika shule hiyo ili iendane na idadi ya wanafunzi 1,667 waliopo shuleni hapo.

Akisoma risala mbele ya Mkuu huyo wa Wilaya, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Judith Kilimo, alisema idadi ya wanafunzi shuleni hapo ni kubwa, hivyo kuna changamoto kubwa ya uhaba wa madarasa na vyoo kwa ajili ya walimu na wanafunzi.

"Mpaka sasa shule yetu ina jumla ya wanafunzi 1,667 na walimu 36... idadi hii ni kubwa ikilinganishwa na vyumba vya madarasa tuliyonayo ambayo ni v 12 tu," alisema na kuongeza: "Pia tuna matundu 6 ya vyoo vya wasichana, vinne ya wavulana na mawili ya walimu."

Akitoa shukurani, alimshukuru mfanyabiashara William Ndila wa Kampuni ya Bill Ndila Enterprises ya jijini Dar es Salaam aliyejitolea mabati 160 kwa ajili ya kuezeka vyumba vinne vya madarasa.

Mwalimu Mkuu huyo alisema itasaidia kuepusha wanafunzi kusomea nje kutokana na ukosefu wa madarasa.

Chongolo aliitaka shule hiyo kuendeleza rekodi yake ya kuwa miongoni mwa shule zinazoongoza kitaifa katika matokeo ya mtihani wa darasa la saba ili kupata maendeleo endelevu katika wilaya hiyo.

"Mwaka jana mlishika namba tatu nataka mwaka huu mshike namba moja kitaifa maendeleo ya watoto wetu ndio maendeleo ya wilaya yetu kwa ujumla," Chongolo alisema.

Ndila alisema ametoa mchango huo ili kuwezesha elimu ya msingi kutolewa pasipo kuwa na vikwazo vitakavyozuia wanafunzi kujifunza kwa ufanisi.

# Rasimu yataka madereva kupewa kifaa cha utambuzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RASIMU ya kanuni ya udhibiti wa madereva na usajili wa wafanyakazi wa magari ya biashara imependekeza kila dereva kupewa cheti cha uthibitisho na kifaa cha kielektroniki cha utambuzi.

Akiwasilisha kanuni hiyo kwa wadau wa usafirishaji wa ardhini, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), Gilliard Ngewe, alisema dereva atakayeendesha magari ya biashara yakiwamo yanayobeba abiria, atapewa cheti cha uthibitisho baada ya kutimiza masharti.

Alisema pia atapewa kifaa cha kielektroniki cha utambuzi ambacho kitakuwa na namba ya siri na taarifa zote za dereva.

"Hii namba ya siri haitaruhusiwa kupewa dereva mwingine, dereva anapoingia kwenye gari itajulikana kuwa gari hilo linaendeshwa na nani na hatua hii ni kuwafanya kuwa na usafiri wa viwango na pia utaondoa tabia ya 'udei waka' ambayo imekuwa ikisumbua katika kudhibiti," alisema.

Ngewe alisema ili kupewa cheti cha udhibitisho, dereva atatakiwa kuwa na leseni ya kuendesha gari husika, cheti cha mafunzo ya udereva, malipo ya ada ya cheti, ripoti ya uchunguzi wa matibabu na anatakiwa kuwa na uzoefu usiopungua miaka mitano ya kuendesha gari ya biashara.

"Kwa kanuni hizi ina maana mamlaka itaweza kumruhusu dereva kuvuka mpaka wa Tanzania na kwenda kufanya kazi katika Jumuiya za Afrika Mashariki, SADC, Comesa," alisema.

Ngewe alisema dereva aliyethibitishwa atatakiwa kuhakikisha gari lina leseni na bima halali, kuvaa kitambulisho, kutoendesha gari akiwa mlevi , kutii maagizo halali na ofisa wa polisi na LATRA na kuhakikisha malipo ya nauli yanafanywa kwa njia ya kielektroniki.

"Dereva wa gari ya abiria atawajibika kutokubeba abiria au mtu aliyezidi, kuhakikisha milango imefungwa kabla ya kuanza kuendesha gari, abiria wanafunga mkanda na kufika kwenye vituo kama inavyoainishiwa kwenye tiketi zao kutokatisha njia au kutoa huduma katika njia nyingine.

"Pia dereva atahakikisha kuwa burudani inayotolewa katika gari la usafiri wa umma kwa wakati wote wa safari inafuata maadili na utamaduni wa kitanzania kwa sauti ya kiwango cha chini, hakuna mtu anayefanya biashara, kuhubiri au kufanya shughuli za kisiasa au kutoa burudani ya kuwabugudhi au kuwasumbua abiria," alisema.

Kuhusu usajili wa wahudumu, Ngewe alisema mtu anayetaka kufanya kazi ya uhuduma kwenye magari ya biashara atatakiwa kuomba usajili akiambatanisha cheti cha afya, cheti cha mafunzo ya huduma ya kwanza au huduma bora kwa wateja ya mafunzo kwenye sekta ya usafirishaji.

# H/shauri yaomba upendeleo kutatua uhaba wa walimu

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

HALMASHAURI ya Mpanda wilayani Tanganyika Mkoa wa Katavi, imeiomba serikali kuongeza idadi ya walimu wanaoajiriwa kufundisha shule za sekondari na msingi pamoja na kuipa upendeleo maalumu kwa kuwapangia walimu wengi ili kukabiliana na uhaba.

Ombi hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Rojas Rumul, katika hafla ya kuwapongeza walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Karema kwa kufanya vizuri na kufaulu mtihani wa kidato cha sita kwa miaka minne mfululizo.

Alisema halmashauri hiyo inauhaba wa walimu 235 wa shule za sekondari na waliopo hivi sasa ni walimu 108, na kwamba upungufu huo unasababisha walimu waliopo kuwa na mzigo mkubwa wa kufundisha kwa kuwa walimu mmoja anatakiwa kufundisha wanafunzi 35, lakini wanalazimika kufundisha wanafunzi zaidi ya hao.

Kutokana na changamoto hiyo, alisema walimu wamekuwa wakiiomba serikali iongeza idadi ya ajira za walimu na halmashauri ili ipewe upendeleo maalumu wa kupelekewa walimu wengi kutatua tatizo hilo.

Mbali na changamoto hiyo, pia halmashauri inakabiliwa na upungufu wa nyumba za walimu wa sekondari idadi ya nyumba zilipo ni 52, wakati waliopo ni 235, hivyo kuna mahitaji makubwa ya nyumba hizo.

Mkurugenzi huyo alisema shule hiyo tangu ilipoanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano mwaka 2014, imekuwa ikifanya vizuri kwa kufaulisha katika mitihani ya kidato cha sita kwa ufaulu wa asilimia 99.9.

Aliongeza kuwa halmashauri yake imekuwa ikitoa hamasa kwa kutoa zawadi kwa wanafunzi wanaofanya vizuri kwenye kila somo, hali inayosababisha ushindani mkubwa kwa wanafunzi.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani akifanya mahojiano na dereva wa pikipiki ya magurudumu matatu baada ya kumkamata akiwa amezidisha mzigo katika Barabara ya Mwai Kibaki, eneo la Mlalakuwa Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**.

# Waziri ataka elimu ya utafiti wa mazingira kwa wananchi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, amewataka wataalamu na watafiti wa mazingira kufikisha elimu ya matokeo ya utafiti wao kwa wananchi ili kuwajengea uelewa juu ya utunzaji na uendelezaji endelevu wa mazingira nchini.

Akizungumza baada ya kufungua mkutano wa tano wa kisayansi juu ya mazingira endelevu wenye mada isemayo 'binadamu na utunzaji wa viumbe hai', Waziri Simbachawene alisema elimu ya mazingira ni muhimu kuwafikia wananchi mara kwa mara ili wawe watunzaji bora wa mazingira kwa maendeleo endelevu.

"Utafiti wenu una umuhimu mkubwa katika suala zima la utuzwaji wa mazingira na endapo elimu zaidi ikatolewa kwa wananchi juu ya matokea ya utafiti huo yatasaidia sana katika kuwejengea uwezo na uelewa," alisema.

Waziri Simbachawene alisema kuna umuhimu kwa jamii zote zinazoishi katika maeneo hayo zikashirikishwa katika hatua zote za utafiti ili kuwa na uelewa wa pamoja wa namna bora ya utunzaji wa mazingira.

"Lazima utafiti huo pia uangalie namna gani jamii hizo zinanufaika na uhifadhi na utunzaji wa mazingira," alisema na kuongeza:

"Utafiti wa kitaalamu ni muhimu sana na mkutano huu umewakutanisha wataalamu wa mazingira, hivyo mtapata muda wa kutosha kufanya majadiliano."

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alisema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa umewakutanisha wadau na wanasayansi katika kujadili juu ya binadamu na utunzaji wa viumbe hai.

"Tunategemea mwisho wa mkutano huu washiriki watakuja na mapendekezo mbalimbali yatakayotoa mwelekeo wa nini kifanyike katika suala zima la kuhakikisha utunzaji bora wa mazingira," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Suleiman Saddiq, alisema mkutano huo umeonyesha dhamira ya dhati katika kulinda mazingira, hivyo ni wajibu wa wataalamu kuleta mapendekezo yatayosaidia kulinda bora ya utunzaji wa mazingira bila kuathiri mazingira na viumbe vingine," alisema.

Akiwakaribisha kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo,

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Richard Kwitega, alisema maudhui ya mkutano huo unaonyesha dhamira ya kweli katika kulinda mazingira na viumbe hai.

# Meya afunguka uchaguzi wa leo

**Na Romana Mallya**

MSTAHIKI Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita, amesema yupo tayari kumpa ushirikiano yeyote atakayeshinda nafasi ya Naibu Meya kupitia uchaguzi utakaofanyika leo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam baada ya kumalizika kwa kikao cha robo ya nne ya mwaka cha Baraza la Madiwani, Meya Mwita alisema yupo tayari kufanya kazi na Naibu Meya yeyote atakayechaguliwa.

"Kutokana na wengi kuhama kwenye nafasi zao na wengine kuhamia Chama Cha Mapinduzi (CCM), bila kujali itikadi ya chama nitafanyakazi na yeyote kwa sababu lengo ni kutumikia wananchi, lazima tofauti za kichama tuziweke pembeni," alisema.

# Wanafunzi waonywa uchaguzi wa vyuo

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KATIBU Tawala Mkoa wa Kusini Pemba, Abdalla Rashid Ali, amewataka wanafunzi Kisiwani Pemba kuchagua vyuo ambavyo ni bora, vyenye sifa mzuri na vyenye usajili wa uhakika.

Alisema kuna utitiri wa vyuo ambavyo vimekuwa vikitoa taaluma mbalimbali, lakini baadhi havina usajili wala havitambuliwi kisheria.

Akizungumza na wanafunzi hao katika Shule ya Maandalizi Madungu Chakechake, Pemba, Katibu aliwataka wanafunzi hao kuwa makini sana wanapotaka kujiunga na vyuo kwani wataweza kupoteza rasilimali fedha na wakati Lakini Mwisho wake wanakuja kuonekana hawakusoma jambo kutokana na vyuo walivyojiunga havitambuliwi na serikali.

Aliwataka wanafunzi hao kujiunga na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kitakapoanzishwa Pemba ili kupata elimu iliyo bora na itakayowasaidia katika maisha yao.

"Sisi vijana tunapenda sana msome, lakini tuangalieni sana na muwe makini wakati wa kuchagua vyuo vya kujiunga ambavyo... ni bora viwe vina sifa mzuri, lakini zaidi viwe vimepata usajili wa uhakika kwani nchini kuna vyuo vingi, lakini baadhi yake havina usajili na wala havitambuliwi," alisema Rashid.

# Watumishi waonywa ubaguzi sehemu za kazi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha Vijijini wilayani Arumeru, Dk. Wilson Mahera, amewataka watumishi wa halmashauri hiyo, kufanya kazi kwa ushirikiano bila ya kubaguana kwa kuangalia vyeo na nafasi walizonazo, ili kufikia malengo ya mpango mkakati wa halmashauri.

Rai hiyo, aliitoa jana katika kikao cha kawaida kilichowakutanisha watumishi wa halmashauri hiyo kwa ajili ya kujadiliana njia mbadala za kutoa huduma na kutatua kero za watumishi wakati wa kuwahudumia wananchi.

Mahera aliwapongeza watumishi kwa jitihada kubwa walizozifanya mwaka uliopita 2018, kwenye sekta mbalimbali kwa lengo la kusukuma mbele gurudumu la maendeleo kwenye halmashauri hiyo.

Alisema kila mtumishi ana haki sawa na anatakiwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa kuzingatia taaluma aliyoisomea.

Aliwataka watumishi kukaa pamoja na kujadili changamoto zinazowakabili katika utendaji kazi wao, ikiwamo kuweka wazi kero walizonazo ili ziweze kukatuliwa na menejimenti badala ya kukaa kimya na kusubiri mambo yaharibike ndipo waanze kulalamika.

Pia aliagiza kuboreshwa dawati la malalamiko na kero kwenye halmashauri hiyo na yanapowafikia, yashughulikiwe kwa wakati na idara husika na watumishi ili kujenga imani kwa wananchi na watumishi wenye kero.

"Dawati la malalamiko siyo la wananchi peke yao, hata nyinyi watumishi linawahusu, unapopata tatizo lililoshindikana ndani ya idara yako, au kitengo chako, wasilisha kwenye dawati hilo, ndio sehemu sahihi litashughulikiwa kwa wakati badala ya kulalamika pembeni," alisema Mahera.

Ofisa Utumishi wa halmashauri hiyo, Hamis Mpume, aliwaahidi watumishi kuendelea kusimamia haki zao, wajibu na usawa, huku akiwakumbushia kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

"Nina imani kuwa kila mtumishi anafahamu vizuri majukumu yake, niwatake kila mmoja wenu kuyatekeleza kwa ufanisi wa hali ya juu na mimi kama msimamizi wenu nitatenda haki kwa kila mmoja wenu bila ya kumwonea mtu yeyote na sitashindwa kumchukulia hatua kali za kinidhamu na kisheria mtumishi atakayeshindwa kutekeleza majukumu yake," Mpume alisema.

Alisema, kuna haja ya halmashauri hiyo kufanya vikao vya kimkakati na watumishi kila mwisho wa mwezi ili kushugulikia matatizo yao kwa wakati.

Akizungumza kwa niaba ya watumishi wenzake, Mhasibu wa halmashauri hiyo, Simon Mwanjwangwa, licha ya kuwapongeza viongozi hao kwa ushirikiano mzuri na watumishi, aliwaomba kutoa motisha kwa watumishi wanaofanya vizuri kazini kwa kuwa itawajengea ari ya kupenda kazi zao.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Hudson Kamoga, akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani jana. Katikati ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Joseph Mandoo na Makamu Mwenyekiti, Joseph Barabojik. **PICHA: GIFT THADEY**.

# Wanafunzi 36 wapata msaada wa masomo

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, imefanikiwa kuwasaidia wanafunzi 36 wa shule za sekondari wanaoishi katika mazingira hatarishi kuendelea na masomo yao.

Makamu Mwenyekiti mstaafu wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Albert Msole, aliyasema hayo jana wakati akielezea mafanikio na changamoto kwenye miaka minne aliyoongoza kamati ya kudhiti Ukimwi katika wilaya hiyo.

Msole alisema kati ya wanafunzi 36, watatu kati yao walifanikiwa kufikia hatua ya chuo kikuu na wanaendelea na masomo hayo hadi sasa.

Alisema hali ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) kwenye wilaya hiyo imepungua kutoka asilimia tatu mwaka 2016 hadi kufikia 2.8, mwaka huu na lengo la taifa ni kufikia asilimia 90 kwa mwaka 2020 kupunguza maambukizi kwa wanaotumia dawa.

"Tutafikia asilimia 90 kwa kupima maambukizi, asilimia 90 watakaokuwa na maambukizi kutumia dawa na asilimia 90 ya wote wanaotumia dawa hali ya maambukizi iwe imepungua, pia tumesaidia mitaji ya vikundi 16 vya wenye VVU ili wajikimu kimaisha," alisema.

Alisema wamewafikia na kuhamasisha wananchi 36,670 wakiwamo wanaume 21,711 na wanawake 14,266 kupima hali zao za maambukizi ambapo watu 373 walikutwa na VVU na wameanza kutumia dawa za kufubaza virusi hivyo.

Alisema Simanjiro inaongoza kwenye Mkoa wa Manyara kwa jamii kuitikia upimaji, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Kiteto, Babati mjini, Hanang' na Mbulu mjini.

"Tunakabiliwa na changamoto katika kupambana na Ukimwi na upungufu wa rasilimali kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kamati ya kupambana na janga la Ukimwi," alisema Msole.

Pia alisema baadhi ya vijana wa jamii ya wafugaji, wanaosafiri nchi za jirani au mikoa mbalimbali, hawajikingi na maambukizi mapya ya Ukimwi kwa kuwa wakirudi nyumbani kwao huwaambukiza wenza wao.

Alisema kuna changamoto ya baadhi ya wachungaji, mitume na manabii wa madhehebu mbalimbali wanaohubiri dini zao, huwaambia waumini wao wenye maambukizi ya Ukimwi watupe dawa za kufubaza (ARV) kwa kuwa watapona kwa imani.

Akielezea changamoto za kupambana na maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi, alisema vijana wafugaji wakienda nchi za Zambia, Afrika Kusini, Msumbiji, Kenya na mikoa mbalimbali nchini wanakuwa wagumu kujikinga na maambukizi ya VVU na kusababisha maambukizi mapya kwa wenzi wao.

Alisema pia walioathirika na VVU wanapata wakati mgumu kuendelea vizuri kiafya kutokana na wahubiri hao kuwahamasisha waumini wao kuwa Mungu anaponya hivyo watupe dawa.

## Tanzania inavyotekeleza mikakati ya Unesco

**Novatus Makunga,** ARUSHA

TANZANIA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazotekeleza mikakati ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco), unaohusu mpango wa binadamu na maeneo tengefu kwa kuwa na maeneo matano nchini.

Akifungua mkutano wa sayansi kuhusu maeneo tengefu nchini, Waziri wa Nchi, Muungano na Mazingira, George Simbachawene, alisema maeneo tengefu yana utajiri mkubwa na rasilimali, pamoja na ikolojia na inaiweka Tanzania katika moja kati ya nchi 12 duniani zenye maeneo ya pekee.

Mkutano huo wa tano umeandaliwa na Baraza la Taifa la Mazingira (Nemc), ukiwa wa kwanza wenye kaulimbiu ya binadamu na maeneo tengefu.

Simbachawene aliyataja maeneo hayo matano kuwa ni pamoja na ikolojia ya Serengeti-Ngorongoro, Hifadhi ya Ziwa Manyara, Misitu ya Usambara Mashariki, Ghuba ya Jozani Chwaka na misitu ya Gombe-Masito-Ugalla.

"Maeneo tengefu siyo kwamba ni kwa ajili ya bionuai za pekee, bali pia yanawakilisha baadhi ya vivutio maarufu vya utalii, katika dunia kama ikolojia ya Serengeti-Ngorongoro," alisema.

Alisema maeneo tengefu yamekuwa na mchango mkubwa katika kukuza maendeleo ya uchumi wa jamii pamoja na uhifadhi wa mazingira.

Simbachawene alisema msingi wa uchumi wa Tanzania kama ilivyo kwa nchini nyingine zinazoendelea, unategemea matumizi ya rasilimali na kilimo kinachotegemea mvua pamoja na ufugaji unaotegemea uchungaji.

"Jamii zinazoishi kuzunguka maeneo tengefu zinanufaika kwa shughuli mbalimbali na hivyo kuchangia katika malengo ya maendeleo endelevu yaani SDG na pia malengo ya maendeleo ya kitaifa na mikakati yake," alisema.

Aliongeza kuwa maeneo tengefu ni muhimu katika kuhifadhi ikolojia na kuhakikisha mahitaji muhimu yanapatikana kama vile chakula, maji, nishati, dawa, uwiano wa hali ya hewa, misitu na mahitaji mengine ya binadamu.

Hata hivyo, alisema pamoja na kwamba maeneo tengefu yana umuhimu mkubwa, lakini bado yanakabiliwa na changamoto kubwa katika kuhakikisha yanaendelea kutunzwa.

Simbachawene alizitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na ongezeko kubwa la watu kuzunguka maeneo tengefu, ambako kunasababisha kuongezeka kwa mahitaji ya rasilimali kwa jamii hizo.

Alisema kuwa tishio lingine kwa mazingira ya maeneo tengefu ni pamoja na ujangili, uvunaji wa misitu pamoja na uvamizi wa maeneo ya ushoroba wa wanyamapori.





# Mil. 11/- zatakiwa kutatua tatizo la uhaba maji kijijini

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

UFUMBUZI wa tatizo la kukosekana kwa huduma ya maji katika vitongoji vya Kikwee na Nakayale katika Kijiji cha Koboko Kusini, Kata ya Nasai, Wilaya ya Siha utaigharimu serikali kiasi cha Sh. milioni 11.497

Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Siha, Mhandisi Joyce Bahati, aliyasema hayo, wakati akitoa taarifa kuhusu maendeleo ya mradi huo kwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) mkoa wa Kilimanjaro, Joseph Thadayo.

Alisema shughuli zilizopangwa kufanyika katika mradi huo ni ulazaji wa bomba la maji, umbali wa kilomita 2.2 pamoja na ujenzi wa vituo viwili vya kuchotea maji.

"Kutokana na tatizo kubwa la ukosefu wa maji ambalo linatishia maendeleo ya shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo, tayari mita 750 zimeshachimbwa na kufukiwa kwa nguvu ya wananchi," alieleza Mhandisi huyo ambaye pia ni Kaimu Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa).

Alisema mradi huo umelenga kusogeza huduma ya maji karibu na makazi ya wananchi na lengo ni kuhudumia kaya zaidi 35.

Akizungumza na wakazi wa vitongoji hivyo, Mjumbe huyo wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi, Thadayo, alisema serikali ina nia njema ya kumaliza tatizo la kukosekana kwa maji katika eneo hilo tangu nchi ilipopata Uhuru mwaka 1961, baada ya kupeleka zaidi ya Sh. milioni 197.310.

"Wilaya ya Siha mmepata motisha ya kiasi cha Sh. 197,310,612.53 ambazo ni fedha za programu ya lipa kulingana na matokeo (P4R), baada ya kuwa washindi wa pili kitaifa kwenye utekelezaji wa programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Ndio maana na ninyi watu wa Koboko Kusini mmepata mradi huu," alisema. Kwa mujibu wa Thadayo, Mradi wa Maji wa Lawate/Fuka ambao utahudumia tawi la Kikwee ni miongoni mwa mradi unaotekelezwa kwa fedha hizo za motisha na ulianza kutekelezwa mwezi Aprili mwaka huu.

Naye Suzan Mshanga alisema toka nchi imepata uhuru, wakazi wa Kijiji cha Koboko Kusini, hawajawahi kuona, wala kupata huduma ya majisafi na salama yanayotoka majumbani mwao na kwamba hali hiyo imekuwa kikwazo kwao kufanya shughuli maendeleo kwani wanatumia muda mwingi kutafuta maji na kutembea umbali mrefu.

# Same wahangaikia matibabu nje ya kata

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WANANCHI wa Kata ya Mtii, Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, hawana kituo chochote cha kutolea huduma za afya, jambo ambalo linawalazimu kutumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo nje ya kata yao.

Hali hiyo imemsukuma Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, kwenda kuchochea ari ya wananchi kufanya msaragambo, kuchangia ujenzi wa kituo cha afya na kukabidhi mifuko 100 ya saruji iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira kwa ajili ya kuwaunga mkono.

Wananchi hao, wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 20 kwenda kutafuta huduma hiyo muhimu katika vituo vya afya vilivyopo kwenye kata za jirani.

"Nawapongeza kwa uamuzi wenu wa kuamua kujenga kituo cha afya na hatua ya ujenzi mliyofikia, itumieni saruji iliyoletwa na Mkuu wa Mkoa wetu kwa lengo lililokusudiwa. Mtendaji wa kata hii na watendaji wa vijiji, nitawakamata na kuwaweka ndani kama nitapata taarifa za kuwapo hujuma katika ujenzi huu, jipangeni na simamieni kazi hii imalizike kwa mafanikio," alisema Senyamule.

Wakazi hao wa Mtii hawana huduma za afya, wakati ambapo mwongozo wa taifa wa sekta ya afya kuhusu huduma pamoja na ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, vikielekeza kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Sera ya afya ya mwaka 1990 iliyopitiwa mwaka 2007, imeweka bayana dira, makusudio, maelekezo ya serikali katika mfumo wa mabadiliko ya kiuchumi na kijamii, matokeo ya utafiti na majaribio na uzoefu katika utoaji wa huduma.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Same, Isaya Mngulu, ambaye pia aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), aliwatia moyo wananchi hao akiwasihi kuendelea kuchangia fedha kwa ajili ya kupaka rangi jengo la kituo hicho cha afya, baada ya kukamilika.

"Afya maana yake ni hali ya ukamilifu kimwili, kiakili, kijamii na kutokuwapo kwa maradhi. Sasa kwa kuwa afya bora ni nguzo na rasilimali muhimu katika kuchangia maendeleo ya mtu binafsi, familia na nchi hususan katika kuleta maisha bora na kupunguza umaskini, nawasihi mwendelee kuchangia mradi huu ukamilike," alisisitiza Mngulu.

Diwani wa Kata ya Mtii, Heriel Msollo, akitoa shukrani kwa niaba ya wakazi wake, aliiomba Halmashauri ya Wilaya ya Same iwasaidie kukamilisha jengo hilo na kwamba kiasi cha fedha kinachotakiwa kumalizia ni Sh. milioni 35.



Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Nestory Chilumba, akizungumza kuhusu ujenzi wa bweni Shule ya Sekondari ya Nangoo, katika mkutano na wananchi wa Kata ya Nangoo wilayani humo juzi. **PICHA: HAMISI NASIRI.**

# Uchaguzi S/Mitaa wawaamsha vigogo CCM

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WAKATI serikali ikiwa imetoa tangazo la uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019 utafanyika Novemba 24, baadhi ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wameanza 'mchaka mchaka' wa ukaguzi wa miradi ya ujenzi wa hospitali za wilaya zinazojengwa kwa fedha za umma.

Miongoni mwa vigogo wake, walioanza kupita huku na huko kukagua miradi hiyo kabla ya kupulizwa filimbi ya uchaguzi ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM (NEC) mkoa wa Kilimanjaro, Joseph Thadayo.

Jana Thadayo alikwenda kukagua ujenzi mkubwa wa majengo sita ya Hospitali ya Wilaya ya Siha, ambao umeigharimu serikali kiasi cha Sh. bilioni 1.5.

Hadi kufikia sasa majengo hayo yamekamilika kwa asilimia 95, huku ikielezwa kukamilika kwake kutapunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali za rufani.

"Nimejiridhisha kwamba kazi kubwa imeshafanyika na ninaamini wananchi hawata tumia gharama kubwa na kupoteza muda mwingi kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya. CCM mwaka 2015 waliahidi kuwapatia wananchi huduma bora za afya na sasa inatekeleza kwa vitendo ilani yake, muipe asante kwa kuipa kura nyingi katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaokuja mwezi Novemba," alisema.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Andrew Method, alisema mradi huo utamalizika hivi karibuni ili kuruhusu kuanza kutumika kutoa huduma kwa wagonjwa wanaofikishwa katika hospitali hiyo.

Mradi huo unahusisha majengo mapya ya wodi ya mama na mtoto, jengo la kuhifadhia maiti (mortuary), jengo la mionzi, jengo la utawala, jengo la dawa na jengo la kufulia.

Pia Halmashauri ya Wilaya ya Siha imefanikiwa kukamilisha mradi mwingine wa jengo la kutolea huduma ya bima afya.

Hospitali ya Wilaya ya Siha, inahudumia wakazi zaidi ya 116,313 (kulingana na takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012) kutoka katika vijiji 60 vilivyopo wilayani humo.

Hospitali hiyo ilianzishwa mwaka 2007 ikiwa kama kituo cha afya, baada ya vyama viwili vya ushirika wilayani humo kutoa ekari 40 za ardhi.



Wahitimu digirii wawabunia walima mboga Dodoma 'soko la kiganjani'

Ukurasa 19

UCHUMI



MVUTANO WA CHINA, MAREKANI

## Huawei inabuni mfumo mpya wa 'simu janja' kuziacha Google, Apple

Ukurasa 14


# BUFE

Ijumaa Agosti 30, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




SADC DAR & TANZANIA YA VIWANDA

## Wahandisi, wawekezaji wanaibukia mayowe serikali iwafanye sehemu ya miradi mikubwa

Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

# UCHUMI

MVUTANO WA CHINA, MAREKANI

# Huawei inabuni mfum 'simu janja' kuziacha

- Mbinu China kukabili vikwazo inayowekewa
- Njia ya soko nyeupe, ila mbele kuna ukungu
- Wachina wametawala mauzo, wapinzani soko

**Na Nimi Mweta**

KAMPUNI ya simu inayoongoza kwa mauzo duniani, Huawei, inajitayarisha kutoa mfumo mpya wa kuendesha simu hizo, yaani wa kukusanya mawasiliano na kusambaza bila kutumia vifaa vinavyoundanishwa na kampuni kubwa za Marekani, hasa Google na Apple.

Washindani hao wa kibiashara kimataifa wamekuwa vyanzo vya vifaa muhimu vinavyoingia katika mfumo wa uendeshaji simu kutumike kwa njia ileile, kokote duniani.

Lakini, serikali ya Marekani imeshaweka zuio la kisheria la kampuni za simu za Marekani dhidi ya Huawei, ama kufanya nayo biashara, au hata kuuza vifaa vyake kwa Huawei.

Baadhi ya wachambuzi wanasema, licha ya Huawei kupitia wakati mgumu hivi sasa, bado hali hiyo inaweza isiivuruge sana kampuni hiyo. Inaelezwa kwamba, inajihami kwa kubuni mfumo wake mpya wa uendeshaji wa 'simu janja' bada la tegemezi ilivyokuwa awali.

Hadi sasa inaelezwa, tayari ilishafanya utafiti wa kuwa na mfumo wa aina hiyo, lakini mahitaji ya soko yanaendana zaidi na kuwa na vifaa vinavyoshabihiana na simu za Marekani na kwingineko duniani, hasa katika maeneo hayo ambako vifaa vya Google na Apple vinatawala soko, ila Huawei inaongoza mauzo.

Tayari wachambuzi waangalia jinsi ambavyo mfumo mpya wa uendeshajii wa 'simu janja' za Huawei unaweza kuleta changamoto katika soko la kimataifa katika miaka ijayo na mwelekeo wa kuwezesha ubunifu kujengeka kuwa 'brandi' inayokubalika upo.

Wanatoa mifano ya kukua kwa baadhi ya kampuni kubwa za teknolojia nchini Marekani, kuwa Google iliunda mfumo wa 'Android' bila kuwa na'brandi' (nembo mahsusi) ya simu inayotumia mfumo huo, na 'Microsoft' iliunda mfumo wa kuendesha kompyuta, bila ya kuwa na kompyuta ya aina yake. Ni mifano halisi.

Takwimu zinaonyesha, mfumo wa 'Android' unaendesha asilimia 87 ya 'simu janja' duniani kote, huku mifumo huru ikichukua sehemu iliyobaki ya soko, hali inayoonyesha kuwa soko la uendeshaji wa 'simu janja' siyo rahisi kujipenyeza.

Wachambuzi wanasema kumpatia mlaji vianzio vipya (ukilinganisha na simu za kawaida, vifurushi vipya, michezo, mapana ya mawasiliano) inabidi kuwashawishi, na kwa hali hiyo itakuwa vigumu Huawei kufanikisha hilo. Ila kuna wasiwasi ni kwa kiasi gani ubora wa mfumo huo mpya, pasipo vifaa vyake, hivyo kumudu ushindani.

Hata hivyo, hakuna wasiwasi kama Huawei watafaulu katika soko lao kubwa la ndani, China na kufaulu kiasi fulani kujipenyeza katika soko la dunia.

Mifumo inayotumika China kwa wingi zaidi, haitumii vifaa vya Google, na vingi kati ya vifaa hivyo havipatikani China.

**Soko la China**

Inaelezwa na wataalamu kuwa, hakuna tatizo kwa Huawei kufanikisha mfumo wake na kuutumia nchini humo, ila kutoa changamoto katika soko la kimataifa itachukua muda. Mfumo huo unaweza kuendana na simu za kati hata kama ni 'simu janja' ila ushindani wa simu za ngazi ya juu hautakuwa rahisi.


Mfumo mpya wa Huawei unaoitwa Weibo, unatazamiwa kuanza kutumika nchini humo mwisho wa mwaka huu na wa kutumika kimataifa kuelekea mwisho wa mwaka ujao.

Tayari imeshaandikisha hati miliki katika Umoja wa Ulaya (EU) ya vifaa au mifumo ya uendeshaji wa 'simu janja' nje ya mfumo wa Android.


Bado kuna wachunguzi wanaotazamia au kueleza kama kungekuwapo uwezekano serikali ya Marekani kuondoa vikwazo dhidi ya Huawei, inagerudia mfumo wa kawaida.

Baadhi yao katika mvutano huo wa kiteknolojia na soko, wanaamini

> **Baadhi ya wachambuzi wakereketwa wanasema, ni hatari kutegemea teknolojia ya Marekani, kwa sababu serikali ya Marekani ikiamua 'hili au lile' kampuni zisizo ya ki-Magharibi zinaumia.**




Duka kubwa la huduma za Huawei. PICHA ZOTE: MTANDAO.




Takwimu zinazoonyesha kiwango cha mzigo wa simu za Huawei na hisa z
ya meli iliyosafirishwa nje ya China, kati ya mwaka 2010 na mwaka jana

# ...o mpya wa Google, Apple

inawezekana Huawei ikaunda mfumo wa kutumia 'simu janja' kwa upande wa China na hata isingekuwa na soko la kimataifa, bado ingekuwa moja ya mifumo mikubwa zaidi kutokana na ukubwa wa soko la nchi yao China.

**Google kufungiwa?**

Kuna wasiwasi China inaweza kuchukua hatua za kufungia simu za Apple au kuzuia mtandao wa Google, ili kazi hiyo ifanywe na kampuni nyingine na siyo za Marekani.

Ila hakuna hatua kama hiyo imefikiriwa wazi, ingeongeza mvutano kibiashara kati ya nchi hizo mbili na kuitenga zaidi China katika soko la kimataifa, badala ya kutuliza kasi.

Wako wanaoiona kuwa hatua ya sasa ni nzuri kwa sababu inawezesha China kujitegemea, isiwe inatumia 'vitu vya watu,' lakini hisia hiyo inatofautiana na mwelekeo wa wazi wa serikali ya nchi hiyo ya kupigania utandawazi duniani.

Baadhi ya wachambuzi wakereketwa wanasema, ni hatari kutegemea teknolojia ya Marekani, kwa sababu serikali ya Marekani ikiamua 'hili au lile' kampuni zisizo ya kiMagharibi zinaumia.

Dai lililopo ni hoja za Rais Donald Trump, dhidi ya Huawei kana kwamba tatizo hilo hasa ni la Marekani, yaani kutumia teknolojia kama chombo cha kukamata mawasiliano ya nchi nyingine.



Mtumiaji akiendelea na huduma ya simu ya Apple.

Mwaka huu ulipoanza, simu za Huawei tayari zilianza kukosa kifaa cha 'Playstore' kukusamya aina tofauti za michezo kwa watumiaji wa 'simu janja' kote duniani, ambayo hasa inamilikiwa na Google

Pia, kampuni zinazouziana teknolojia na mifumo na vifaa vya uendeshaji, kujenga mfumo mpya usio na 'apps' zote zilizozoeleka kwa watumiaji kote duniani, hakuelekei kufaulu nje ya China, kwani watumiaji watahitaji kutumiana habari, picha, mikanda au vielelezo vingine kwa mifumo na 'apps' zinazofahamika. Kuanza upya hakuna tija.

**Nje ya Marekani**

Tatizo zaidi ni ushindani wa Huawei katika soko la kimataifa nje ya Marekani, kwa kutumia mfumo usio na vifaa au mifumo ya Marekani, kunabanwa na kampuni takribani zote ambazo ni huru kutengeneza 'apps' za aina tofauti, zinategemea kwa kiwango fulani uhusiano na soko la Marekani.

Hivyo hata katika nchi ambazo zina mifumo ya ziada mbali na Google na Apple, kuwa na uhusiano mzuri na kampuni hizo kutumia mifumo yao na Marekani katika soko la nchi nyingine, ni jambo muhimu .

Ni jambo linalojenga maana kuwa, Huawei haitakuwa na uwezo hivi karibuni wa kuchangia mwelekeo wa soko la 'simu janja' duniani, ila kwao China na wakazi wa China walioko nje, au jamii za Kichina zenye uwezo wa kujumuika katika mtandao ambako watumiaji wengine hasa ni Wachina au ndugu zao wanaokaa nchi nyingine.

Mbele ya safari, kuna shaka ya tatizo kubwa la kimkakati ni nchi ipi itabadilika kwanza hali itulie, kama ni Marekani itabadilika iwe na serikali nyingine isiyokuwa na ugomvi na China au Huawei, au ni China itakayolazimishwa kubadilika.

Licha ya kwamba China haisemi hivyo na ilikanusha taarifa zilizotolewa na msemaji wa Ikulu ya Marekani miezi kadhaa iliyopita, bado ina kila sababu ya kutazamia na hata kujitahidi, kuhakikisha Rais Trump anashindwa katika uchaguzi wa kumpa muhula wa pili mwakani.

Historia haionyeshi kuwa hilo litakuwa rahisi au kuwezekana. Katika miaka 50 iliyopita ni rais mmoja tu nchini Marekani aliyeshindwa kura akitaka muhula wa pili, Jimmy Carter mwaka 1980, kwa Ronald Reagan.




zake sokoni, kulingana na mizigo
.



Wakulima wakizalisha mpunga Nigeria. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Buhari acharuka uvushaji mchele

RAIS Muhammadu Buhari wa Nigeria, ametangaza azma ya kuwa na mkutano na nchi jirani zake, ambao ni Kaskazini Benin na Niger.

Anasema kuwa, lengo ni kuzungumzia hatua za kuchukuliwa kudhibiti biashara ya magendo kuvuka mipaka baina ya nchi zao

Serikali ya Nigeria ilieleza kwamba, Jumatano wiki hii ingefunga sehemu ya Magharibi ya mpaka wake na Benin, ili kuzuia usafirishaji magendo wa mpunga, ambao unatishia juhudi za nchi hiyo kuimarisha uzalishaji wa ndani.

Nchi hiyo inataka kuwa inajitegemea yenyewe katika uzalishaji mpunga na imeweka masharti ya uingizaji mchele, lakini jambo hilo limesababisha bei kupanda na kupelekea usafirishaji kwa njia ya magendo kutoka Benin kuingia Nigeria.

Rais wa Nigeria Muhammadu Buhari, alianzisha sera tangu alipoingia madarakani mwaka 2015, ambazo zinalenga kusitisha uingizaji mchele nchini humo.

Anafafanua kuwa, lengo ni kuimarisha uzalishaji wa ndani na kulinda akiba ya fedha za kigeni ya Nigeria, isitetereke.

Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari, anasema kuwa usafirishaji mchele kwa njia ya magendo kupitia mpaka wa Magharibi umetishia sera yake ya nchi kujitegemea, yenyewe bila msaada wa nje, akimaanisha kuwaondolea njaa wananchi wake.

Kiongozi huyo alikaririwa katika taarifa iliyotolewa na msemaji wake, kwamba serikali yake imeweka akiba kubwa ya fedha za kigeni kutokana na sera yake badala ya kuzitumia fedha chache za kigeni kuagizia mchele kutoka nje.

Anasema kamba hawawezi kuruhusu usafirishaji haramu wa bidhaa katika kiwango hicho kuendelea. Taarifa hiyo haikusema ni lini sehemu ya mpaka huo ulifungwa.

Serikali hiyo inasema uingizaji mpunga na ngano nchini Nigeria kwa pamoja unagharimu takribani Dola za Marekani bilioni nne kwa mwaka.

Anafafanua kuwa, raia wake milioni 190 wanategemea bidhaa zinazoagizwa kutoka nje kwa sehemu kubwa ya mahitaji yao kutokana na upungufu wa uwezo wa uzalishaji nchini humo, kutokana na kidhibiti cha uwezo wa uzalishaji.

Nigeria inadhamiria kukuza kilimo kwa ajili ya kupeleka bidhaa nje ya nchi ili kupata fedha zaidi na kuongeza mapato kutoka nje ya eneo lake lenye utajiri wa mafuta.

**• Habari hii kwa mujibu wa VOA. Ends**



Mchele unaozalishwa Nigeria.

UCHUMI

## SADC DAR & TANZANIA YA VIWANDA

# Wahandisi, wawekezaji wanaibukia mayowe serikali iwafanye sehemu ya miradi mikubwa

- Vilio vya ujuzi, ajira, vyangongana na soko
- Serikaii yakiri kuwapokea, sheria iko jikoni

**Na Beatrice Moses**

PINDI watu wanapopatiwa fursa kutoa maoni chanya, daima kuna mengi yanayoibuliwa kukiwa na mchango chanya kwa maendeleo ya serikali na umma kwa jumla.

Itakumbukwa, kwa miaka mingi sasa serikali ilianzisha utaratibu wa ushirikishaji wahusika katika maamuzi mengi muhimu kitaifa, kama vile bajeti kubeba maoni ya wadau kama vile Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (TIC) na Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA).

Pia, wastani zaidi ya nusu muongo uliopita, ilipitishwa sheria inayoshikamanisha sekta binafsi na umma. Yote hayo yalilenga, kujenga ushirikishwaji wa kila pande.

Ndani ya mtazamo na mustakabali wa aina hiyo, hivi karibuni wawekezaji na wahandisi kwa nyakati, wameiomba serikali kuweka kipengele mahususi kwenye mikataba inayohusu miradi mikubwa ya ujenzi nchini, vitakavyosaidia kuinua uchumi wa nchi na kuwaongezea uzoefu katika sekta ya ujenzi.

Dhana iliyojitokeza ni maoni tofauti ya kitaaluma na kiuchumi, wawekezaji wakieleza haja yao kwa serikali kuweka kipengele cha kisheria kinachowabana makandarasi wa miradi mikubwa ya ujenzi, kama majengo na barabara kununua vifaa wanavyohitaji vya ujenzi nchini, ili kuvijengea uwezo viwanda vilivyopo.

Hali kadhalika, wahandisi nao wameibua mtazamo wa kuitaka serikali kuwabana kisheria makandarasi kutuwatumia wahandisi wazawa kwa kupewa idadi maalum kulingana na ukubwa wa mradi husika, hatua wanayoamini itawasaidia kuvuna uzoefu utakaowawezesha kumudu ujenzi wa miradi kama hiyo kwa siku sijazo.

Ni mawazo ambayo Waziri wa Viwanda na Biashara Innocent Bashungwa, anayapa majibu ya mtazamo mkuu wa kiserikali kwamba, hivi sasa imejipanga kuhakikisha sheria na sera zinazokwaza biashara na uendeshaji wa viwanda nchini, zinapitiwa upya ili zirekebishwe.

Akizungumza katika Maonyesho ya Awamu ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Bashungwa anaeleza, hatua hiyo itasaidia kufanikisha maono ya Rais Dk. John Magufuli kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Kwa mujibu wa Waziri Bashungwa, muswada utokanao na mapitio ya sheria na sera zinazohusiana biashara, zitapelekwa katika kikao kijacho cha Bunge, ili kufanyiwa marekebisho sahihi.

**Mwekezaji anena**

Mkurugenzi wa kampuni ya Lodhia Group, Sailesh Pandit, anasema kutokana na msamaha wa kodi unaotolewa kwa makandarasi, imewachochea kununua vifaaa hivyo ikiwamo nondo, nje ya nchi, hatua inayoingiza mzizi wa kudhorotesha viwanda vya ndani.

Akizungumza kiwandani kwake wilayani Mkuranga, mkoa wa Pwani hivi karibuni, Pandit aliwambia wajumbe wa mkutano wa SADC walioondoka hivi karibuni kwamba ni athari inayopunguza fursa za ajira kitaifa, kwani viwanda vinalazimika kuzalisha bidhaa chache kulingana na uhalisia wa soko.

"Kwa sasa wafanyakazi wetu wanazalisha kwa saa nane pekee, lakini tungekuwa na uhakika wa soko, ni wazi kwamba tungekuwa tunafanya uzalishaji wa bidhaa nyingi, hivyo tungelazimika kuajiri wengi pengine hata mara mbili ya waliopo sasa,"anasema Pandi.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, ameajiri wafanyakazi 600, huku kiwanda hicho kuwa na uwezo wa kuzalisha tani 10,400 kwa mwezi na kinazingatia kiwango cha ubora Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

"Ni jambo la kushangaza, tunafanikiwa kuuza nje ya nchi hadi tani 2,000 huko katika nchi ya Kongo (DRC). Tunatarajia kujitanua zaidi kwenye nchi nyingine, wakati nchini kuna miradi mikubwa inaendelea tungeweza kuuza zaidi bidhaa zetu," anasema.

"Miradi hii mikubwa inayotekelezwa nchini kwa sasa ni ya reli ya kisasa ya kati (SGR), mradi wa umeme wa Rufiji, tulitegemea viwanda vya ndani kikiwamo hiki, tuuze kwa wingi bidhaa zetu, lakini imekuwa sivyo," analalamika Pandit.

**Sauti ya serikali**

Katika ziara hiyo, Mhandisi wa Viwanda nchini, Kamara Gombe, akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, anasema serikali inajipanga kutengeneza fursa zaidi kwa viwanda vya vyuma nchini, kutokana na upana wa mahitaji yake.

Anakiri serikali imeshapokea maombi kutoka kwenye viwanda vya vyuma nchini iongeze kodi ya forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa bidhaa za vyuma zinazoingia nchini, hatua wanayoamini itasaidia kukuza soko na bidhaa zinazozalishwa.

Mhandisi huyo anataka takwimu za mahitaji ya vyuma nchini kwa mwaka; nondo tani 300,000 wakati viwanda nchini vinazalisha tani 200,000. Hata hivyo, anasema kuna uzalishaji ulioongezeka kutokana na mwitikio mzuri wa baadhi ya viwanda, kikiwamo cha Lodhia.

"Kiwanda hiki kimekuwa cha mfano, kwani ni cha kwanza kuzalisha malighafi kwa ajili ya kutengeneza chuma, zikiwamo bidhaa kama nondo, tofauti na kampuni nyingi zinazozalisha nondo hapa nchini zinaagiza malighafi kutoka nje ya nchi, "anasema.

Mgeni Mwanasadc Renatus Joseph, kutoka nchini Afrika Kusini, akizungumzia katika ziara hiyo, anabainisha kuwa licha ya changamoto za masuala ya gharama za umeme kitaifa, naye anaungana kukiri kuna uwekezaji mkubwa umefanyika kitaifa.

Anasema ni hatua inayoonyesha dalili nzuri kwa Tanzania kusonga mbele katika sekta ya viwanda na kuifikia Afrika Kusini inayotegemea viwanda katika ukuaji wake kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, anasema ni jukumu la serikali kuendelea kuboresha mazingira ili kuvutia wawekezaji wa viwanda, hivyo hatua zinazidi kuchukuliwa kuhakikisha azma hiyo inatimizwa.

"Sisi Mkuranga tumejipanga vyema, kuna maeneo mengi yametengwa kwa ajili uya ujenzi wa viwanda vikubwa, tunakaribisha wawekezaji kutoka nchi mbalimbali ikiwamo za SADC kuja kuwekeza," anasema Sanga.

**Wahandisi nao?**

Dai la wahandisi ni kuitaka serikali kuwekeza kwenye miradi mikubwa ya ujenzi kama reli ya kisasa na barabara za juu maarufu 'fly over' inayotekelezwa nchini, na ihakikishe uwapo wao wahandisi na wanafunzi wa fani za ujenzi wa nchini, hali itakayowasaidia kupata ujuzi zaidi.

Alipokuwa katika ziara ya kutembelea Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) siku kadhaa zilizopita, Katibu Mtendaji wa Taasisi ya Wahandisi, Ipyana Moses, alieleza kubaini ushiriki mdogo wa wahandisi wazawa kwenye miradi hiyo.

Hivyo, anasema wamewasiliana na serikali kuona namna inavyoweza kubadilisha sera miongozo kwenye mikataba ya awali, kutoa fursa kwa wataalamu wenyeji.

"Wahandisi Watanzania wanapaswa kuwekewa nafasi ya kushiriki moja kwa moja kwenye miradi hii mikubwa, ikiwezekana bajeti iwe inaongezwa kidogo kuwawezesha, ili waweze kuwa na bidii ya kujifunza itakayosaidia kuongeza ujuzi wao hivyo kuwajengea uzoefu.

"Wenzetu madaktari mafunzo yao ya vitendo ni kwenye hospitali, kwa hiyo kwetu sisi ushiriki kwenye miradi kama hii ndiyo sehemu ya kujifunza zaidi," anafafanua.

Anasema, taasisi yao ina jukumu la kuwaunganisha wahandisi wote nchini wajifunze na kushauri cha kufanya, ili kumudu mahitaji ya soko, pia kufikia Tanzania ya Viwanda.

Mshauri wa masuala ya ujenzi wa nyumba na barabara, Erasto Machume, anasema wataalamu wa ujenzi wa barabara wanaelemewa na tatizo la vitendea kazi na uzoefu.

Anasema, kwa Tanzania barabara za juu ya kwanza kujengwa ni daraja la Mfugale, iliyopo katika eneo laTazara jijini Dar es Salaam, hivyo kuna vifaa ambavyo baadhi ya wahandisi mchini waliviona kwa mara ya kwanza.

"Tukitafuta namna ya kuwa na mitambo tunaweza, hawa hawakutoka mbinguni ni watu wamesoma kwenye vyuo tulivyosoma sisi. Wanachotuzidi ni vifaa," anasema Machume na kuhitimisha:

"Kushiriki kwenye miradi hiyo mara nyingi hivyo wamechota uzoefu, kwa hiyo hata sisi tunaweza kujenga kama tunakuwa na vifaa vinavyohitajika."



*Wajumbe wa mkutano wa SADC uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni, walipotembelea kampuni ya Lodhia Group inayotengeneza nondo, wilayani Mkuranga. **PICHA: BEATRICE MOSES.**

> **"Sisi Mkuranga tumejipanga vyema, kuna maeneo mengi yametengwa kwa ajili uya ujenzi wa viwanda vikubwa, tunakaribisha wawekezaji kutoka nchi mbalimbali ikiwamo za SADC kuja kuwekeza," anasema Sanga.**



Daraja la Mfugale, moja ya maeneo wahandisi wamedai mahali sahihi pa kujifunza. **PICHA: MTANDAO.**

# BIASHARA KATIKA PICHA



Mfanyabiashara wa viungo vya chakula, akisubiri wateja katika makutano ya Mtaa wa Mkunguni na Bonde, eneo maarufu kwa biashara hiyo, Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**



Mchuuzi wa mapera akiwa ameyasheheni kwenye baiskeli yake, wakati akisaka wateja katika Barabara ya Kivukoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akizungumza wakati akifungua mkutano wa wafanyabiashara na wasindikaji wa mazao ya nafaka, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WK**

UCHUMI



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Profesa Palamagamba Kabudi, akiwasilisha hoja katika kikao cha SADC, kilichobariki Kiswahili. Picha nyingine, wajumbe walipokuwa mkutanoni. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

TOKA JK 'KULIANZISHA' AU...

# Mcheza kwao JPM ameingiza bidhaa Kiswahili soko la SADC

- ADB yaridhia matumizi yake chapchap
- Kabudi afungulia, Dk.Shein akamilisha
- Mtaalamu Dk. Khatib aweka angalizo

**Na Beatrce Moses**

"MCHEZA kwao hutunzwa." Ni msemo wenye ujumbe mzito, unaoweza kutumika kuelezea hatua ya mafanikio ya kampeni iliyoanzishwa na Rais Dk. John Magufuli kupigia debe matumizi ya lugha ya kiswahili.

Rais Dk. Magufuli ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), amezichanga vyema karata zake katika kampeni ya kupigia debe Kiswahili kipewe nafasi ya kuwa lugha rasmi ya nne kwenye shughuli za jumuiya hiyo.

Sasa heshima hiyo haishi kwa maana ya lugha tu pekee, lakini ni bidhaa katika lugha jumumu hilo ambalo ni mahsusi kiuchumi.

Tayari Benki ya Maendeleo Afrika (ADB)imeshapitisha rasmi kuwa lugha rasmi katika shughuli zake kibiashara, huku Afrika Kusini, inaingia katika mchakato ifundishe na kutumika.

Hao wote wanaungana na uamuzi uliofikiwa miaka kadhaa iliyopita, kulihalalishwa katika kikao cha Umoja wa Afrika (AU), kutoka kwenye juhudi kubwa ya mtangulizi wake, Rais Mstaafu Jakaya Kikwete.

Mnamo Agosti 18 mwaka huu, akitoa hotuba yake wakati wa kufunga mkutano wa SADC jijini Dar es Salaam, Rais Dk. Magufuli, alieleza kukifanya Kiswahili lugha rasmi ya nne katika Jumuiya hiyo, ni furaha kwa kuwa ilitumika kwenye mafunzo ya harakati za ukombozi.

Pia, anasema ni heshima kwa Mwalimu Julius Nyerere aliyeongoza harakati za ukombozi zilizofanywa na wapigania uhuru barani Afrika, kutokana na upendo wake kwa mataifa mengine ya Afrika, alikubali taifa na wananchi wake wateseke ili kufanikisha ukombozi huo.

Rais Dk. Magufuli anakitumia Kiswahili kutoa hotuba yake hiyo, anaeleza Tanzania imekuwa ikifanya juhudi kubwa kuhakikisha amani na utulivu, inapatikana kwa nchi za Bara la Afrika.

Anatoa mfano, mwaka 1975 Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) liliienda nchini Shelisheli kuzima mapinduzi na kiongozi wa kijeshi nchini, alishikilia uongozi wa nchi hiyo kwa muda mfupi.

Rais Dk. Magufuli anabainisha kwamba, Kiswahili kitasaidia ushirikiano na utengamano wa wananchi: "Tunapaswa kuitumia lugha ya Kiswahili, viongozi wa nchi za SADC kuiga mfano wa nchi ya Afrika ya Kusini, ambayo kuanzia mwakani itaanza kufundisha Kiswahili katika shule zake."

Anathibitisha utayari wa Tanzania kusaidia kufanikisha malengo ya kufundisha lugha hiyo.

Wakati alipofungua mkutano huo alitumia Kingereza kuwashawishi viongozi wenzake wamruhusu kutoa hotuba yake ya ufunguzi kwa lugha ya Kiswahili na baada ya kupitishwa alitamka:

"Mniruhusu nitoe hotuba yangu ya ufunguzi kwa lugha ya Kiswahili. Kwa kufanya hivyo mtashawishika kukubali na kukipitisha Kiswahili kuwa lugha rasmi ya SADC ni lugha iliyotumika kufundisha wakati wa harakati za ukombozi."

Rais Dk. Magufuli anasema tayari Kiswahili kinazungumzwa kwenye nchi 34 za Afrika, kati ya hizo sita ni za SADC.

Kupitia uenyekiti wake, alitumia vyema ardhi ya nyumbani 'kuchombeza' na vionjo vya faida na umuhimu wa matumizi ya lugha hiyo.

**Mswahili Seif Khatib**

Dk. Mohammed Seif Khatib, ni mwanasiasa na mtaalamu wa lugha hiyo, anampongeza Rais Dk. Magufuli kuipigia Kiswahili kuwa rasmi ndani ya SADC.

Kiongozi huyo aliyewahi kuwa Waziri katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), anabainisha kuwa juhudi zinazofanywa zitakuwa na manufaa, iwapo utekelezaji wake utafanywa kwa mikakati madhubuti .

Anabainisha kuwa, katika miaka sita iliyopita nchi za AU zilikubaliana kuwa Kiswahili zilianza kutumia kama lugha kuu barani Afrika.

Hata hivyo, anaeleza shaka yake katika utekelezaji, akidai iwapo haitosimamiwa vyema, kuna uwezekano maagizo yaliyotolewa AU, ni vyema nafasi ya uenyekiti Tanzania ijipange vyema kuhakikisha linatekelezwa kwa mafanikio yaliyokusudiwa.

"Tumepata bidhaa nzuri ya kuuza, Kiswahili ni bidhaa, Rais Magufuli amekuwa mfano," anasema, huku akiwataja viongozi kadhaa waliojitokeza kuunga mkono kampeni hizo za Rais Magufuli.

**Kabudi alivyochangamka**

Katika nafasi ya pekee anatajwa Waziri wa mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, aliyehakikisha anasimamia uwezeshaji mapendekezo ya lugha hizo kuwa rasmi SADC.

Akiwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Profesa Kabudi, aliwaambia wanahabari kuwa, Baraza la Mawaziri la SADC, lilivyowasilisha mapendekezo yake kwenye mkutano huo.

Anabainisha, Kiswahili ni miongoni mwa ugha kubwa duniani, tangu kuanzishwa kwa SADC nchi wanachama zimekuwa zikitumia lugha tatu pekee ambazo ni Kiingereza, Kireno na Kifaransa.

Profesa Kabudi anasema, wajibu wa baraza hilo ni kutoa mapendekezo yanayopelekwa kwa wakuu wa nchi wanachama kwa ajili ya kuyatolea maamuzi.

"Kwetu ni heshima kubwa, Kiswahili ni lugha ya ukombozi, sasa lugha yetu ikipitishwa itakuwa lugha rasmi ya nne katika jumuiya yetu, hii ni kama wakuu wa nchi wataafiki," anasema Profesa Kabudi

**Dk. Shein ajitosa**

Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, naye alijiunga kupiga debe la Kiswahili alipofunga Maadhimisho ya Maonesho ya Nne ya Wiki ya Viwanda SADC.

"Hii ni hatua muhimu katika kuimarisha umoja na mshikamano kwa wanachama wa jumuiya hii, pamoja na kukuza shughuli za biashara na viwanda," anasema.

Anaeleza kuwa historia inaonyesha kwamba Kiswahili kimeweza kuwaunganisha Watanzania kuwa pamoja na anafafanua kwamba itarahisisha mawasiliano na kukuza biashara katika kwa nchi za SADC.

"Kwa hivyo, wazo la kukifanya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha rasmi za SADC ni muhimu na vyema tukaungana katika kulifanyia kazi suala hili," anasema.

BIASHARA



Mkurugenzi wa Ijen Agripreneurship, Wilfred Ngalaba, akijadiliana jambo na wafanyakazi wenzake.

# Wahitimu digirii wawabunia walima mboga Dodoma 'soko la kiganjani'

## • Wasahaulishwa wadudu kuharibu mazao shamba

**Na Renatha Msungu, Dodoma**

KUTOKANA na serikali hivi sasa kusisitiza suala la uchumi wa viwanda, kundi la vijana waliohitimu vyuo mbalimbali vya juu nchini, wameanzisha umoja ujulikanao 'Ijen Agripreneurship' lengo lake ni kusaidia kuboresha vikundi vya wajasiriamali wa mboga katika maeneo mbalimbali nchini.

Ni kikundi kinachojumuisha wataalamu wa kilimo, na ufugaji waliounda mfumo unaoitwa 'Ijen store' ambao ni soko la kiganjani unaolenga kuwafikia wajasiriamali katika bustani zao kununua mboga shambani zikiwa bado katika hali nzuri.

Inaelezwa kuwa na manufaa ya kuwasaidia kupanua soko la mazao shambani, lengo ni kuunda umoja kuwasaidia vikundi vya wakulima wa mboga katika utunzaji wa bustani za kilimo cha mboga, ambazo nyingi huanza kuharibiwa na wadudu kabla ya kufika sokoni.

Umoja huo unatembelea vikundi vya wajasiriamali katika mikoa mbalimbali kuwafundisha jinsi ya kuhudumia mboga hizo, pamoja na kuwaelekeza kujiunga na soko la kiganjani, linalowasaidia kupata soko haraka kutoka kwa jamii inayowazunguka.

**Mkurugenzi Ijen**

Mkurugenzi wa Ijen Agripreneurship, Wilfred Ngalaba, anasema soko la kiganjani limeanzishwa kuwakwamua wakulima wa mboga na hasara wanazozipata shambani.

Ngalaba anasema, wajasiriamali wengi shambani hawajui jinsi ya kukabiliana na changamoto hiyo na ndio maana wameanzisha soko hilo, ili kuwasaidia wajasiriamali kuuza mboga zao kupitia soko hilo la kiganjani.

Anasema, ni jambo linalotazamiwa kuleta tija kwa wajasiriamali wengi wanaoendesha kilimo hicho cha mboga, kupitia kazi ya umoja huo.

Wanachofanya ni kutembelea vikundi vya kilimo, wakiwashauri na kuwafundisha jinsi ya kujiunga na soko la kiganjani, hali itakayowasaidia kuinua kiwango cha biashara hizo, ambazo ndizo shughuli zao za kila siku bustanini.

Anafafanua kuwa zaidi ya soko la kiganjani, pia itakuwa mbinu mbadala kwa wakulima wa mboga kutokana na kwamba linaongeza thamani ya mboga ambazo baadae zitapelekwa sokoni.

"Soko la kiganjani linakwenda kuwa suluhisho la wakulima wa mboga, kwa sababu kila mmoja anakwenda kufaidika akianza kulitumia," anasema Ngalaba.

Faida nyingine wanayoitaja ni wakulima hao kufaidika kupitia soko hilo kusaidia upatikanaji kirahisi wa bidhaa, kwa sababu wahitaji wanawafuata waliomaji walioko shambani na kisha wanazitawanya kwa wateja.

Mkurugenzi huyo anasema, hivi sasa taifa linapoelekea kwenye Uchumi wa Viwanda, ni muhimu kwa jamii kutambua masoko ya aina hiyo ambayo yanaweza kusaidia kuhudumia jamii kwa kiasi kikubwa, ndani ya muda mfupi.

**Meneja Masoko**

Cynthia Lelo, ndiye Meneja Masoko anayesema kuwa lengo la kuanzisha soko hilo, ni kuwaelimisha wakulima wa mboga, ikiwamo kuwarahisishia upatikanaji soko la bidhaa hizo kutoka kwenye jamii zenye uhitaji.

Anafafanua zaidi kuwa, hivi sasa wakati jamii inaingia katika soko la ushindani na baadhi ya nchi jirani, soko hilo linakuwa na nafasi ya kuwa kichocheo cha ushindani kwa wakulima, kwa sababu litawasaidia kusambaza bidhaa zao kirahisi.

"Baada ya kuona changamoto wanazopitia wakulima wa mbogamboga tukaamua kuanzisha 'Ijen Store' ambayo ni mbinu mbadala ya kuepuka kupoteza mbogamboga," anasema Cynthia Lelo.

Anafafanua imani yake kuwa, mfumo huo utawajenga wakulima, ikiwamo kuzalisha bidhaa na kuzitafutia soko haraka hapa nchini, jambo linalowasaidia wakulima hao wa mboga.

Anafafanua kuwa, soko hilo la kiganjani ni moja ya mbinu muhimu kwa wajasiriamali wanaoendelea na kilimo cha mboga katika maeneo ya Dodoma, ndani na nje ya jiji.

Kwa mujibu wa bosi huyo wa masoko, lengo lao ni kuona wakulima wanafahamu maana ya soko kiganjani, ikiwamo jinsi ya kulitumia lilete faida kwa jamii kwa ujumla

Cynthia anasema,vikundi hivyo baada ya kupewa mafunzo, wamekuwa wakiwafundisha wenzao wegine jinsi ya kutumia soko ambalo itakuwa moja ya njia ya kuwapunguzia hasara, itokanayo na uharibifu wa wadudu wanaokula mazao shambani, kabla hayajaingia sokoni.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk Binilith Mahenge na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk Rehema Nchimbi, walipotembelea banda la maonyesho ya kazi za Ijen Agripreneurship. **PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU.**

Cynthia anasema, moja ya mikakati waliojiwekea ni pamoja na kutumia vitu mbalimbali kwa ajili ya kuwafikia wakulima wa mboga, kwa sababu itawasaidia wakulima kujua wanachokifanya.

Anasema, malengo yaliyopo ni kuona vikundi vya kilimo vinapata uelewa wa kutumia soko ambalo ni njia rahisi ya uuzaji wa bidhaa za mboga kwa jamii inayozunguka.

**Wakulima wasema**

Baadhi ya wakulima wa mboga wanasema soko hilo ni zuri, endapo litawafikia wakulima wa mboga katika maeneo wanayolima bidhaa hizo, kwa sababu linawasaidia kupata soko.

Manzala Joseph, anasema soko la kiganjani ni muhimu kwao, kutokana na ukweli linawafuata waliko shambani, jambo ambalo ni rahisi kwa sababu linaondoa adha ya kuwatafuta wateja mmoja mmoja mtaani. Anasema, wanafurahi kuona Ijen imebuni soko la kiganjani, linalolengo kuwakomboa wakulima wa mboga.

Mwingine ni Zacharia Jonas, anasema soko hilo ni zuri iwapo mkulima atajua jinsi ya kulitumia, kwa sababu linamrahisishia kuuza bidhaa zake, kwa sababu mboga zinafuatwa bustanii.

Ukiacha hilo soko hilo ni vema wakulima wa mboga mboga wakalijua hilo kwa sababu linapunguza gharama ya kwenda kuzunguka kila kona kwa lengo la kutafuta wateja kwa ajili ya kununua bidhaa hizo.

UCHUMI

**Na Sabato Kasika**

## UNAJUA?

# Uwekezaji wa 'haba na haba hujaza kibaba' wapigiwa debe




Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS, Daudi Mbaga, akitoa mada juu ya uwekezaji wa pamoja kwa wafanyakazi kutoka taasisi mbalimbali. **PICHA: MTANDAO**

Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa Mfuko wa Uwekezaji (UTT-AMIS), Daud Mbaga, anasema hisa katika masoko ya fedha, daima haiwekwi sehemu moja akitumia mfano kama 'mayai kikapuni.'

Anasema uwekezaji unazidi kukua ukiwa katika kanuni ya makubaliano ya pamoja ya jumuiya, ambayo mara nyingi ni katika thamani ya mwanzo ya kipande na sehemu za kuwekeza.

UTT- AMIS, ni taasisi ya kiserikali inayoendesha mifuko kadhaa ya uwekezaji wa pamoja nchini, ikiwamo: Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza Maisha, Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Kujikimu na Mfuko wa Ukwasi.

Katika kanuni, mtu anaweka kadri anavyoweza, lakini ni busara kuitawanya mitaji na kuzipa muda wa kukua. Kiasi cha chini katika uwekezaji wa mashirika hayo ni Sh.10, 000 kwa kila mfuko, isipokuwa Mfuko wa Ukwasi, unaoanzia Sh. 5,000.

"Cha msingi ni kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa, ikizingatiwa kuwa lengo ni kupata faida. Kwa mfano kwenye hisa na katika masoko ya fedha, katika dunia ya uwekezaji, hakuna sababu ya kuweka mayai yote katika kapu moja," anasema Mbaga, akizitaja ni mbadala wa vibubu, uwekezaji usio na changamoto zilizopo kwenye vicoba. Anasema, kupitia utaratibu huo, mwekezaji anapata faida kila siku, pia anapewa fursa kuchagua mfuko kutokana na malengo yake, akitoa mfano wa Mfuko wa Umoja, kwa ajili ya kukuza mtaji wa Jikimu, wenye gawiwo mara nne kwa mwaka.

"Inawezekana ukawa ni Mfuko wa Watoto ambao unahusu elimu na maisha baada ya kufuzu na pia Mfuko wa Ukwasi, unaohusu kipato cha muda mfupi wa kati na mrefu, yote hiyo mtu anaweza kuwekeza," anasema.

### UFAFANUZI ZAIDI

Mbaga anasema, hasara katika hilo inapunguzwa, kwani msimamizi wake anatamka kuwa 'mtaalamu mbobezi' na anaongeza:"Watu pia wanajiuliza akaunti ya muda maalumu ni nini na hati fungani ni nini? Maswali hayo na jinsi ya kushiriki katika uwekezaji huo, ambao mengi yake ni faida."

Mkurugenzi anafafanua kuwapo faida nyingi, ikiwamo kujiunga hakuzingatia kipato cha anayejiunga.

"Cha msingi ni kwamba hata mwenye Sh. 5, 000 hadi 10,000 anaweza kuwa mwekezaji na anaweza kuwekeza mara nyingi vile anavyoweza bila kujali muda, hivyo basi mwenye biashara anapata faida kila siku," anasema.

Mbaga anasema uwekezaji ni jambo linalohitaji muda kukabiliana na mawimbi ya thamani. Anasema: "Gharama za uwekezaji zinapungua kwa kiasi kikubwa, tukiwekeza pamoja, sote tunajua tunalipa nauli kubwa kama tukisafiri peke yetu kwa teksi kuliko tukisafiri pamoja kwa daladala," anasema.

Anaongeza kusema: " Pia tunapata punguzo dogo zaidi tukijadili bei kwa bidhaa chache kuliko tunapojadili manunuzi ya bidhaa nyingi. Kilo moja inapunguza asilimia mbili, lakini kuanzia kilo 10 kuendelea asilimia nne, hivyo pesa zikiwa nyingi zinaongeza nguvu ya majadiliano."

> **"Meneja anatakiwa awe amebobea, awe na ufanisi wa hali ya juu, awe mkweli anayefuata masharti ya uwekezaji. Kwa mfano, kampuni ya UTT AMIS ni ya serikali na ipo tangu mwaka 2003 na ilianzisha uwekezaji wa pamoja mwaka 2005 na kwa kipindi chote hicho imekuwa ikifanya vizuri zaidi," anasema.**

Anasema fedha zikiwa nyingi zinampa mtu nafasi ya kufanya uwekezaji, ambao peke yake usingeweza kwa pesa chache akitolea mfano hati fungani, hisa na akaunti za muda maalumu ni vitu vinavyohitaji kuanzia kiasi cha fedha.

Mkurugenzi huyo anasema, zaidi ya hapo, mwekezaji anapewa fursa ya kuchagua mfuko kutokana na malengo yake. Mfano Mfuko wa Umoja kwa ajili ya kukuza mtaji, Jikimu wenye gawiwo mara nne kwa mwaka.

Anataja mfuko mwingine kuwa ni wa Watoto ambao unahusu elimu na maisha baada ya kufuzu na pia mfuko wa Ukwasi, unaohusu kipato cha muda mfupi wa kati na mrefu.

### CHANGAMOTO

Anakiri pia kuwapo changamoto, ikiwamo wawekezaji kumpa fedha meneja awekeze kwa niaba yao, ambaye wakati mwingine siyo mbobezi na mkweli.

"Meneja anatakiwa awe amebobea, awe na ufanisi wa hali ya juu, awe mkweli anayefuata masharti ya uwekezaji. Kwa mfano, kampuni ya UTT AMIS ni ya serikali na ipo tangu mwaka 2003 na ilianzisha uwekezaji wa pamoja mwaka 2005 na kwa kipindi chote hicho imekuwa ikifanya vizuri zaidi," anasema.

Anataja changamoto nyingine katika uwekezaji, ni watu kutotambua mojawapo ya sehemu fedha zinawekezwa kwenye hisa, pia hisa zinapanda na kushuka na hisa ni kioo cha vipande kwa mifuko yenye asilimia fulani ya hisa katika uwekezaji wa mtu.

"Hisa zikishuka, thamani ya mfuko inashuka pia. Thamani ikishuka mwekezaji na hata meneja wanapata kidogo. Hivyo meneja ni lazima awe makini kwenye kuchagua ni hisa zipi anunue," anasema.

Mbaga anasema, ni kawaida serikali au mtu binafsi anakuwa mwanzilishi, kisha fedha zitakazowekezwa zitatoka kwa wawekezaji na mwanzilishi atapata faida na mara huwa haifiki zaidi ya asilimia mbili ya thamani ya kiasi kilichowekezwa.

"Wawekezaji wakiwa wengi fedha zitakuwa nyingi na kuweza kufidia gharama za lazima na gharama nyingine za uendeshaji, na kama kuna madeni, ni lazima uwiano kati ya mtaji na madeni uwe mzuri," anasema.

Anasema inaweza ikatokea kufilisika, na kusababisha kutoa mali zote zilizowekezwa kukiwa na bado kuna uwekezaji haujawiva, na kwamba UTT AMIS inasimamia takriban Sh. bilioni 280 na kila siku inazidi kupanuka.

Inawezekana kukawa na mabadiliko katika sera za uwekezaji, hali ya uchumi wa nchi na mabadiliko yakiwamo ya kutoa fedha katika uwekezaji wa muda mrefu na kwa ajili ya kuwekeza muda mfupi, au mfupi kwenda muda mrefu.

"Muda wa kwanza wa kuwekeza ukiisha inabidi uwekezaji uendeleee na pengine riba kwa wakati huo zinakuwa zimeshuka, aidha kwa soko la awali au la pili na kupungua kwa thamani ya fedha, mfumuko wa bei," anasema.

# Wadau usafirishaji kujadili mapendekezo ya rasimu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa usafirishaji katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Kusini wamekutana kwa ajili ya kujadili na kutoa mapendekezo ya rasimu za usafirishaji zitakazowezesha kuandaa kanuni mpya zitakazoanza kutumika na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

Akifungua mkutano huo wa wadau uliofanyika jijini Mbeya, Mkurugenzi wa huduma za Uchukuzi kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Haruni Kisaka, alisema wameandaa rasimu nane kwa sasa zinajadiliwa na wadau na zikikubaliwa na waziri mwenye dhamana zitakuwa kanuni rasmi.

Mhandisi Kisaka alisema kuwa miongoni mwa rasimu ambazo zimeandaliwa na zinajadiliwa ni ya kuwatambua na kuwasajili madereva na LATRA itaweka mkataba na madereva badala ya wamiliki kama ilivyo sasa.

"Rasimu hii inatoa fursa kwa wamiliki, madereva na wadau wengine wa usafirishaji kujadili na kutoa mapendekezo yao ili kanuni zitakazopitishwa ziwe rafiki na kuepusha malalamiko utakapoanza utekelezaji wake," alisema Mhandisi Kisaka.

Aliongeza kuwa kanuni ya kuwatambua na kuwasajili madereva ikipita itakuwa msaada kwao kwani wataweza kushughulikia malalamiko, tozo na kuanzisha mafunzo mbalimbali.

Baadhi ya wamiliki na madereva wa usafirishaji mkoani Mbeya walisema kuwa endapo rasimu hiyo itapatishwa na kuwa kanuni rasmi itasaidia vikwazo vilivyopo sasa ikiwa ni pamoja na kuwashughulikia madereva ambao walikuwa wakifanya makosa makusudi wakidhani kuwa watakaoshughulikiwa ni wamiliki.

Walisema wamefurahishwa na kipengele cha usajili wa madereva katika rasimu hiyo kwa madai kuwa itasaidia kuwakamata na kuwalipisha faini pindi wanapofanya makosa na kutoroka badala ya kuwalipisha faini wamiliki wa vyombo vya moto.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Meloe Bulema, alipendekeza kuanzishwa kwa chuo maalum cha makondakta ili kuwajengea uwezo wa kufanya kazi zao kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kutambulika.

Alisema makondakta wengi hawana uzoefu na kazi yao kwa sababu wanatafutwa kiholela na madereva hali inayosababisha kuwanyanyasa abiria hususani wanafunzi.

# Makondakta watakiwa kuwa na vitambulisho vya wajasiriamali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UMOJA wa Wamiliki wa Mabasi Barabara kuu ya Mbeya- Tunduma (Uwambetu), wametoa siku tatu kwa makondakta wa magari ya kusafirisha abiria kuwa na vitambulisho vya wajasiriamali.

Maagizo hayo yalitolewa juzi na Katibu wa Umoja huo, Leopard Mwanyika, wakati wa kikao kilichowahusisha, Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, makondakta, madereva, maofisa wasafirishaji, wapiga debe, watendaji wa kata ambacho kilifanyika katika stendi kuu ya mabasi ya mkoa.

Mwanyika alisema agizo hilo ni sehemu ya kuunga mkono agizo la Rais Dk. John Magufuli, ambalo linamtaka mtu yeyote anayefanya biashara zake kwa mtaji chini ya Sh. milioni nne kuwa na kitambulisho cha wajasiriamali.

Alisema makondakta ni miongoni mwa kundi hilo, hivyo wanapaswa kuwa na vitambulisho na kwa kuanzia umoja huo walitoa Sh. milioni 1.5 kwa ajili ya kuwanunulia vitambulisho makondakta 75.

Alisema lengo ni kuhakikisha makondakta wote 250 wanaosafirisha abiria kuanzia Mbeya hadi Tunduma wanakuwa na vitambulisho ambavyo vitagharimu kiasi cha Sh. milioni tano.

"Tulibaini kundi la makondakta ni sehemu ya wajasiriamali wanaopaswa kuwa na vitambulisho, lakini hawana, hivyo kupitia umoja wetu tumeona ni vyema tukahamasisha ili kuunga mkono juhudi zake za kuleta maendeleo kupitia kodi zetu naamini suala hili litafanikiwa serikali itajipatia mapato," alisema Mwanyika.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, James Kasusura, alipongeza hatua ya wamiliki hao kuwanunulia vitambulisho makondakta wao kwa madai kuwa ni cha kizalendo.

Aliwahakikishia makondakta wote kuwa watendaji wamejipanga kuwahudumia na kuwasisitiza kufika katika maeneo yanayowazunguka ili kupata vitambulisho hivyo.

Alisema vitambulisho hivyo vitawasaidia makondakta kufanya kazi mahali popote nchini hivyo wavitunze ili kuepuka usumbufu.

Miongoni mwa makondakta hao, Jacob Amanyisye, alishukuru wamiliki hao kuwanunulia vitambulisho, lakini alisema haoni sababu ya kuwa na vitambulisho hivyo kwa sababu magari wanayofanyia kazi yamekidhi vigezo vyote vya kulipa ushuru na tozo mbalimbali.



Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma (wa pili kushoto), akijadiliana jambo na Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Andrea Tsere, wakati alipotembelea na kukagua Mahakama ya Wilaya hiyo mkoani Njombe jana. **PICHA: LYDIA CHURI.**

# Vijana 39 wanufaika mradi wa YESB

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

JUMLA ya vijana 39 ambao wanaishi kwenye mazingira magumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wamenufaika na Mradi wa Vijana wa YESB unaofadhiliwa na Shirika la CRS, unaofanya kazi ya kuwapatia mafunzo ya ufundi, ujasiriamali, uhasibu na namna ya kuandika miradi ili wanufaike na mikopo inayotolewa na halmashauri.

Hayo yalisemwa jana na Meneja Mradi huo, Mhandisi Ephraim Tonya, wakati wa kutembelea na kukagua ujenzi wa vyoo bora shuleni vinavyojengwa na vijana waliopata mafunzo ya ujenzi kupitia mradi huo.

Mhandisi Tonya alisema mradi huo wa miaka mitatu unatekelezwa kwenye wilaya tatu za Mkoa wa Mbeya ambazo ni Chunya, Mbarali na Mbeya Vijijini na makadirio ya mradi huo ni kuwanufaisha vijana 135.

Alisema kupitia mradi huo vijana wamejengewa uwezo wa kuboresha afya kupitia ujenzi wa vyoo bora na matarajio ni kufanikisha jamii zisizo na vyoo bora wafikie kwenye hatua ya ujenzi wa vyoo vilivyokidhi vigezo.

"Mradi huu umewasaidia vijana kujikwamua na umaskini kwa sababu kupitia mafunzo hayo wamepata ujuzi wa Tehama, matumizi ya simu janja ili waweze kufuatilia shughuli zao za kila siku," alisema Mhandisi Tonya.

Alisema kwa sasa wapo katika mafunzo ya ufundi wa ujenzi wa vyoo kwenye shule na wamechagua kata tisa zenye shule kwa wilaya zote tatu wanazofanya nazo kazi na kwamba kila shule itajengewa choo kimoja ambacho kitakuwa na matundu ya wavulana na wasichana.

Alisema shirika limeamua kuisaidia jamii kujenga vyoo hivyo ambavyo vimekidhi vigezo vilivyotolewa na Wizara ya Afya kwa maana ya viwango, ukubwa, kundi la wenye ulemavu kama sehemu ya kuunga mkono ujenzi wa matumizi ya vyoo bora.

Alisema vijana waliofundishwa wakiwamo wanaume na wanawake ndio wanaojenga vyoo hivyo kama sehemu ya kuonyesha ujuzi wao na kujitangaza na kuisaidia jamii na kuzitaja kata zilizonufaika na mradi huo wilayani Chunya kuwa ni Sangambi, Chalangwa na Mbugani.

Mkuu wa Shirika la CRS Tanzania, Kellie Hynes, alipongeza jitihada zinazofanywa na serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi na wanaiunga mkono kwa kuanzisha miradi yenye lengo la kuisaidia jamii.

Alisema wataendelea kutoa misaada na fursa mbalimbali mkoani Mbeya katika kuwainua vijana ili kujikwamua na umaskini.





# Maoni yaanza kutolewa kanuni usafirishaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeanza kukusanya maoni kutoka kwa wadau wa usafirishaji wa nchi kavu, ili kusaidia kuboresha rasimu nane za kanuni zilizoandaliwa na wizara, ili kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya uchukuzi.

Akizungumza jana jijini hapa na wadau wa usafirishaji pamoja na Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini (Latra), Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Leonard Chamriho, aliwataka kutoa maoni yao yatakayosaidia kuondoa baadhi ya vikwazo vya usafiri wa ardhini.

Chamriho alisema hakuna sababu ya kuhofia kutoa maoni kuhusiana na kile wanachoona kinafaa katika uboreshaji wa kanuni hizo.

Alizitaja kanuni hizo kuwa ni kuwathibitisha madereva na usajili wa wafanyakazi na vyombo vya biashara, kuwathibitisha madereva na kuwasajili wafanyakazi wa treni, tozo, ukodishaji wa magari madogo na pikipiki, kushughulikia mapitio ya uamuzi ya mamlaka, magari ya abiria na magari ya mizigo.

Kwa mujibu wa Chamriho, kupitia kanuni hizo, wadau wanatakiwa kushiriki kikamilifu kutoa maoni yao kwa lengo la kupata kanuni ambazo ni bora na zitakazotekelezeka kwa urahisi.

Alisema mbali na wadau kujadili rasimu hiyo katika mkutano huo, pia wana nafasi ya kuwasilisha maoni yao kwa njia ya maandishi hadi Septemba 7, mwaka huu, ili kutoa nafasi ya hatua zingine za maandalizi kufanyika.

Hata hivyo, alisema elimu itaendelea kutolewa mara kwa mara kwa wadau wote wanaohusika na sekta hiyo ili kuzifahamu vyema kanuni hizo na kutoa maoni yao.

Mkurugenzi Mkuu wa Latra, Gerald Ngewe, alisema tayari sekta ya uchukuzi ina sera ambayo inatoa mwongozo na mwelekeo. Alisema rasimu hizo nane zitakazowasilishwa zitawezesha wadau kutoa maoni mbalimbali ili kuboresha sekta ya usafiri wa ardhini.

Ngewe alisema kumekuwa na adha inayojitokeza kwenye magari ya biashara baada ya madereva kuwaruhusu wafanyabiashara kuuza bidhaa zao

ndani ya vyombo vya usafiri jambo ambalo linasababisha usumbufu kwa wateja na kuongeza kuwa wanaomba serikali kushirikiana nao kutatua changamoto hizo.

## Wakosa nafasi kidato cha tano

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WANAFUNZI 187, waliomaliza kidato cha nne katika mwaka wa masomo 2018, wameshindwa kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano kutokana na masomo yao waliyofaulu kukosa muunganiko katika tahasusi walizochagua.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alipokuwa akitangaza matokeo ya wanafunzi waliochaguliwa katika awamu ya pili kujiunga na masomo ya kidato cha tano na vyuo vya ufundi vya kati.

Jafo alisema wanafunzi 1,861 walikosa nafasi ya kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika matokeo yaliyotangwaza awali Juni, mwaka huu.

"Katika awamu ya pili ambayo tunatangaza leo (jana) wanafunzi wavulana 1,861 waliokuwa wamebaki wakati tukitangaza matokeo Juni, kati yao 1,674 wamepangiwa shule na wengine 187 wamekosa nafasi kutokana na kukosa ufaulu mzuri katika tahasusi walizochagua," alisema Jafo.

Alifafanua kuwa wanafunzi hao 187 waliokosa nafasi kutokana wengi wao kufaulu katika masomo ambayo hayawezi kuweka muunganiko mzuri katika kupata tahasusi za masomo ya kidato cha tano.

"Unakuta kuna mtu kafaulu ana alama ya A katika somo la hesabu, lakini ana B ya Kiswahili, hivyo hakuna uwezekano wa kuwa na tahasusi iliyonyooka katika masomo yake aliyochagua kujiunga," alisema.

Aidha, alisema kwa wanafunzi 1,674 waliobahatika kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano, 178 wamepangiwa katika masomo ya sayansi na wengine 1,496 masomo ya sanaa na biashara.

Waziri Jafo, aliwashauri wanafunzi waliokosa kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano kuomba nafasi katika vyuo mbalimbali vya ufundi vya kati ambavyo vipo chini ya Nacte.

Jafo aliwataka wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano kuripoti katika shule zao kuanzia Septemba 2 hadi 16, mwaka huu na atakayeshindwa kufanya hivyo atakuwa amepoteza nafasi.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), anayeshughulikia afya, Dk. Dorothy Gwajima (aliye kaa), akimsikilia muuguzi Shija Makeja wa zahanati ya kijiji cha Chiboli wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wakati alipofanya ziara ya kikazi juzi. **PICHA: PAUL MABEJA**.

# Wapewa somo kutumia wasaidizi sheria

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

JAMII imeshauriwa kuwatumia watoa huduma wa msaada wa kisheria wanaopatikana katika kila wilaya pindi wanapokumbwa na changamoto za kudai haki yao.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkurungenzi wa Miradi kutoka Shirika la Kiraia la Msaada wa Kisheria (LSF), Scholastica Jullu, katika mkutano ulioyakutanisha mashirika 47 ya utoaji wa msaada wa kisheria nchini uliofanyika jijini hapa.

Alisema kutokana na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu masuala ya kisheria, shirika hilo limeweka watoa msaada wa kisheria kila wilaya nchini na wanatoa huduma hiyo bure.

Jullu alisema lengo la mkutano huo ni kujadili mafanikio na changamoto ambazo wanakutana nazo katika utoaji wa huduma za msaada wa kisheria.

Kwa mujibu wa Jullu, kwa miaka minne shirika hilo limetoa msaada wa ruzuku ya zaidi ya Sh. bilioni 19 kwa mashirika yasiyo ya kiserikali 47 kwa Tanzania Bara na Visiwani.

Alisema tangu mwaka 2017 wametoa ruzuku kwa mashirika mapya manane na ya zamani 39 kwa ajili ya kutoa misaada ya kisheria katika maeneo mbalimbali. Mradi huo ni wa miaka mitano na unatarajiwa kumalizika mwakani.

"Haya ni mashirika ambayo tunayapa ruzuku na wamekuwa wakifanya kazi kwa kutumia wasaidizi wa kisheria. Tupo kujadiliana changamoto ambazo wanakutana nazo katika kuwafikia wananchi, jinsi gani ya kuboresha utendaji kazi na kuangalia thamani ya fedha iliyotumika baada ya kuwapatia," alisema Jullu.

Naye Mwakilishi wa Shirika la Utoaji wa Huduma za Kisheria mkaoni Kilimanjaro (Kwieko), Peter Mashungia, alisema changamoto ambayo wamekuwa wakikutana nayo katika utoaji wa msaada wa kisheria ni ukatili wa kijinsia katika jamii.

Alisema familia nyingi zinazofanyiwa ukatili huo, zimekuwa zikificha kutoa ushahidi kutokana na kuwa undugu hivyo kumaliza kifamilia. Mashungia alisema makosa ya ukatili wa kijinsia ni suala ambalo wamekutana nalo mara nyingi na kinamama ndio waathirika wa tatizo hilo, hivyo bado wanajitahidi kuwaelimisha zaidi.

Naye Ofisa Habari wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Salima Mseta, alisema Watanzania wengi hawana uelewa wa mambo ya kisheria hali ambayo husababisha kukosa haki za msingi.

Mseta alisema uhitaji ni mkubwa kwa Watanzania katika mambo ya kisheria hali ambayo imekuwa ikisababisha wengi kukosa haki zao za msingi.



# Dk. Shein awahakikishia wajasiriamali sauti zao kusikika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuwa nia ya serikali ni kuhakikisha sauti za wajasiriamali zinasikika na zinafanyiwa kazi ili kufikia malengo waliyoyakusudia.

Akizungumza na uongozi wa Wizara ya Biashara na Viwanda wakati ilipowasilisha Mpango Kazi wa Julai 2018 hadi Juni 2019 sambamba na Mpango Kazi wa Utekelezaji kwa mwaka 2019/2020, alieleza kuwa matajiri walio wengi duniani walianza na ujasiriamali hivyo ni vyema wakapewa kipaumbele katika shughuli zao wanazozifanya.

Alieleza kuwa mbali ya matajiri wa duniani, hata Zanzibar matajiri wengi wameanza na ujasiriamali hivyo, si jambo la busara kuwabeza na badala yake ni vyema wakapewa kipaumbele na ushirikiano wa kutosha.

Alisema ipo haja ya kuwasaidia wajasiriamali ili na wao waweze kuwa wafanyabiashara wakubwa na kufikia malengo waliojiwekea jambo ambalo limeiibua serikali katika kuhakikisha inawatekelezea matakwa yao na kuwashirikisha kikamilifu.

Pamoja na hayo Rais Dk. Shein, alitumia fursa hiyo kutoa pongezi kwa uongozi wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa kuwasilisha vyema Mpango Kazi wao na kueleza kuwa utendaji wao pamoja na wafanyakazi wa wizara hiyo ndio uliofanya kupata mafanikio.

Aliutaka uongozi huo kuongeza kasi na kufanya kazi kwa bidii ili mafanikio zaidi yaendelee kupatikana katika kuimarisha sekta hiyo ambayo ina umuhimu katika kuimarisha uchumi na kukuza sekta za kijamii.

Alieleza matumaini ya kuimarika kwa zao la mwani ambalo lina aina nne na kueleza kuwa hatua hiyo itafanya kupata mafanikio mazuri ya zao hilo ikiwa ni pamoja na mchakato wa kujenga kiwanda, Chamanangwe Pemba.

Alisema Zanzibar ina historia kubwa ya kulima mazao mbalimbali yakiwamo ya viungo vya chakula kwa muda mrefu, hivyo ni vyema mazao hayo yakaimarishwa ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wakulima kuyalima vikiwamo viungo kama pilipili hoho.

Naye Mshauri wa Rais wa Zanzibar, Pemba, Dk. Maua Abeid Daftari, alitoa pongezi kwa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kwa kuendeleza zao la mchaichai kisiwani Pemba kwa kuwa wananchi wengi wamehamasika na kuomba wasaidiwe kuwekewa vinu karibu na sehemu wanazoishi.

Kwa upande wake Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, akiwasilisha muhtasari wa utekelezaji Mpango Kazi wa wizara hiyo, alisema katika kipindi cha mwaka 2018/2019, tani 218,911 za chakula ukiwamo mchele, sukari na unga wa ngano zilikuwapo kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani na kuifanya Zanzibar kuendelea kuwa na chakula cha kutosha cha aina hizo katika kipindi chote.

Alisema sensa ya viwanda iliyofanyika mwaka 2016 ilionyesha idadi ya viwanda imeongezeka na sukari imeongezeka kutoka tani 677 iliyozalishwa mwaka 2017 hadi tani 3,339 kwa mwaka 2018 sawa na ongezeko la asimilia 79.7 na uzalishaji wa unga wa ngano nao uliongezeka kutoka tani 25,196 mwaka 2017 hadi tani 26,963 mwaka 2018.

Balozi Amina alieleza kuwa katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Shirika la Biashara la Taifa limenunua karafuu tani 211.34 kwa jumla ya Sh. bilioni 2.9 na pia uzalishaji wa mafuta ya mimea ulifikia kilo 40,955.3 kwa jumla ya Sh. bilioni 1.5.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC), Maalim Kassim Suleiman (kulia), akizungumza wakati wa Mkutano wa Utekelezaji wa Bajeti na Mpango Kazi wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwezi Julai 2018 hadi Juni 2019, ukiongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani), uliofanyika ukumbi wa Ikulu Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Ashauri wataalamu kusomea fani zenye upungufu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameuagiza uongozi wa Wizara ya Afya Zanzibar kuendelea kuwashawishi wataalamu wake wa afya kusomea fani nyingine zenye upungufu wa watendaji ili kuziba mapengo yanayojitokeza katika utoaji wa huduma za afya.

Alisema lazima ifikie wakati hospitali za serikali ziwe na uwezo kamili wa kuwa na wataalamu wa kutosha badala ya kuendelea kutumia mfumo wa muda mrefu uliozoeleka wa kutegemea wataalamu wa nje.

Akifanya ziara fupi ya kukagua uwajibikaji kwa watendaji tofauti kwenye vitengo mbalimbali vinavyotoa huduma za afya kwa wananchi ndani ya Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja Balozi Iddi, alisema hatua hiyo ya ushawishi inaweza pia kusaidia kuziba mapengo ya wataalamu wanaostaafu kwenye vitengo vya fani hizo.

Alitoa mfano kitengo kinachohudumia wananchi wanaopatwa na ajali ambacho kinastahiki kuimarishwa zaidi kwa vifaa pamoja na wataalamu wazalendo waliobobea kwa vile ajali za vyombo vya moto hivi sasa vimeongezeka barabarani kutokana na harakati za kimaisha.

Alisema takwimu inaonyesha wazi kwamba wagonjwa wengi wanaopelekwa hospitali kwa ajili ya huduma za afya ni wale wanaopatwa na ajali za barabarani ambao wengi kati yao hulazimika kupelekwa nje ya Zanzibar baada ya wagonjwa mifupa kushindwa kuhudumiwa.

Alieleza kuwa lazima taasisi za umma zijitegemee kwa kuwa na wataalamu pamoja na vifaa vya kutosha ili kuepuka tatizo la kuwapeleka wagonjwa nje Zanzibar na kuacha kusubiri wataalamu wa misaada.

Naye Mkurugenzi wa Kitengo cha Maabara katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Dk. Msafari Marijani, alisema uwezo wa kutoa huduma kwa saa 24 kwenye kitengo hicho bado haujakamilika kutokana na uhaba wa wataalamu wa fani hiyo inayohitaji kufanyiwa kazi ya kuwahamasisha watendaji wake kuzidi kupata mafunzo zaidi ili kujaza pengo liliopo.

Dk. Marijan alisema kitengo hicho hutoa huduma kuanzia asubuhi hadi saa tatu za usiku kwa sasa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Ali Salum Ali, alisema, Wizara ya Afya kupitia uongozi wa hospitali hiyo ina mpango wa kuimarisha miundombinu mipya katika hospitali hiyo tegemezi kwa wananchi wengi kisiwani Unguja.

Dk. Ali alisema majengo mengi ya hospitali hiyo ni ya zamani ambayo yanahitaji kufanyiwa matengenezo.

Akizungumzia changamoto inayojitokeza ya hewa ya Oxygen kwenye hospitali hiyo, Dk. Ali, alisema, timu ya Wizara ya Afya hivi sasa iko jijini Dar es salaam kufanya mpango wa utafiti wa upatikanaji wa mfumo mwingine wa liquid oxygen badala ya ule uliozoeleka ambao hukumbwa na matatizo ya mara kwa mara.

# Watoto watakiwa kushirikishwa afya ya uzazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZAZI, walezi na walimu wametakiwa kushirikiana katika kuwaelimisha watoto afya ya uzazi ili waweze kujikinga mapema.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo kwa wahusika hao kuhusu ushirikishaji jamii katika kuboresha utoaji na upatikanaji wa elimu ya jinsia, afya ya uzazi na maadili kwa vijana, Mkurugenzi wa Idara ya Elimu Sekondari wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Asya Iddi, alisema watoto hasa wasichana wamekuwa wakipata vishawishi mbalimbali ambavyo vinaweza kuathiri mwelekeo wa afya zao.

Aliwataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao na kuvunja ukimya kwa kupunguza ukali na badala yake wawaelimishe ili wanapopata matatizo waweze kuwajulisha kwa haraka na kuwasaidia.

Pia aliwataka kuyatumia vizuri mafunzo watakayoyapata kwa kuwaelimisha na wenzao ili taaluma hiyo iweze kuwafikia na wengine kwa haraka na kuwasaidia watoto wao kuwa na afya bora.

Naye Ofisa Elimu Wilaya ya Magharibi A' Unguja, Ahmed Abdulmajid Shaaban, alisema elimu ya afya ya uzazi imekuwa ikizungumzwa kwa kipindi kirefu na kutokana na umuhimu wake pia Wizara ya Elimu imekuwa ikitoa vitabu kuhusu ya elimu ya stadi za maisha, huku taasisi mbalimbali zimekuwa zikijihusisha katika kuhakikisha athari wanazozipata watoto.

Alisema kumekuwapo na mambo mengine ambayo yanawakuta watoto kulingana na umri wao, hivyo amewaomba wazazi na walezi kuitumia vyema nafasi hiyo waliyoipata ili kuwasaidia watoto katika masuala ya afya zao.

# Takukuru yaitwa harufu ya ufisadi ujenzi kituo cha afya

**Restuta Damia,** BUKOBA

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Bukoba imeiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kufuatilia fedha iliyotumika katika ujenzi wa majengo manne ya Kituo cha Afya cha Zamzam kilichopo Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera.

Maagizo hayo yalitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Deodatudus Kinawilo, kwa kushirikiana na viongozi wa Baraza la Amani na Maridhiano wilayani humo katika ukaguzi wa miradi mitano yenye thamani ya shilingi bilioni 1.7 ya miundombinu ya afya inayoendelea kujengwa katika vituo vinne na hospitali moja ya wilaya hiyo.

Kinawilo alisema fedha zinazotolewa na serikali zinapelekwa kwa wananchi ili kufanya shughuli za maendeleo na kuwanufaisha kwa kuwapatia huduma.

Alisema Juni mwaka jana, serikali ilitoa Sh. milioni 400 kwa kituo hicho sawa na pesa ilitolewa kwenye kituo cha Kata Maruku, Kituo cha Kata Katoro na Kata Kishanje.

Vituo hivyo vitatu vimefikia hatua ya kuridhisha katika kukamilisha ujenzi na kuwa na majengo mazuri yanayokidhi hadhi.

"Vituo vingine vimepokea pesa sawa na hapa kituo cha Katoro Sh. milioni 500. Kituo Majengo Matano cha Maruku Sh. milioni 400, Kishanje Sh. milioni 400 majengo yanaendelea na fedha bado ipo...iweje Zamzam majengo machache pesa imekwisha na mnadai kuongezewa Sh. milioni 30?" Alihoji Kinawilo.

Aliongeza majengo yaliyopo katika kituo hicho ni jengo la mama na mtoto ambalo limefanyiwa ukarabati, jengo la maabara, jengo la kufulia ambapo katika vituo vingine umefanyika ujenzi wa jengo la mama na mtoto, chumba cha kuhifadhia maiti, sehemu ya kufulia, maabara na jengo la upasuaji.

"Iweje katika kituo hiki itumike pesa kwa majengo manne pekee na pesa isitoshe kukamilisha wakati vituo vingine vikipatiwa pesa sawa na hiki na wamefanya vizuri na kujenga majengo matano na hawakuomba pesa nyingine kuongezewa?" Alihoji zaidi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa hiyo, Richard Mihayo, alisema kazi ilibakia katika majengo hayo ni uwekaji mifumo ya umeme, maji, milango na baadhi ya sehemu za kunawia mikono.



Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana wa Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalang'anya (kulia), akiwagawia taulo za kike baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari za jijini humo jana, zilizotolewa msaada na Shirika la Umati, katika hafla iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Chinangali. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

# Mwarobaini ukatili jinsia

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZWA kuwa ili kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia kwa jamii kupitia maeneo yanayowazunguka, inatakiwa kuundwa kwa kamati za Mtakuwwa kuanzia ngazi za chini hadi ngazi za juu.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Programu Mwandamizi kutoka TGNP Mtandao, Deograthias Temba, alipokuwa akizungumza wakazi wa Mwananyamala na wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Mchangani, iliyopo Mwananyamala jijini Dar es Salaam.

Katika mkutano huo uliowakutanisha washiriki wa semina za jinsia na maendeleo (GDSS), ambapo kuna wanafunzi wa Shule ya Mchangani baadhi yao wanashiriki katika klabu za shule ambazo zinazungumzia kupinga ukatili wa kijinsia.

Temba alisema kuwapo kwa matukio ya ukatili wa kijinsia kwa jamii, alisema kamati za Mtakuwwa kuanzia ngazi ya chini hadi juu, itasaidia kupunguza matukio hayo.

"Mtakuwwa ni Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia dhidi ya wanawake na watoto na ulianza kutekelezwa toka mwaka 2016/2017 na utaendelea mpaka mwaka 2022," alisema.

Aliongeza kuwa mpango huo umeletwa na serikali ili kusaidia kuondoa matukio hayo kwa jamii.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Mchangani, ambaye ni mlezi wa kitovu cha jinsia, Goodlack Misago, alisema ukatili unaanzia nyumbani na inatakiwa ukemewe.

Alisema ili kufikia malengo ya kuuondoa ukatili, kwanza wazazi wavunje ukimya, wawe karibu na watoto, wasifiche siri pale mtoto anapofanyiwa ukatili, wajenge urafiki na watoto pia utaratibu wa kuwalaza watoto na watu wasio wa familia wauache kwa kuwa kufanya hivyo ni kichocheo cha uovu, kwa kuwa matukio mengi hufanywa na baadhi ya watu wa karibu, hivyo ni vigumu kuwachukulia hatua.

# Ukosefu wa barabara wakwamisha biashara

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

UKOSEFU wa barabara katika Shehia ya Mgelema Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba, inasababisha kuzorotesha shughuli za kibiashara na kupelekea kudumaa kwa uchumi wa shehia hiyo.

Barabara hiyo yenye urefu wa kilomita sita kutoka barabara kuu ya Chake-Mkoni hadi kufikia vijiji vya Mgelema, ambapo imejengwa kwa kiwango kilomita tatu (3) tu kutoka Kipapo.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi kijijini kwao Mgelema, wananchi wa shehia hiyo wamesema, hata gari za abiria zinashindwa kufika kutokana na barabara hiyo kuchimbuka huku ikiwa na milima.

Walisema wanashindwa kufanya shughuli zao za kijamii ikiwamo za kibiashara kutokana na ubovu wa barabara hiyo, jambo ambalo linaendeleza umaskini kwa wakaazi wa vijiji vya shehia hiyo.

Ali Juma Nassor alisema ubovu wa barabara hiyo unasababisha kutumia gharama kubwa kwa kitu kidogo, kutokana na wenye magari kukataa kufika katika vijiji hivyo.

"Ukiwa na biashara zako inabidi ukodi gari na hiyo gharama yake basi bora bidhaa zako uwe unakula mwenye maana hakuna faida tunayoipata," alisema.

Bimkubwa Omar Khatib, alisema wajawazito ndio wanaopata shida wakati wa kujifungua, kwani hulazimika kubebwa au kuingizwa ndani ya gunia mpaka Kipapo kwenye barabara kuu, jambo ambalo ni kuhatarisha maisha ya kinamama na watoto.

"Hapa tunatumia Hospitali ya Chakechake kujifungulia, lakini tunapata shida maana hatuna barabara na hiki kipindi cha mvua ndio kabisa hata umpe kiasi gani cha fedha dereva hakufuati," alisema.

Sheha wa shehia hiyo, Omar Iddi Zaina, alisema kutokana na miundombinu ya barabara yao ilivyo, wanashindwa kufanya shughuli zao za kila siku.

"Mimi nina zaidi ya magunia 100 ya mihogo kwenye shamba langu, lakini nashindwa kwenda mjini kuuza, maana ni hasara kubwa kukodi gari... wenye gari wanasema hawataki kuharibu gari zao."

Ofisa Mdhamini Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Hamad Ahmad Baucha, alisema wana mpango wa kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ambapo serikali kupitia wizara imeshaagiza vifaa vya ujenzi.

# China yapeleka vikosi vipya Hong Kong

**HONG KONG, China**

CHINA imepeleka vikosi vipya katika kituo chake cha kijeshi Hong Kong.

Hong Kong kwa sasa inakabiliwa na mgogoro wa kisiasa uliyokuwa mbaya zaidi tangu iliporejea katika utawala wa China mwaka 1997.

Shirika la Habari la Serikali, Xinhua, lilisema kupelekwa kwa vikosi hivyo ni utaratibu wa kawaida wa kubadilisha wanajeshi na vifaa katika kambi ya jeshi la ukombozi wa wananchi kwenye jiji hilo ambalo ni kituo kikuu cha kibiashara.

Televisheni ya taifa hilo ilionyesha picha za video za magari yasiyopitisha risasi na malori ya kubebea wanajeshi yakiingia katika kambi hiyo baada ya kuvuka mpaka wa mji jirani wa Shenzhen.

Hong Kong imekumbwa na mvutano na vurugu za maandamano kwa takriban miezi mitatu ambayo yalianza kama kupinga muswada wenye utata wa kuwarudisha wahalifu China, lakini tangu wakati huo yamebadilika na kushinikiza kuwapo kwa demokrasia zaidi na uchunguzi wa kujitegemea kuangalia madai ya ukatili wa polisi.

Jeshi la Polisi la Jiji hilo, juzi lilikataa kutoa kibali kwa kikundi cha wanaharakati cha Civil Human Rights Front kufanya maandamano mengine, likitoa sababu ya kuhofia kutokea vurugu kati ya polisi na waandamanaji kama ilivyokuwa wakati wa maandamano yaliyotokea mwishoni mwa wiki.

Polisi walitumia mabomu ya kutoa machozi na maji maalumu dhidi ya waandamanaji ambao walijitenga na kundi kubwa lililokuwa linaandamana kwa amani.

Baadhi ya waandamanaji hao waliwatupia polisi matofali, waliwashambulia kwa fimbo, nondo na kutupa sabuni mitaani ili kufanya polisi wasiweze kupita katika barabara hizo kutokana na utelezi.

Maandamano yaliyopangwa kufanyika mwishoni mwa wiki yatakuwa ni kilele cha miaka mitano tangu Beijing kukataa Hong Kong kuchagua viongozi wake kidemokrasia.

Wanaharakati wanaounga mkono demokrasia nchini humo wanahofia kuwa China inaendelea kukandamiza uhuru ambao wamekuwa wakinufaika nao tangu mwaka 1997, wakati Hong Kong ilipokabidhiwa kutoka katika utawala wa Uingereza. **VOA**

# Wabunge wapandisha mori bunge kusitishwa

**LONDON, Uingereza**

SIKU moja baada ya Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, kusitisha bunge, kumesababisha hasira kutoka kwa wabunge wa upinzani wanaopinga kuidhinishwa Brexit bila mpangilio.

Hatua hiyo ilisababisha kuzuka kwa maandamano nchini humo, kesi iliowasilishwa dhidi ya hatua hiyo na waraka uliosainiwa na watu zaidi ya milioni moja wakipinga.

Hata hivyo, Serikali ya Uingereza imesema kusitishwa kwa vikao vya bunge kwa muda wa wiki tano kuanzia Septemba hadi Oktoba kutaruhusu muda wa kutosha kujadili Brexit,

lakini wakosoaji wanasema ni hatua isiyo ya kidemokrasia kuzuia wabunge kupinga Brexit bila ya mpangilio.

Waziri Michael Gove alisema kusitishwa huko kwa bunge kulikoidhinishwa na Malkia siku ya Jumatano siyo hatua ya kisiasa kuzuia upinzani kwa hatua ya Uingereza kujitoa Brexit.

Alisema kwamba kutakuwa na muda mwingi wa kujadili Brexit kabla ya muda uliooroddheshwa wa kuondoka Oktoba 31.

Jana Johnson alisema hotuba ya Malkia itatolewa baada ya kusitishwa kwa vikao vya bunge, ifikapo Oktoba 14.

Kiongozi wa bunge, Jacob Rees-Mogg, aliyekuwa katika mkutano na Malkia alisema vikao hivi vya bunge vilikuwa virefu kuwahi kushuhudia katika takriban miaka 400, kwa hivyo ni sawa kusitishwa na kuanza kikao kipya.

Kiongozi wa chama cha Leba, Jeremy Corbyn, alitaja hatua hiyo kama pigo na ukandamizaji wa demokrasia.

Mwanaharakati anayepinga Brexit, Gina Miller - aliyewahi kushinda kesi dhidi ya mawaziri kuhusu kipengele cha 'Article 50' aliwasilisha ombi la kuikagua sheria dhidi ya uamuzi uliotolewa na Johnson.

Johnson alisema anataka kuondoka katika Umoja wa Ulaya mwishoni mwa Oktoba, huku kukiwapo na mpangilio, lakini yuko radhi kuondoka pasi kuwapo mapangilio huo kuliko kuikosa tarehe ya mwisho.

Mwanzoni mwa wiki waandamanaji walikusanyika Westminster wakipiga kelele wakisema: "Sitisha mapinduzi" huku wakibeba mabango ya kupinga kujitoa katika Umoja wa Ulaya.

Maandamano hayo yaliandaliwa saa chache yalianza nje ya makao ya bunge kabla ya kusambaa kuelekea Downing Street.

Wakati huo huo, muswada wa kielektroniki katika mtandao wa serikali unaotaka bunge lisisitishwe ulifanikiwa kupokea saini za watu zaidi ya milioni moja katika muda wa siku moja.

Watu kadhaa akiwamo aliyekuwa Waziri Mkuu John Major, waliwahi kutishia katika siku za nyuma kwenda mahakamani kusitisha hatua ya Johnson iwapo atalisitisha bunge ili kuwasilisha Brexit bila ya kuwapo kwa mpangilio. ***BBC***



Wananchi wa Uingereza wakiandamana kupinga nchi yao kujitoa katika Umoja wa Ulaya na bendera za muungano huo. **PICHA: REUTERS**

# Warundi waendelea kutoroka, wakimbilia DRC

**BUJUMBURA, Burundi**

SIKU za hivi karibuni, kambi za muda za wakimbizi katika maeneo ya Sange na Kavimvira, Mashariki mwa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) zimeendelea kupokea wakimbizi kutoka Burundi.

Imeelezwa kuwa watu wapatao 100 wanaripotiwa kuvuka mpaka kwa siku na kuoroddheshwa katika kambi hizo.

Kwa mujibu wa Gazeti la Burundi la Iwacu lilieleza kuwa hali hiyo ilianza wiki mbili zilizopita, wakati wanaendelea kusubiri msaada, wakimbizi hao wanaishi katika mazingira mabaya, baadhi wanaonekana mitaani wakiomba.

Katika kambi ya muda ya wakimbizi ya Sange, iliyoko kilomita 15 kutoka Mto Rusizi, kwenye mpaka wa Burundi na DRC, watu wengi wamekuwa wakiyakimbia makazi yao upande wa Wilaya ya Buganda katika mkoa wa Cibitoke, Magharibi mwa Burundi, wakielekea katika kambi hiyo, inayopatikana katika Jimbo la Uvira.

Kwa mujibu wa gazeti hilo, ili kupata chakula cha kutosha, wakimbizi hao ambao wengi wao ni watu wazima na watoto wamekuwa wakiranda randa mitaani wakiomba omba kwa kusubiri misaada ya kibinadamu.

Kwa mujibu wa mkazi mmoja wa Sange, akinukuliwa na gazeti hilo, watoto huingia nyumba kwa nyumba wakiomba msaada.

Wakati huo huo, serikali ya Tanzania hivi karibuni ilitangaza kwamba itachukuwa hatua ya kuwarudisha makwao wakimbizi wa Burundi waliokimbilia nchini Tanzania.

Hayo yanajiri wakati Serikali ya Rwanda imetangaza kuwapa bima ya afya wakimbizi kutoka Burundi waliokimbia nchini humo tangu mwaka 2015 kutokana na mzozo wa kisiasa na kiusalama nchini mwao.

Tangu mwaka 2017 Rwanda inatoa hifadhi kwa wakimbizi 172,000, huku asilimia 50 wakitokea nchini Burundi na wamepewa hifadhi katika kambi ya Mahama. ***RFI***

# Wanafunzi 300 Mwanza wapata ujauzito 2018

**Na Rose Jacob, MWANZA**

WANAFUNZI 300 wa shule za msingi na Sekondari mkoani Mwanza, walipata ujauzito mwaka jana huku kesi nyingi zikionekana kuishia vituo vya polisi na ofisi za kata.

Idadi hiyo imebainishwa na ripoti iliyotolewa na sekta ya elimu mkoani Mwanza kuwa baadhi ya wanafunzi wanaoishi shule za bweni, wamekuwa na tabia ya kutoroka usiku na kuwafuata wanaume uraiani huku baadhi yao wakikutwa na simu za mkononi wanazotumia katika mawasiliano ya mapenzi. Akiwasilisha ripoti hiyo juzi katika kikao cha semina iliyohusisha Kamati ya Mkoa ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto na Shirika la Kutetea Haki za Wanawake na Watoto (Kivulini), Ofisa Elimu Taaluma Mkoa wa Mwanza, Jovitha Mwombeki, alisema ripoti hiyo inahusu halmashauri nane za mkoa huo.

Kwa mujibu wa Mwombeki, kwa shule za msingi, wanafunzi waliopata ujauzito wakiwa shuleni ni 49. Alitaja halmashauri na idadi ya waliopata ujauzito kwenye mabano kuwa ni Ilemela (mbili), Kwimba (11), Magu (26), Jiji Mwanza (tatu), Sengerema (tisa), Ukerewe (tisa).

Mwombeki alisema upande wa sekondari, mimba zilikuwa 251 huku Misungwi iliwa kinara kwa matukio 98. Halmashauri zingine na idadi katika mabano ni Buchosa (23), Ilemela (mbili), Kwimba (42), Magu (17), Jiji Mwanza (36), Ukerewe (32) huku Sengerema haikupata tukio la mimba.

"Katika kukabiliana na suala hili, hatua mbalimbali zimechukuliwa kwa walioshiriki. Mfano Buchosa kuna matukio 23 ya msingi na sekondari na kesi zote ziko polisi. Pia Ilemela kuna mimba tano na kesi zote ziko polisi. "Kwimba kuna mimba 53 na kesi 37 ziko polisi, 10 mahakamani na sita ziko kwa watendaji wa kata wakiendelea kuchunguza na kuwatafuta watuhumiwa. Upande wa Magu kuna mimba 43 na zote ziko kwa watendaji wa kata. Misungwi kesi 54 ziko polisi, 37 mahakamani na tano zimetolewa uamuzi," alisema.

Mwombeki alisema katika kufuatilia suala hilo, wamebaini baadhi wa wasichana wanaoishi katika shule za bweni wamekuwa wakitoroka usiku na kwenda kutafuta wanaume uraiani na ripoti iliyopo kuanzia Januari hadi sasa inaonyesha wako wanafunzi saba waliokamatwa wakitoroka usiku bwenini na wawili walikutwa na simu zinazotumika kwa mapenzi.

Bila kutaja majina ya wanafunzi na shule husika, Mwombeki alisema baadhi ya matukio yanayofanyika shuleni yanasababisha kushuka kwa ufaulu kwa shule za sekondari ingawa kwa shule za msingi ufaulu unapanda.

Alitaja sababu hizo ni utoro, wanafunzi kujihusisha na shughuli za uchumi zikiwamo uvuvi, kilimo, kuchunga mifugo na biashara ndogondogo hasa Wilaya ya Ukerewe, Buichosa na Sengerema .

Madhara mengine, alisema wanafunzi wanaojihusisha na ngono kukosa umakini darasani, baadhi ya wanafunzi kuwa na maadili mabaya, umbali wa shule na makazi yao na kukosa lishe shuleni kitendo kinachosababisha nyakati za mchana watoto kutoroka na wengine kusinzia darasani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kivulini, Yassin Ally, aliiomba serikali kupunguza takwimu za watoto wanaopata ujauzito huku akilitaka Jeshi la Polisi kujitathmini hasa upande wa upelelezi kesi za mimba.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi (wa pili kushoto), wakizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha SACIDS Foundation for One Health chenye makao yake mkoani Morogoro, Prof. Mark Rweyemamu (wa pili kulia) na Kiongozi wa Kituo hicho, Prof. Gerlad Masinzo katika Mkutano wa Saba wa TICAD, unaoendelea kwenye Hoteli ya Pacifico Yokohama nchini Japan jana. **PICHA: OWM**

# Sababu Rufiji, Kibiti kukosa wawekezaji muda mrefu

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema wilaya za Rufiji na Kibiti kwa muda mrefu hazikuchangamkiwa na wawekezaji kwa sababu ya changamoto mbalimbali ikiwamo nishati ya umeme.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, aliyasema hayo juzi mkoani humo wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi kwenye kiwanda cha kampuni ya Huatang cha kuchakata betri za magari na pikipiki zilizokwisha muda wake.

Baada ya kuchakata betri zilizokwisha muda wake kiwanda hicho kitakuwa kinazalisha 'lead engot' ambayo hutumika kama malighafi ya kutengeneza betri mpya.

Akizungumza kwenye shughuli hiyo iliyofanyika kijiji cha Nyamwage, wilayani Rufiji, Ndikilo alisema miongoni mwa changamoto ya wilaya hizo zilikuwa ni nishati, na kwamba umeme wa awali unatoka Mbagala.

"Ujenzi wa bwawa la Nyerere utawezesha wilaya hizi kupata zaidi ya megawati 2115 na kituo cha kupoozea umeme kitakuwa Kibiti," alisema.

Ndikilo alimpongeza mwekezaji huyo wa kiwanda hicho kwa kuamua kuchagua kuwekeza Wilaya ya Rufiji ambayo ni miongoni mwa ambazo baadaye zitakuwa na viwanda vingi kutokana na kuwa na ardhi ya kutosha.

Alisema ofisi yake ina mawasiliano na moja ya nchi za Uarabuni na kuwa moja ya nchi hizo inataka kuja kufanya uwekezaji wa kujenga kiwanda cha kuzalisha sukari na mashamba ya miwa na zipo hekari 20 wilayani humo.

"Ukizungumzia kiwanda cha miwa tunazungumzia ajira zaidi ya 4,000. Kutoka bwawa la Nyerere hadi Geta kuna zaidi ya hekta 150,000 za ardhi zinazofaa kilimo cha umwagiliaji," alisema.

Alisema mkoa hauwezi kuruhusu watu wachache waende kuharibu maeneo hayo, na kuwataka wakulima na wafugaji kila mmoja kuheshimu na kufuata sheria.

Alisema ana taarifa baadhi ya wananchi wa maeneo hayo wanataka kuuza maeneo kwa mabilioni ya shilingi kwa wawekezaji na kuwataka waache.

"Yapo maeneo yatatengwa na halmashauri, yapo ambayo serikali ya kijiji tumewapa maelekezo wayatenge kwa ajili ya viwanda, pia wananchi kwa kushirikiana na halmashauri muyatenge maeneo kwa ajili ya uwekezaji, tatizo ninaloambiwa tunataka kuyauza kwa mabilioni ya shilingi kitu ambacho hakiwezekani mtakimbiza wawekezaji," alisema.

Ndikilo alikipongeza Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa kuwaongoza wawekezaji na hatimaye wameanzisha kiwanda hicho wilayani hapo.

Meneja wa TIC Kanda ya Mashariki, Venance Mashiba, alisema usajili wa mradi huo ulifanyika Novemba mwaka 2017 na una gharimu kiasi cha dola za Marekani zaidi ya 600,000.

Alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Machi mwakani na kwamba utaleta manufaa kwa nchi.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Ding Xian alisema wameanzisha mradi huo kuitikia wito wa Rais John Magufuli na Balozi wa China nchini, kuhusu kupeleka nchi kwenye uchumi wa kati wa viwanda.

Xian ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Biashara China-Afrika, alisema mradi huo utaleta mabadiliko chanya kwa wananchi wa kijiji cha Nyamwange, Rufiji kwa kutoa ajira na kukuza uchumi wa nchi.

# Wadau wa nondo wanolewa kuhusu ubora

**Na Joseph Mwendapole**

WADAU wa uzalishaji, uagizaji, usambazaji na uuzaji wa nondo nchini wamepatiwa elimu kuhusu taratibu na mifumo ya ukaguzi wa bidhaa hizo nje ya nchi kabla ya kuingizwa nchini ili kuhakikisha zinakidhi viwango.

Akizungumza wakati akifungua semina kwa wadau hao jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Yusuf Ngenya, alisema wadau hao wataelimishwa utaratibu za uthibitishaji ubora wa bidhaa za nondo, matakwa ya viwango na taratibu za kupata huduma za shirika kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

Semina hiyo kwa wadau imefanyika siku chache baada maofisa wa shirika hilo kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika maduka mbalimbali ya kuuza nondo na kubaini kuwapo kwa baadhi ya nondo zenye dosari mbalimbali za ubora wa viwango hususan kwenye urefu na upana.

Dk. Ngenya alisema nondo ni bidhaa muhimu kwa taifa hasa kipindi hiki ambacho taifa lipo kwenye mkakati wa ujenzi viwanda.

"Tumeona ni muhimu kukaa na wadau wote wa nondo na kukumbushana umuhimu wa kuzalisha, kuagiza, kusambaza na kuuza nondo zenye viwango," alisema Dk. Ngenya.

Mkurugenzi huyo alikiri kwamba kuna kasoro ndogo ndogo wamezibaini kwenye uzalishaji wa nondo na kwamba hiyo ni moja ya sababu za kuandaa semina hiyo.

Hata hivyo, alisema semina kama hizo zinatolewa kwa wazalishaji wa bidhaa mbalimbali kwa ajili ya kukumbushana masuala ya viwango.

Alitoa wito kwa Watanzania kutonunua nondo bila kujua urefu na upana wake ni kiasi gani na kwamba wanatambua kuwa siyo rahisi kwa mnunuzi kujua viwango vya nondo kwa macho, ndiyo maana shirika hilo linaweka msisitizo kwa wazalishaji, waagizaji, wasambazaji na wauzaji ili kuhakikisha wanazalisha nondo zenye viwango.

Pia alisema kwa kuzingatia kifungu cha 36 cha Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009, serikali ilipitisha kanuni za udhibiti wa shehena kupitia notisi ya Serikali Na. 405 ya Desemba 2009.

Kwa mujibu wa Dk. Ngenya, kanuni hizo ziliipa TBS mamlaka ya kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingia nchini kabla ya kusambazwa kwenye soko la ndani.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI), Leodgar Tenga, aliipongeza TBS kwa kuandaa semina hiyo hasa kwa kuzingatia kwamba viwango ni jambo la muhimu.

"Ni muhimu kwa wazalishaji wote kuhakikisha viwango vinaheshimika, ubora wa nondo zinazozalishwa nchini na zinazotoka nje ni muhimu sana, hivyo wadau wote lazima wazingatie viwango," alisema.

0000

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

## NAFASI ZA KAZI

Anahitajika - Mhasibu na sales Lady
Sifa – Awe Mwanamke
Elimu – Diploma

Ofisi yetu ipo Posta – Dar es Salaam
Kwa Mawasiliano :- 0715 – 885 533


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ONESMO IGNATIO WILSON,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Boxer, yenye Namba MC649CDC, chasis No.81782KNV, Engine No. DUZWJH66484 . Kadi ilibiwa na aliripoti kituo cha polisi cha Bukoba tarehe 26/08/2019 na kupewa RB. No. **KAG/BUK/RB/244530/2019.**

Kwa yeyote atakayeiona aipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye. Au awasiliane naye. **No: 0768848168.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA
KAGERA LILILOPO BUKOBA
RUFAA NA: 31/2019**

**MUSTAPHA ISSA ............................MDAI**
**DHIDI YA**
**ABDU COSTA ..................................MDAIWA**

KWA: ABDU COSTA
(POPOTE PALE MLIPO)

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Rufaa Na. 31/2019 imepangwa kutajwa tarehe 30.09.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 23.08.2019


MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MUSSA MOHAMED NDYESHOBORA .** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya NISSAN X-TRAIL, yenye Namba **T176CJL. chasis No: NT30003881, Model QR20(DE)1998** . Kadi ilipotea kipindi anahama kutoka Pwani kwenda Kemondo Bukoba, na aliripoti kituo cha polisi cha Bukoba tarehe 6/05/2019 na kupewa No. KAG/BUK/RB/246527/2019.

Kwa yeyote atakayeiona aipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye. Au awasiliane naye. **No: 0767301160**

## KUPOTEA KWA VYETI



**Cyprian Aloyce Rajabu** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0121-0009** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1991 katika shule ya Sekondari St. James Seminary, Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S0134-0510** kilichotolwa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1994 katika shule ya Sekondari Moshi . yeyote atakayeviona vyeti hivyo atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi taarifa: 7947/07

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**WAZIRI HUSSEIN NDALO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NO MC812AEE ENGINE NO LC6PCJK21 CHASSES S NO 0007844

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**ARU/ARU/RB/250584/2019.**

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**ADELHA JULIUS LIKALAGALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MITSUBISH FUSO yenye namba za usajili T 821 AFU, Chassis Na. FK417J543319, Engine Na.6DI6656168.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: MOR/IFA/RB/135797/2019.

## KUPOTEA KWA CHETI



**Wambura George Mirambo** anatangaza kupotea kwa kwa Result slip iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa, cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1662/0074** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Mkono.
Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**MAR/MUS/RB/166002/2019**

115396202

## VYETI VIMEPOTEA




**Steven Kamoga** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo; cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.3090/0418** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari Manzese na cheti cha darasa la saba kilichotolewa na shule ya msingi Kawawa mwaka 2008.

Yeyote atakayeiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: URP/RB/1720/18**

215395302

## KUPOTEA KWA CHETI



**Zakayo Nade Raphael** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha UALIMU chenye index namba E522/340 kilichotolewa na chuo cha Kinampanda mwaka 2004.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**MAN/HAN/RB/247625/2019**

115395502


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie 0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# RONALDO
## AIPAISHA JUVE MITANDAO YA KIJAMII

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus wameipita Manchester United kama timu ya tatu maarufu ya mpira wa miguu kwenye vyombo vya habari vya kijamii duniani, baada ya kuona ongezeko la wafuasi milioni 20 baada ya ujio wa Cristiano Ronaldo.

Mchezaji huyo raia wa Ureno alijiunga na Juve kipindi cha majira ya joto mwaka 2018 na kuongeza idadi hiyo na kuizidi kete klabu ya zamani wa Ronaldo, United.

Juve ilikuwa na ongezeko la wafuasi milioni 10, lakini baada ya ujio wa Ronaldo ukafanya ongezeko hilo kwa kasi.

Miamba wenzao hao wa Ulaya kwa sasa wana wafuasi milioni 77.6.

Real Madrid bado ipo kileleni kwa kuwa na wafuasi wengi zaidi duniani, na walinufaika na uwepo wa Ronaldo ambaye alikaa kwenye klabu hiyo kwa muda mrefu.

Ronaldo yeye ndiye kinara duniani kwa kuwa mwanamichezo mwenye wafuasi wengi zaidi kwenye mitandao ya kijamii akiwa na wafuasi milioni 131


# BAYERN KUMPA MKATABA MPYA LEWANDOWSKI

**MUNICH, Ujerumani**

MKATABA mpya unanukia kwa mshambuliaji wa kimataifa wa Poland, Robert Lewandowski, ambao wana matumaini atawasaidia kwenye mbio za ubingwa wa pili mfululizo wa Ligi akiwa na Bayern Munich wakati mabingwa hao wakiwavaa Mainz 05 Jumamosi.

Baravia hao wamefanya usajili wa nguvu kwa wiki za hivi karibuni, wakimsajili mshindi wa pili wa kombe la Dunia akiwa na Croatia, Ivan Perisic, nyota wa Brazil Philippe Coutinho na chipukizi wa Ufaransa, Mickael Cuisance.

Lakini Lewandowski mwenye umri wa miaka 31 ambaye amekuwa hapo Bayern tangu mwaka 2014, ambaye amefunga mabao yote matano kwenye mechi zao mbili za ufunguzi wa Ligi Kuu, akifunga mawili katika sare ya 2-2 dhidi ya Hertha Berlin na pia alifunga mabao matatu 'hat-trick' dhidi ya Schalke 04 wiki iliyopita.



Huku mkataba wake ukitarajia kumalizika mwaka 2021, mshambuliaji huyo amedokeza kwamba anatarajia kusaini mkataba mpya.

"Kuna mambo mengi katika kuongeza mkataba," alisema akiliambia gazeti la Sport Bild wiki hii.

"Nipo kwenye hatua za kukamilisha taratibu za kusaini mkataba mpya. Najisikia vizuri hapa Munich, klabu ina malengo mengi kwa upande wangu na hata mimi mwenyewe. Kushinda mataji, likiwemo la ligi ya mabingwa Ulaya."

Lewandowski tayari amekuwa mchezaji muhimu zaidi wa nje katika historia ya Ligi Kuu ya Ujerumani, akifunga mabao 207 kwenye Bundesliga katika mechi 292 alizoichezea Borussia Dortmund na Bayern.

## LAMPARD: CHELSEA ITAKUMBWA NA CHANGAMOTO UEFA

**LONDON, England**

CHELSEA inakabiliwa na 'changamoto kubwa' kuchangia mafanikio ya soka la Uingereza kwenye ligi ya mabingwa Ulaya msimu huu kwa sababu ya kufungiwa kufanya usajili wa wachezaji, kwa mujibu wa kocha wake, Frank Lampard.

Msimu uliopita ligi ya mabingwa Ulaya na ile ya europa ilitawaliwa na timu za Uingereza kwa kucheza fainali zote mbili, lakini Lampard anaona kwake itakuwa ngumu kung'ara kwenye mashindano hayo msimu huu.


Chelsea imerudi kwenye ligi ya mabingwa Ulaya baada ya kuwa na mafanikio msimu uliopita kwa kutwaa taji la ligi ya Europa, na itaungana na mabingwa Manchester City, Liverpool na Tottenham.

Lampard alisema: "Nafikiri Ligi Kuu ya England iko imara na hilo ni wazi kwamba unapokuwa na timu mbili kwenye fainali.

"Manchester City kwa uhakika kabisa ni timu kubwa duniani na kwa ligi yetu inamaana kwamba tuna timu imara na zenye vikosi bora kabisa.

"Uingereza kwa sasa ipo imara. Tuna matumaini timu za Uingereza zitaendelea kutawala, lakini kwa upande wa Chelsea kuna tatizo kidogo.

"Tuna furaha kufanya hivyo. Itakuwa changamoto kubwa zaidi kwetu. Tunajua kwamba changamoto ya kufungiwa ni ngumu kwetu na hatuna cha kufanya, maana usajili tumeshindwa kufanya.



"Hivyo, tunaweza tusiwe imara zaidi kwenye ligi ya mabingwa, maana changamoto ni kubwa zaidi kwa upande wetu."

HABARI MICHEZO

# REAL MADRID

## KUMBADILISHA NAVAS NA AREOLA WA PSG




**MADRID, Hispania**

REAL Madrid ipo kwenye mazungumzo ya kumpeleka golikipa, Keylor Navas kwenda Paris Saint-Germain kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili la Ulaya Septemba 2, kwa mujibu wa ESPN.

Miamba hao wa La Liga awali walikuwa wanataka kiasi cha euro milioni 20 ili kumwachia mchezaji huyo wa kimataifa wa Costa Rica, lakini kwa mujibu wa ESPN dili hilo litamhusisha golikipa wa PSG, Alphonse Areola kwenda Madrid.

Ilikuwa ni wiki iliyopita wakati kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane, aliposema majaliwa ya Navas yalikuwa Bernabeu licha ya Thibaut Courtois kuwa chaguo la kwanza.

"(Navas) ni mchezaji wa Real Madrid, hilo ni muhimu, mara zote amekuwa hapa na ataendelea kuwa hapa," alisema Zidane katika mkutano wake na waandishi wa habari wiki iliyopita.

"Sifikirii kuhusu kuondoka, najua anachangia mengi na ataleta ushindani. "Anasema kama anaharaka ya kuondoka. Yeye yupo hapa, anataka kucheza na kubakia na sisi na kuonyesha ubora wake ulivyo."

Awali ESPN iliripoti kwamba Navas alikuwa anataka kwenda sehemu anayopata nafasi ya kucheza mara kwa mara na wakala wake, Jorge Mendes tayari amesema uwezo wake wa kwenda PSG.

# Klopp: Timu za England hazitatawala tena Uefa

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp haoni kama timu za Uingereza zitatawala michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu na ameonyesha wasiwasi kama Liverpool itatetea taji hilo.

Timu zilizopo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ni imara na zina vikosi bora, amesema Klopp.

"Sitakuwa na tatizo kama watafika tena fainali, lakini wakati huu sidhani kama itatokea tena," amesema Klopp.

"Tuna nafasi sawa kama ilivyo kwa timu nyingine yoyote, lakini yote kwa yote, sioni kama timu za Uingereza zitapata nafasi kama msimu uliopita.

"Kutwaa tena Ulaya, sioni nafasi hiyo, na sidhani kama tutafanikiwa kwa hilo," alisema Klopp."

"Nidhani kama kutakuwa na timu imara zaidi kama ilivyo kwa ligi nyingine, naamini msimu huu itakuwa ngumu."

Klopp aliongeza kusema: "Angalia kikosi kama Borussia Dortmund nimekiona namna kilivyo bora msimu huu.

"Kwa uhakika safari hii changamoto itakuwa kubwa na nafasi za timu za Uingereza itakuwa kwenye wakati mgumu mno.




"Angalia timu kama Juventus, PSG zitakuwa pale. Real Madrid? Usifikiri haitakuwapo, kwani hawajakata tamaa kama watu wanavyodhani. Lakini pia kuna Bayern Munich iliyowanunua wachezaji kama (Ivan) Perisic na (Philippe) Coutinho ambao wamekiimarisha kikosi chao.

"Pia kuna Barcelona nao watakuwapo, naamini msimu huu watakuwa na njaa zaidi, kwani mashindano ya msimu huu kwa timu za Uingereza yanachangamoto nyingi."

## Ratiba raundi ya tatu Carabao hadharani

**LONDON, England**

BINGWA mtetezi wa kombe la Carabao, Manchester City itacheza na timu ya ligi daraja la kwanza Preston North End katika droo ya raundi ya tatu ya mashindano hayo iliyofanyika Jumatano.

Droo hiyo ilifanyika baada ya mechi zote za raundi ya pili kumalizika, ambapo ilishuhudia Everton ikiifunga Lincoln City, Leicester City ikaichapa Newcastle United kwa penalti na Sunderland ikaitoa Burnley.

Liverpool na Manchester United pia zitacheza raundi hiyo na timu za daraja la kwanza, huku wekundu hao wakisafiri kwenda Milton Keynes Dons na United itawakabili Rochdale.

Mechi nyingine zitawahusisha Arsenal watakaowakaribisha Nottingham Forest na Colchester United itacheza na Tottenham Hotspur.

Mshindi wa pili wa mashindano hayo msimu uliopita, Chelsea itacheza na Grimsby and Macclesfield ambao watacheza raundi ya tatu Septemba 10.

**Raundi hiyo ya tatu itachezwa Septemba 23 mwaka huu.**

**Ratiba kamili:**

Preston North End vs Man City
Milton Keynes Dons vs Liverpool
Man United vs Rochdale
Arsenal vs Nottingham Forest
Colchester vs Tottenham Hotspur
Chelsea vs Grimsby/Macclesfield
Sheffield Wednesday vs Everton
Wolverhampton Wanderers vs Reading
Oxford vs West Ham United
Watford vs Swansea City
Brighton & Hove Albion vs Aston Villa
Sheffield United vs Sunderland
Portsmouth vs Southampton
Burton Albion vs AFC Bournemouth
Luton Town vs Leicester City
Crawley Town vs Stoke City

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# OLE GUNNAR SOLSKJAER AMGEUKIA JADON SANCHO

**Afurahia Sanchez, Lukaku kuondoka Man United licha ya kukosa mbadala wa...**

**Manchester, England**

Ole Gunnar Solskjaer anajiandaa kusubiri hadi majira ya joto yajayo kuimarisha upya safu yake ya ushambuliaji, huku Jadon Sancho akiendelea kuwa lengo namba moja la Manchester United.

Kocha huyo raia wa Norway ni mwenye furaha kwa kuondoka kwa Romelu Lukaku na Alexis Sanchez, licha ya ufinyu wa mbadala katika safu ya ushambuliaji msimu huu.

Lakini hana mpango wa haraka wa kusajili mbadala wa dharura, kama Fernando Llorente ambaye ni mchezaji huru na amekiri itakuwa vigumu kupata mchezaji wa kiwango cha juu katika dirisha la dogo la Januari.

Sanchez jana alikuwa akijiandaa kukamilisha usajili wake wa mkopo wa muda mrefu wa kujiunga na Inter baada ya klabu hizo mbili kukubaliana na malipo juzi, Jumanne usiku.

Atajiunga na Lukaku katika dimba la San Siro, kufuatia nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji kusajiliwa na miamba hiyo ya Italia kwa pauni milioni 73 mapema mwezi huu.

Solskjaer alikuwa mkali akitaka angalau mmoja kati ya washambuliaji hao nafasi yake kuzibwa majira haya ya joto, lakini hatimaye alikuwa ni mwenye furaha kuwaruhusu kuondoka hata bila kupata mbadala.

Kuondoka kwao kumewaacha na washambuliaji watatu tu; Marcus Rashford na Anthony Martial kama washambuliaji wazoefu, na straika kinda Mason Greenwood, 17, akiwa ndiye mbadala.

Greenwood anaweza kujumuishwa kikosi cha kwanza mwishoni mwa wiki dhidi ya Southampton baada ya Martial kukumbwa na majeraha katika mechi iliyopita dhidi ya Crystal Palace.

Ni bahati nasibu kubwa kutoka kwa Solskjaer, ambaye amepewa jukumu la kuirejesha United katika utukufu wao wa zamani.

Lakini amekuwa akishawishika na uongozi wa klabu hiyo kwamba atapewa fungu kwa ajili ya kufanya 'fujo zaidi sokoni' ili kukibadili kikosi hicho alichokikuta, ambalo litajumuisha kurejea matamanio yake kuinasa huduma ya Sancho mwishoni mwa msimu.

Solskjaer alitaka kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa England kutoka Borussia Dortmund majira haya ya joto, lakini klabu hiyo iliweka wazi kuwa kinda huyo hauzwi.

Na kuanzia hapo alitia saini mkataba mpya na klabu hiyo ya Ujerumani, lakini hilo halijawa sababu ya kuiondoa United katika mbio hizo.

## KWA UFUPI

**PSG YAMCHELEWESHA NEYMAR**
Barcelona na Paris St-Germain zimekubaliana ada ya uhamisho kwa mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil, Neymar, 27, lakini mazungumzo bado yanaendelea kuhusu mkataba huo. PSG inataka mshambuliaji wa Barca, Mfaransa Ousmane Dembele, 22, kuwa sehemu ya makubaliano hayo. ***(Mirror)***

**DEMBELE AIGOMEA BARCA**
WAKALA wa Ousmane Dembele, 22, amesema mchezaji huyo hataondoka Nou Camp, jambo ambalo litasababisha dili la Neymar kutua Barcelona kuvunjika. ***(Daily Mail)***

**BAKAYOKO KWA MKOPO MONACO**
KIUNGO wa Chelsea, Mfaransa Tiemoue Bakayoko, 25, amekubaliana na malipo ya kujiunga na Monaco kwa mkopo, huku kukiwa na uwezekano wa kumnunua jumla kwa pauni milioni 31.8. ***(RMC Sport, via Sun)***

**NACHO AKARIBIA SOCIEDAD**
BEKI wa Arsenal, Nacho Monreal, 33, anaweza kurudi nchini kwao Hispania kabla ya dirisha la Ulaya kufungwa Jumatatu, wakati huu Real Sociedad ikiwa tayari kuinasa saini ya mchezaji huyo wa zamani wa Osasuna na Malaga. ***(Evening Standard)***

**ZIDANE KAMZUIA POGBA REAL**
Paul Pogba, 27, hakwenda Real Madrid kwa sababu kiungo huyo wa Manchester United na Ufaransa asingeendelea na kocha wa Los Blancos hao, Zinedine Zidane, ameeleza kocha aliyeibua kipaji chake. ***(Optus Sport via Goal)***

**LOVREN NJIA NYEUPE ROMA**
BEKI Dejan Lovren bado anaweza kuondoka Liverpool na kujiunga na Roma, wakati miamba hiyo ya Serie A ikiendelea kumhitaji nyota huyo wa kimataifa wa Croatia. ***(Corriere Dello Sport via Football.London)***

**KINDA ARSENAL AIVUTIA JUVE**
MSHAMBULIAJI wa Arsenal na England, Sam Greenwood, 17, ameivutia miamba ya Italia, AC Milan na Juventus katika michuano ya Ulaya U-17 mapema majira haya ya joto. ***(Sun)***

**SANCHEZ KUIGHARIMU UNITED**
Manchester United itamlipa Alexis Sanchez pauni 300,000 kila wiki kama sehemu ya mshahara wake wa pauni 400,000 katika kipindi chote atakachokuwa akiitumikia Inter Milan kwa mkopo. ***(Metro)***

**NAVAS ATAKA KUSEPA MADRID**
KIPA wa Real Madrid, Mcosta Rica Keylor Navas, 32, anatoa msukumo wa kujiunga na Paris St-Germain. ***(Mirror)***

**WERNER AFUNGUA MILANGO NJE**
MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig na Liverpool, Timo Werner, 23, bado hawezi kuweka kando kwenda kucheza soka nje ya Ujerumani kwa mbeleni, licha ya Mjerumani huyo kusaini dili mpya na miamba hiyo ya Bundesliga. ***(Mirror)***

**BEGOVIC KUONDOKA BOURNEMOUTH**
KIPA wa Bournemouth na Bosnia-Herzegovina, Asmir Begovic, 32, anaweza kuachana na klabu hiyo baada ya kupoteza nafasi kikosi cha kwanza kutoka kwa mlinda mlango Muingereza Aaron Ramsdale, 21. ***(Sun)***



HABARI MICHEZO

# MAYANGA ATOA SIRI 'KUIPAPASA' YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Ruvu Shooting, Salum Mayanga, amesema siri ya timu yake kufanya vizuri na kuweza kuanza Ligi Kuu kwa ushindi dhidi ya Yanga, ni nidhamu waliyonayo wachezaji wake pamoja na kuzingatia maelekezo aliyowapa.

Akizungumza na Nipashe juzi mara baada ya kumalizika kwa mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu dhidi ya Yanga, kocha huyo alikiri kuridhishwa na nidhamu na utulivu wa wachezaji wake nje na ndani ya uwanja na kufafanua kuwa hiyo ni moja ya siri ya ushindi katika mchezo huo.

"Siri ya mafanikio yetu ni nidhamu waliyonayo wachezaji kila mara na wasisitiza kuwa na nidhamu na leo imewasaidia," alisema Mayanga.

Alisema mapungufu machache ambayo aliyabaini kwenye michezo ya kirafiki, hayajajitokeza kitu ambacho kimempa matumaini makubwa ya kuendelea kufanya vizuri.

Alisema ataendelea kukipa kikosi chake mazoezi ya nguvu kuhakikisha kifanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yao.

"Nitaendelea na mazoezi kama kawaida kwa ajili ya kujiweka sawa na michezo ijayo lengo ni kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu," alisema kocha huyo.

Timu hiyo juzi iliifunga Yanga bao 1-0 katika dimba la Taifa jijini Dar es Salaam.

Bao la dakika ya 20 kupitia kwa Sadat Mohamed katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Uhuru juzi, lilitosha kuizamisha Yanga na kuifanya Ruvu Shooting kuanza vema Ligi Kuu msimu huu

MLIPAKODI...



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango (kulia), akimkabidhi mipira nahodha wa timu ya soka ya Naipanga Stars, Fred Daud, katika uzinduzi wa 'Wiki ya Mlipakodi na Tozo za Serikali' uliofanyika juzi wilayani Nachingwea ukiambatana na michezo mbalimbali ikiwamo soka. **MPIGAPICHA WETU**

## Watanzania wafundwa Jackpot ya SportPesa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubashiri ya SportPesa, imewataka Watanzania kucheza kwa kupitia kampuni hiyo kujaribu zaidi kwenye Jackpot kwani mtu yeyote ana nafasi ya kushinda mamilioni.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abbas baada ya Watanzania wawili kujishindia Sh. 825, 913, 640 ambao ni Kingsley Pascal na Magabe Marwa.

Washindi hao walishinda Jackpot wiki iliyopita kabla ya juzi kukabidhiwa mamilioni yao ikiwa ni baada ya kutabiri kwa usahihi mechi 13 kwa pamoja na kushinda Sh. milioni 825 ambazo waligawana kwa kila mmoja kuchukua kitita cha Sh. milioni 412.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Tarimba alisema ni wakati wa Watanzania kucheza kwa kasi ili wajishindie mamilioni hayo, kwani mtu yeyote ana nafasi ya kushinda.

Tarimba alisema kama SportPesa wanapenda kuona Watanzania wakishinda kwa ajili ya maisha yao kupitia ubashiri wao wa mechi mbalimbali zitakazochezwa.

Aliongeza kuwa kikubwa Watanzania waamini mshindi anayepatikana ni halali kwani katika kubashiri pia vigezo na masharti huzingatiwa kwa kuwa kubashiri mechi sio mchezo wa siri.

"Hiyo ni baada ya Pascal na Marwa wote kutoka mikoani kushinda Jackpot kubwa ya Sh. milioni 825 ambazo wamekabidhiwa jana Jumatano hundi ya fedha hizo.

"Hivyo niwatake Watanzania kuamini na kucheza na SportPesa kwa ajili ya kubadili maisha yao kwani kila mmoja ana nafasi ya kushinda pale atakapoweka utabiri mzuri wa mechi zake," alisema Tarimba.

# Uganda, Kenya hapatoshi fainali U-15

**Na Somoe Ng'itu, ASMARA**

YOSSO kutoka Uganda wanatarajia kukutana na wenzao wa Kenya katika fainali ya kwanza ya mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 15 ya Afrika Mashariki na Kati (U-15) itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Asmara nchini Eritrea.

Uganda ambayo imeshinda mechi zake zote za mashindano hayo kuanzia hatua ya makundi, imetinga hatua hii baada ya kuwafunga Burundi mabao 6-0 wakati Kenya yenyewe imefika fainali kwa kuwaondoa Rwanda kwa penalti 4-2 baada ya kutoka sare ya bao 1-1 katika dakika za kawaida.

Kocha Mkuu wa Uganda U-15, Magwera Jackson, ameliambia gazeti hili kuwa mechi hiyo kwao ni muhimu kama michezo mingine iliyotangulia katika mashindano haya yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati ( Cecafa).

Magwera alisema hana majeruhi katika kikosi chake na kila mchezaji amejiandaa kupambana ili kutimiza malengo ya kurejea nyumbani kwao na kikombe.

"Tumejiandaa vizuri, malengo yetu ni kushinda kikombe hiki, tutakuwa makini na tutaingia uwanjani tukiwaheshimu Kenya, si timu mbaya, tunatarajia ushindani katika mechi hiyo ya fainali," alisema Magwera.

Naye Kocha Mkuu wa Kenya U-15, Sal Lakhan, alisema kwanza anawapongeza wachezaji wake kwa hatua ambayo wamefikia na anaamini wataendelea kupata matokeo mazuri.

"Najua haitakuwa mechi rahisi kwetu, tumeiona Uganda katika mechi zake zilizopita, ni timu ngumu, lakini naamini wachezaji wangu watapambana, wamekuwa wakiimarika katika kila mechi wanayocheza, nimewaambia wawe watulivu zaidi kila wanapokuwa na mpira," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa kupitia mashindano haya, wachezaji wake wameimarika na wamejifunza mbinu mbalimbali, na anatarajia mwakani watakuwa bora zaidi na anaamini wanaweza kupandishwa katika kikosi kinachofuata cha vijana cha umri chini ya miaka 17.

Mechi hiyo itatanguliwa na mchezo wa kusaka mshindi wa tatu ambayo itawakutanisha majirani, Rwanda dhidi ya Burundi.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Cecafa, Nicholas Musonye, alisema maandalizi ya fainali hiyo yamekamilika na mgeni rasmi katika mechi ya leo atakuwa Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (Caf), Ahmad Ahmad.

Musonye amesema michuano hii imefanyika kwa mafanikio na anazipongeza timu zote 10 zilizoshiriki na kuwataka wanachama wote wa Cecafa kuendelea na maandalizi kwa ajili ya mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (U-20) yatakayofanyika baadaye mwezi ujao jijini Kampala, Uganda.

## Tanzania mwenyeji tamasha la Jamafest

**Na Gwamaka Alipipi**

TANZANIA inatarajia kuwa mwenyeji wa Tamasha la Utamaduni na Sanaa Afrika Mashariki (Jamafest) litakalofanyika kuanzia Septemba 21 hadi 28, mwaka huu katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe alisema tamasha hilo litashirikisha vikundi vya utamaduni kutoka nchi sita za Afrika Mashariki.

"Tamasha hili lilianzishwa mwaka 2011 nchini Rwanda na baadhi ya viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, watazamaji 17,500 walihudhuria, likafanyika Kenya na walihudhuria watazamaji 21,000, Uganda wakafuata kwa kuandaa, wakahudhuria watazamaji 46,500, sasa ni zamu yetu," alisema Dk. Mwakyembe.

Alisema kauli mbiu ya tamasha hilo ni 'Uainui wa kitamaduni, msingi wa utengemano wa kikanda, maendeleo ya kiuchumi na kushamiri kwa utalii".

Aidha, Dk. Makyembe alivitaka vyombo vya habari nchini kulitangaza tamasha hilo kwa kuweka uzalendo, pamoja na kuwaomba Watanzania, wasanii kujitokeza kwa wingi siku ya tukio ambapo alifafanua kuwa mbali na masuala ya sanaa, pia kutakuwapo na maonyesho ya kitalii yatakayofanyika sambamba na kupanda Mlima Kilimanjaro.

Michezo

Ijumaa Agosti 30, 2019

Nipashe



# Solskjaer amgeukia Sancho

HABARI UK 30

HESABU...



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, akipiga hesabu ya kumtoka beki wa JKT Tanzania, Mohamed Fakhi kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Vodacom iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jana na 'Wekundu wa Msimbazi' hao kushinda kwa mabao 3-1. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# SIMBA MOTO NDIO UMEANZA LIGI KUU

● ● ● Kagere, Miraji wawapigisha kwata 'wajeda' wa JKT Uhuru, waifuata Lipuli kileleni huku...

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Simba jana ilianza vema kampeni yake ya kutetea ubingwa wake baada ya kuichapa JKT Tanzania mabao 3-1 kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliopigwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Timu hiyo ambayo iliondolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Jumapili iliyopita, iliingia kwa dhamira moja tu ya kuwarudishia furaha mashabiki wake, ingeweza kuvuna mabao mengi kama wachezaji wake wangekuwa makini wanapofika golini.

Simba ilipata bao dakika ya kwanza tu ya mchezo likifungwa na mshindi wa Kiatu cha Dhahabu msimu uliopita, Meddie Kagere baada ya kupata pasi safi kutoka kwa Mzamiru Yassin.

Ingeweza kuwa na jumla ya mabao matatu kabla ya dakika 10 za mwanzo, kama Claotus Chama angekuwa makini, au angeacha uchoyo.

**Kipindi cha pili Simba iliingia kwa kufanya mashambulizi kwa kasi na dakika ya 58, Kagere tena alifunga bao la pili kwa shuti kali akiwa karibu na lango, baada ya pasi nyingine murua kutoka kwa Mzamiru.**

Kagere angeweza kufunga 'hat-trick' kama shuti lake lisingegonga mtambaa panya dakika chache baadaye.

JKT nusura ipate bao dakika ya 62 baada ya kombora la Danny Lyanga kupanguliwa na kipa Aishi Manula na kuwa kona ambayo haikuzaa kitu.

Bao la tatu la Simba lilifungwa na mchezaji iliyomsajili kutoka Lipuli FC, Miraji Athumani dakika ya 73, akiunganisha kwa kichwa krosi kutoka winga ya kulia ilinyunyuziwa na Kagere.

Wachezaji wa JKT Tanzania hawakukata tamaa kwani dakika tatu kabla ya mechi kumalizika, Edward Songo alifunga bao la kufutia machozi kwa shuti kali la mbali lililomshinda Manula na kujaa wavuni.

Kwa matokeo hayo, Simba na Lipuli FC ambayo iliifunga Mtibwa Sugar mabao 3-1 ndizo zinazoongoza ligi kwa sasa baada ya mechi ya raundi za kwanza.

## Zahera ashukiwa visingizio Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa Yanga wamemshukia Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Mwinyi Zahera wakimtaka kumulika matatizo yanayoikabili klabu hiyo badala ya kutafuta visingizio visivyo na maana wakati timu hiyo inapopoteza.

Baada ya Yanga kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Ruvu Shooting kwenye mechi yao ya ufunguzi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Uhuru juzi, Zahera aliitupia lawama Bodi ya Ligi, kwa kitendo cha kutoisogeza mechi hiyo mbele kufuatia kutoka kwenye majukumu ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika nchini Botswana.

"Jumamosi tumecheza dhidi ya Township Rollers ugenini, tukarudi Jumapili, lakini wenzetu Simba wamecheza hapa nchini [dhidi ya UD Songo Jumamosi], hata hivyo wao ratiba inaonyesha wanacheza Alhamisi [jana], wakati sisi tulikuwa ugenini tumerudi tumechoka tunapangwa kucheza Jumatano [juzi], hii si sahihi," alilalamika Zahera.

Hata hivyo, wakijadili uwanjani hapo katika vikundi mbalimbali vilivyokusanyika baada ya mechi, mashabiki hao waliojawa na sura ya huzuni walidai tatizo la timu si uchovu bali ni kushindwa kuwa na muunganiko mzuri hususan safu ya ushambuliaji.

"Lazima tukubali timu yetu haina mshambuliaji kama Makambo [Heritier], tumekosa nafasi nyingi na muunganiko wa timu bado, kulaumu suala la ratiba na uchovu hapo tunashindwa kulimulika tatizo na kwa namna hii hata kama tungecheza Jumamosi ijayo bado tusingeshinda," alisema Juma Abdallah.

Mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Nurudin Kassim, alisema: "Angalia hata aina ya mabao timu yetu iliyofunga mechi zilizopita, kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Kariobangi Sharks, tumepata sare tukisawazisha kwa penalti kisha jijini Arusha dhidi ya AFC Leopards tukafunga kwa faulo Ligi ya Mabingwa dhidi ya Township Rollers Uwanja wa Taifa tukasawazisha kwa penalti na kisha ugenini bao la faulo, hii inaonyesha kuna shida kwenye ushambuliaji."

Aidha, wamemtaka Zahera kuifanyia kazi safu ya ushambuliaji mapema kabla ya mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Zesco itakayopigwa Uwanja wa Taifa mwezi ujao, Septemba 13.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002